# UTAMADUNI
# WA
# MWAMKO WA KIJAMII

ثقافة النهوض الاجتماعي

**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hassan Musa al-Saffar

05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 1 8/27/2015 2:17:14 PM

ترجمة

# ثقافة النهوض الاجتماعي

تأ ليف

الشيخ حسن بن موسى الصفار

من اللغة العربية الى اللغة السواحلية

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
AL-ITRAH FOUNDATION

**ISBN:** 978 - 9987 – 17 – 027 – 2

**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hassan Musa al-Saffar

**Kimetarjumiwa na:**
Abdul-Karim Juma Nkusui

**Kimehaririwa na:**
Alhaji Hemedi Lubumba
Alhaji Ramadhani S. K. Shemahimbo

**Kimepitiwa na:**
Mubarak A. Tila

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Agosti, 2015
**Nakala:** 2000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com
**Tovuti:** www.ibn-tv-com
**Katika mtandao:** www.alitrah.info

# YALIYOMO


Dibaji ........................................................................ vi
Neno la Mchapishaji ........................................................ 1
Utangulizi.......................................................................... 3
Jamii na Kutengeneza Mtazamo ........................................ 7
Fursa Zilizopo ................................................................. 11
Taasisi za Kutengeneza Rai ............................................ 12
Wingi wa Rai na Chaguo ................................................ 13
Mkakati wa Nchi na Juhudi za Amani ............................. 15
Kuanzisha Uvumilivu wa Kidini ..................................... 19
Dini ya Makuzi ya Kifamilia ........................................... 22
Mazingira ya Kijamii ni Mlezi wa Dini .......................... 24
Ugonjwa wa Kasumba na Maslahi .................................. 27
Mtazamo wa Qur'ani ....................................................... 28
Qur'ani Iliyohamwa.......................................................... 33
Wameifanya Qur'ani Mahame.......................................... 34
Madhumuni ya Qur'ani na Mfumo Wake ......................... 35
Ratiba ya Maisha.............................................................. 40
Kutazama Katika Kitabu cha Ulimwengu ....................... 41
Mifumo ya Uhusiano wa Kijamii .................................... 45
Vijana na Kurejea kwenye Qur'ani................................... 49
Harakati za Utambuzi na Maarifa Katika Jamii............... 55
Maarifa na Utambuzi Katika Maisha ya Mwanadamu ..... 56
Utambuzi wa Kidini.......................................................... 58
Mtazamo wa Dini.............................................................. 60
Kujielimisha .................................................................... 62

Harakati za Kujielimisha ..... 63
Uwezo na nguvu ..... 64
Ustawi wa Maarifa na Utoaji wa Wananchi..... 66
Jukumu la Mwamko..... 70
Kujitolea Katika Jambo la Umma ..... 73
Kutilia Umuhimu Mambo ya Utamaduni ..... 75
Al-Babatin ni Mfano wa Kuigwa ..... 76
Wakfu za Kukuza na Kustawisha Maarifa ..... 78
Mageuzi ya Kijamii na Kipengele cha Wakati..... 81
Makundi ya Kijamii na Ushindani Mzuri ..... 86
Wingi ni Hali Nzuri ..... 87
Uhusiano Baina ya Makundi ya Kijamii ..... 89
Vipi Uratibiwe Muundo wa Uhusiano Baina ya Makundi ..... 90
Makundi ya Kijamii na Kuboresha Uhusiano ..... 92
Kujitolea Katika Kuhudumia Jamii ..... 95
Kukuza Utashi wa Kheri..... 96
Kulingania Kheri..... 98
Kwenda Mbio na Kufuatilia..... 100
Kujitolea Katika Amali ya Kheri ..... 101
Msomi na Jukumu la Kudhihirisha Rai ..... 104
Kufuta Utu wa Mtu Binafsi..... 107
Istikhara na Kusitasita Katika Maamuzi..... 112
Akili na Uendeshaji wa Maisha ..... 113
Kufaidika na Akili za Wengine ..... 117
Nafasi ya Istikhara ..... 119
Anwani ya Mtunzi..... 124

# DIBAJI

Kitabu hiki ni toleo la Kiswahili la taasisi ya Al Itrah Foundation. Chapisho lake limelenga kukidhi mahitaji ya kiroho ya zama hizi pamoja na Ubongo na fikra zinazokuwa za Muislam. Jitihada kub wa zimefanywa na Taasisi kuweka chapisho hili la Kiswahili katika msingi wa haki na wenye kukubalika katika Uislam.

Unaombwa kwa Taadhima ukisome kitabu hiki katika malengo yaliyokusudiwa. Pia Unaombwa kuwasilisha kwetu maoni yako huru juu ya chapisho letu hili, jambo ambalo tutashukuru sana.

Kutangaza ujumbe wa Uislam ni kazi ambayo inahitaji ushirikiano wetu sote. Taasisi inakuomba kuungana na kushirikiana kama ilivyoagizwa katika aya ya Qur'an: (Surat Saba' 34:46).

Na rehma za Allah ziwe juu yako.

Wako katika Uislam
Al Itrah Foundation
Barua Pepe: alitrah@yahoo.com
SMS: +255 778 300 140



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 6 8/27/2015 2:17:14 PM

بسم الله الرحمن الرحيم

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako ni tarjuma ya Kiswahili ya kitabu cha Kiarabu kiitwacho, *Thiqafatu 'n-Nahdhi 'l-Ijtima'iyyi,* kilichoandikwa na Sheikh Hasan Musa as-Saffar. Sisi tumekiita, *Utamaduni wa Mwamko wa Kijamii.*

Utamaduni *(thiqafah)* maana: ni kukua na kukomaa kwa fikra na mwili wa mwanadamu kutokana na mafunzo na uzoefu wa kufanya kazi. Maana nyingine: ni hali ya maendeleo ya maarifa, elimu ya watu, ustaarabu, fani zote (za kielimu), imani, mila, desturi na asasi za kijamii zitambulishazo jamii. Kwa ujumla, hii ndio maana ya utamaduni kama ilivyofasiliwa katika Kamusi ya TUKI.

Uislamu ni mila na utamaduni ulioletwa na Mitume waliotumwa na Mwenyezi Mungu ili kuwafundisha wanadamu mila na utamaduni huu. Kama maana ya neno utamaduni inavyoonesha hapo juu, Uislamu umeletwa ili kuuboresha na kuukamilisha utamaduni huo. Mitume wote waliotumwa na Mwenyezi Mungu (takriban 124,000) kuanzia Mtume Adam mpaka Mtukufu Mtume Muhammad, kazi yao ilikuwa kufundisha utamaduni huu wa Kiislamu katika nyanja zote za maisha ya mwanadamu - kimwili na kiroho. Ndio maana tunasema: "Uislamu ni mfumo kamili wa maisha."

Mwandishi wa kitabu hiki anaelezea kwa uzuri kabisa kuhusu utamaduni huu kwa kutaja vipengele muhimu kwa kurejea katika Qur'ani Tukufu, Sunnah, historia ya Kiislamu na matukio yake, n.k.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 1 8/27/2015 2:17:14 PM

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya kielimu ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi tena katika akili za watu.

Kutokana na ukweli huu, taasisi yetu ya Al-Itrah imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu Alhaji Abdul-Karim Juma Nkusui kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kukitarjumi kitabu hiki kwa Kiswahili kutoka lugha ya asili ya Kiarabu. Aidha, tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na kesho Akhera – Amin.

**Mchapishaji**
**Al-Itrah Foundation**



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 2 8/27/2015 2:17:14 PM

بسم الله الرحمن الرحيم

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mola mlezi wa viumbe. Ewe Mwenyezi Mungu mteremshie rehema hitisho la Manabii na ukamilisho wa Mitume, na kizazi chake kitwaharifu na masahaba wake wema.

بسم الله الرحمن الرحيم

# UTANGULIZI

Jamii haitavuka hali yake ya kutokuendelea maadamu watu wake hawajashiba utamaduni unaowasukuma kuelekea kwenye mabadiliko na mwamko. Hiyo ni kwa sababu nyuma ya kila hali inayoishi nayo jamii kuna utamaduni unaoimarisha hali hiyo na kuutetea na kuuhami. Qur'ani tukufu imeshaeleza ukweli huu dhahiri shahiri ambapo inasema:

إِنَّ ٱللَّهَ لَا يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتَّىٰ يُغَيِّرُوا۟ مَا بِأَنفُسِهِمْ ﴿١١﴾

**"Hakika Mwenyezi Mungu habadilishi yaliyopo kwa watu hadi wabadilishe yalimo katika nafsi zao." (Sura Ra'ad: 11)**.

Na yaliyomo katika nafsi ni utamaduni ambao unatengeneza hisia na kutengeneza misimamo ya kitabia. Na ujumbe wa mbinguni



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 3 8/27/2015 2:17:15 PM

ulikuwa unawakilisha utamaduni wa mabadiliko na mwamko ambao walikuja nao Manabii kwa umma zao ili kuamsha yaliyofichikana katika akili zao na ili kukomboa matakwa yao kutokana na minyororo na hali ya kutoendelea. Ili waanze kuimarisha ardhi na kujenga jamii tukufu yenye maendeleo.

Na hivyo haikuwa ni kulingania tu itikadi ya moyoni na nembo za kiibada, zisizokuwa na mwingiliano wa kimaisha. Na kama ingekuwa hivyo basi wasingepigwa vita na watawala na mafisadi. Hakika ulinzi wenye nguvu wenye kutawala katika jamii katika utamaduni na mfumo wa waliotangulia ulikuwa dhidi ya ujumbe wa Manabii, kwa sababu utamaduni huo uliorithiwa ndio ambao ulikuwa unadhamini kuendelea kwa hali iliyokuwepo, na unahami maslahi yao na kuimarisha nguvu yao. Anasema (swt):

وَكَذَٰلِكَ مَآ أَرۡسَلۡنَا مِن قَبۡلِكَ فِي قَرۡيَةٖ مِّن نَّذِيرٍ إِلَّا قَالَ مُتۡرَفُوهَآ إِنَّا وَجَدۡنَآ ءَابَآءَنَا عَلَىٰٓ أُمَّةٖ وَإِنَّا عَلَىٰٓ ءَاثَٰرِهِم مُّقۡتَدُونَ ٢٣

**“Na kadhalika hatukumtuma mwonyaji kwenye mji wowote ila wapenda anasa wake walisema: Hakika sisi tuliwakuta baba zetu juu ya desturi na tunafuata nyendo zao.” (Sura Zukhuruf: 23)**.

Hakika wao wanaogopa utamaduni mpya kwa sababu unawapa watu hali ya kujiamini na kuwashajiisha katika kufikiri na kuchukua misimamo, kutumia matakwa, na kwa hiyo inafungua mbele ya watu njia ya mageuzi na mwamko, na wanavuka udhibiti wa watawala na wenye kiburi.

Hakika kazi ya msingi ya utamaduni wa kutoendelea ni kuwakinaisha watu kujisalimisha kwenye hali wanayoishi nayo, katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii, kwa madai kwamba



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 4 8/27/2015 2:17:15 PM

hiyo ndio hali bora zaidi, au kwa kisingizio cha kutokuwa na uwezo wa kubadilisha au kwa sababu hayo ndio ambayo yanaamrishwa na dini, na kwamba jaribio lolote la mageuzi linaweza kuleta hatari katika uwepo wa dini na maadili ya kitabia, na hicho ndicho kisingizio alichokitangaza Firaun ili kulinda uovu wake. Anasema (swt):

وَقَالَ فِرْعَوْنُ ذَرُونِيٓ أَقْتُلْ مُوسَىٰ وَلْيَدْعُ رَبَّهُۥٓ ۖ إِنِّيٓ أَخَافُ أَن يُبَدِّلَ دِينَكُمْ أَوْ أَن يُظْهِرَ فِي ٱلْأَرْضِ ٱلْفَسَادَ ﴿٢٦﴾

**"Na Firauni akasema: Niacheni nimuuwe Musa, naye amwite Mola Wake! Hakika mimi nachelea asije kubadilisha dini yenu, au adhihirishe uharibifu katika nchi." (Suratu AL-MU'MIN: 26).**

Na miongoni mwa aina mbaya mno za utamaduni wa kutoendelea ni utamaduni unaonasibishwa na dini, na ambao unapotosha maneno ya dini katika kuwekwa kwake, na kuipuuza Qur'ani. Yanachukuliwa yale yasiyodhuru maslahi ya nguvu za kutoendelea, kama nembo ya ibada, na kuachwa yale ambayo yanalingania kwenye marekebisho, kusimamisha uadilifu na kutimiza haki. Na haya ndio mambo ambayo wananchi wetu wengi wa nchi za Kiislam wanakabiliwa nayo, ambao wananyenyekea utamaduni unaoimarisha hali ya kutoendelea na kuihami kwa jina la dini.

Hivyo miongoni mwa madhumuni ya kwenda mbio kuvuka hali ya kutokuendelea ni kusheheni utamaduni sahihi unaosukuma jamii kuelekea kwenye mageuzi na mwamko na kuiongoza kwenye ustawi na maendeleo. Utamaduni unaowarejeshea watu kujiamini na kwamba wao wanaweza kufanya na kubadili, na kwamba wao ndio wenye jukumu la hali wanayoishi nayo. Utamaduni unaowasukuma kwenye kutafakari na kuendeleza akili zao na kuwakomboa kutokana



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 5 8/27/2015 2:17:16 PM

na ukhorafi (imani zisizo na uhalisia zinazoingizwa kwenye dini), dhana na ngano, kwa kuangalia kanuni za ulimwengu na maisha, na kuvumbua wigo wa elimu na maarifa, na kunufaika kutokana na uzoefu wa umma na wananchi wengine.

Utamaduni unaoeneza upendo baina ya watu na kuwashajiisha katika kusaidiana baina yao na kuondoa mifundo, chuki na vikwazo vya kutengeneza ili juhudi na nguvu zishirikiane kwa ajili ya kufanikisha mipango katika kustawisha jamii na kuleta miradi ya kujenga na kuboresha.

Na mbele ya msomaji mtukufu kuna maneno machache yanabeba kiasi kidogo katika utamaduni unaotakikana, nimeyaandika katika nyakati mbalimbali, ndani ya mapito ya harakati za ushirikiano wa kijamii. Nataraji kutakuwepo humo yale ambayo yanaunga mkono juhudi za warekebishaji na wenye kushughulika kwa ajili ya maslahi ya dini na jamii. Na Mwenyezi Mungu ndio mwenye kuwafikisha.

**Hasan Musa as Saffar**
**20 Dhul-Hijjah 1432 Hijiria / 16 Novemba 2011**



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 6 8/27/2015 2:17:16 PM

بسم الله الرحمن الرحيم

# JAMII NA KUTENGENEZA MTAZAMO

Jamii ya kibinadamu na hususan katika nyakati za matatizo na shida, inahitajia sana kupevuka katika rai na uwazi wa mtazamo, kwa sababu hilo linasaidia sana katika kuvuka matatizo na kuvuka shida, rai iliyopevuka na mtazamo ulio wazi unaelekeza mwelekeo wa jamii katika njia na mwendo bora zaidi, na hivyo haupotezi juhudi na nguvu isipokuwa katika yenye kuleta faida na manufaa yanayofaa kuhudumia maslahi ya jamii. Na kwa ajili hiyo imepokewa kutoka kwa Amirul-Muuminina Ali عليه السلام kwamba amesema: "Hakuna harakati yoyote isipokuwa unahitaji kuwa na maarifa nayo."[1]

Na Imamu as-Sadiq عليه السلام anamhadharisha mwenye kutoa juhudi bila maarifa kwamba anaweza kupoteza lengo lake badala ya kulitimiza. Anasema عليه السلام katika yaliyopokewa kutoka kwake: "Mwenye kutenda bila ya uoni ni sawa na mwenye kwenda bila ya kujua njia na kwenda kwake mbio hakumzidishii isipokuwa kuwa mbali zaidi."[2]

Na tangu zamani amesema mshairi Abu Twayib al-Mutanabi:

"Rai kabla ya ushujaa ni ushujaa, hilo ndio la kwanza na ushujaa ndio nafasi ya pili."

---

[1] Muhammad Baaqir al-Majilisiy katika *Biharul-Anuwar,* Juz. 74, Chapa ya Tatu 1403 Hijiria, (Beirut: Daru Ihiyai Turathil-Islaamiy) Uk. 267.

[2] Muhammad bin al-Hasan al-Hurr al-Amiliy katika *Wasailu Shi'a,* Juz. 27, Chapa ya Kwanza 1413 Hijiria, (Beirut: Muasasatu Aal Bait) Uk. 24.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 7 8/27/2015 2:17:16 PM

Ushujaa katika mahala pake panapofaa unaleta matunda makubwa, hivyo utumiaji nguvu huambatana na maamuzi ya kisiasa, na taasisi za kijeshi zinatoa kipaumbele katika upande wa utafiti na mbinu. Huu ndio ukweli haukatai wala haujadili mwenye akili timamu, hakuna anayesimama kutenda kitendo na harakati bila ya kutafakari na kujua mbinu na lengo lake, au bila kupanga njia ya kuliendea, lakini sisi tunapozungumzia juu ya mambo ya jamii, kutengeneza rai na mtazamo wa kulielekea jambo, tunahitaji kutazama nukta na angalizo kadhaa:

**Nafasi ya Wataalamu:**

Wataalamu wa kila jamii wao ndio wenye vipaji na ndio sehemu ya nguvu na uwezo, miongoni mwa maulamaa wa kidini, wataalamu, wasomi na wafanyakazi. Jopo hili, kutokana na wanayoyamiliki miongoni mwa vipaji, maarifa na ujuzi wa kivitendo, ndio lenye jukumu kwa daraja la kwanza katika kutengeneza rai na kutengeneza mtazamo kuhusu mambo ya jamii na matatizo yake. Lakini kwa masikitiko makubwa wengi kati ya watu wa kundi hili hawaoni nafsi zao kuwa ndio wenye kuhusika na utafiti wa kudurusu mambo ya jamii yao na kujitahidi katika ufumbuzi na utatuzi, ama kwa kushughulika na mambo binafsi au kwa udhaifu wa kujali shida za watu.

Na inawezekana kuwa baadhi yao kuna mwenye rai lakini hataki kubeba jukumu la rai yake na hivyo hadhihirishi kwa kujihadhari na kupingwa na upande huu au ule, au kujikuta nafsi yake anatakiwa kutekeleza jukumu fulani kutokana na rai yake. Kisha tatizo jingine linatokana na kukosekana uoni na ratiba ambayo itaweza kuwakutanisha watu wa jopo hili, ili washauriane na kujadili katika kuboresha fikra na kuivisha, kusaidiana katika kuifanyia kazi, kwa kuiga jamii nyingine ambazo katika jamii hizo kumeandaliwa



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 8 8/27/2015 2:17:16 PM

sehemu za kukutania taasisi zinazokusanya maulamaa wa kidini, wasomi, wanaharakati wa kisiasa na wa kijamii.

Hakika wataalamu kuacha nafasi yao ya kuongoza katika shughuli za kijamii kunarefusha muda wa mateso ya jamii na kutoa nafasi ya kujitokeza mielekeo inayoweza kukosa hekima au upevu, jambo ambalo linaleta madhara katika maslahi ya jamii na mustakabali wake. Na katika watu wa jopo hili kuna ambaye anaweza kuwa na mchango hasi dhidi ya shughuli za kijamii, hatoi rai wala hafanyi jukumu lake, hivyo ili kutoa kisingizio cha kuzembea kwake anadadisi kujitolea kwa wengine na mapendekezo yao.

**Jukumu la Jamii:**

Ikiwa jopo hili la wataalamu na wasomi ndio lenye jukumu kwa daraja la kwanza katika kutengeneza rai na mtazamo, hakika hiyo haimaanishi watu wengine wa jamii wameepukana na jukumu na wajibu wao, wanajamii wote ni washirika katika yanayofungamana na mambo yao ya jamii, hayamhusu mmoja bila ya mwingine, wote ni wenye wajibu juu ya hali mbaya ambayo wanaishi nayo na wanatakiwa kuibadilisha na kuirekebisha.

Anasema (swt):

وَٱلْمُؤْمِنُونَ وَٱلْمُؤْمِنَٰتُ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَآءُ بَعْضٍ ۚ يَأْمُرُونَ بِٱلْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ ٱلْمُنكَرِ ﴿٧١﴾

**"Na waumini wanaume na waumini wanawake ni marafiki wao kwa wao; huamrisha mema na kukataza maovu." (Sura Tawba: 71)**.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 9 8/27/2015 2:17:16 PM

Imepokewa kutoka kwa Mtume ﷺ kwamba amesema: "Ninyi nyote ni wachunga na nyote mtaulizwa juu ya mlichokichunga."[3] Na Mwenyezi Mungu alipoisifu jamii ya waumini kwa kushauriana kwa kauli yake (swt): **"Na jambo lao ni shura baina yao."** Hakika hakufunga suala la kushauriana katika kundi maalumu.

Na Mwenyezi Mungu alipomwamuru Nabii Wake ﷺ katika kushauriana akasema (swt): **"Na washauri katika jambo."** Hakika hilo linawajumuisha Waislamu wote, na kwa hiyo Mtume ﷺ alikuwa anawahutubia Masahaba wake wote kwa kusema: "Mshaurini Ali."[4]

Mwenyezi Mungu amempa kila mwanadamu akili ili atafakari kwayo, na inaweza kuzalika fikra muhimu kutoka katika akili ya mtu wa kawaida, na yeyote kati ya watu wa kawaida anaweza kuzindua jambo hatari ambalo hakuzinduka kwalo mwingine asiyekuwa yeye, kama ilivyosemwa: "Elimu yote iko katika ulimwengu wote." Na anapokea Hasan bin Jaham, amesema: "Tulikuwa kwa Imam Ridhaa عليه السلام tukamtaja baba yake, akasema: "Akili yake ilikuwa hailinganishwi na akili nyingine, lakini kuna wakati alikuwa akiwataka ushauri watumwa wake, siku moja akaambiwa: 'Unamtaka ushauri mtu kama huyu?' Akasema: Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu huwenda ameweka utatuzi katika ulimi wake."[5]

Na anaashiria Amirul-Muuminina Ali عليه السلام dharura ya kusaidiana baina ya wanajamii, hivyo asihisi yeyote vyovyote itakavyokuwa nafasi yake kujinyanyua na kutosheka na nguvu nyingine, wala asimdharau yeyote katika kuchangia jambo la jamii. Anasema ﷺ: "Mtu yeyote hata kama ana cheo kikubwa sana na ana fadhila kubwa

---

[3] *Biharul- An'war*, Juz. 72, Uk. 38.

[4] Alau Diyn Ali al-Mutaqiy al-Hindiy katika *Kanzul-Ummaal*, Chapa ya Tano 1985, (Beirut Muasasatu Risala) Uk. 484, Hadithi ya 30153.

[5] *Wasailu Shi'a*, Juz. 12, Uk. 45, Hadith 15602.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 10 8/27/2015 2:17:16 PM

sana katika dini, asione vibaya kuhitajia msaada katika wajibu aliobebeshwa na Mwenyezi Mungu. Na hata kama anadharauliwa na nafsi na kupuuzwa na macho asione vibaya kusaidia katika wajibu huo au kusaidiwa juu ya wajibu huo."[6]

Na ikiwa kulikuwa na tofauti kubwa ya kimaarifa katika wakati uliopita baina ya wataalamu na watu wa kawaida, hakika masafa hivi sasa yameshapungua kwa kiasi kikubwa ambapo elimu imeenea na njia za maarifa na utambuzi zimeenea na kimenyanyuka kiwango cha kujiamini. Jambo ambalo limepelekea kupanuka wigo wa ushiriki wa wananchi katika jambo la kijamii, na haya ndio yanayopatikana katika nchi zilizoendelea ambapo watu wanashiriki katika kuchukua maamuzi yanayofungamana na hali yao, na wanaipigia kura katiba ya nchi yao na wanachagua viongozi wao wa kisiasa na wanachagua wawakilishi wao wa kisharia na wasimamizi na kamati ya utendaji. Na wala hasiti mwananchi yeyote katika nchi hizo kutoa rai yake katika jambo la umma mbele ya vyombo vya habari.

**Fursa Zilizopo:**

Hivi sasa tunaishi zama ambazo humo kumeenea njia zinazosaidia kutengeneza rai, na humo kumetolewa fursa za kutoa rai, maalumati mengi juu ya masuala ya kijamii na mambo yake yametolewa na yako wazi kwa anayetaka kuyaangalia. Na ujuzi wa kutafiti na kuchambua unawezekana kupatikana kwa yeyote anayeutaka kupitia vipindi ambavyo vinatangazwa na vyombo mbalimbali vya habari na taarifa. Na hakujabaki vikwazo vikubwa vinavyozuia kutoa rai, ambapo mwanadamu kupitia chumba chake cha kulala anaweza kusambaza rai zake na kuzitangaza katika sehemu zote za dunia kupitia tovuti (na sasa simu za mkononi).

[6] Sharifu Ridhaa katika *Nahjul-Balaghah*, Khutba ya 217, Chapa ya Kwanza 1387 Hijiria, (Beirut Darul- Kitabi al- Libnaany), Uk. 234.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 11 8/27/2015 2:17:16 PM

Na mamlaka za usalama na siasa haziwezi tena kukandamiza rai na kuzizuia, kama ilivyokuwa mwanzo. Haya ni mazingira mwafaka na fursa nzuri ingawa sio kwa namna ya jumla, nyudhuru zote na visingizio vinapukutika, ambavyo baadhi wanaviegemea ili kuzembea katika kushiriki katika mambo ya umma, wakati vilipasa viwe ni msukumo wa kupanua wigo wa ushiriki na kushikamana kwa ajili ya kuhudumia mambo ya kijamii.

**Taasisi za Kutengeneza Rai:**

Kwa juhudi za uongozi na juhudi bora za wananchi kumeanzishwa katika jamii taasisi zinazojali shughuliza za kidini, kiutamaduni na kijamii, miongoni mwa shule za kidini, jumuiya za kheri, vitengo vya kiutamaduni na jumuiya zinazojali matukufu ya kimadhehebu.

Na jamii katika hatua hii katika mabadiliko yake inahitajia taasisi za maarifa zinazohudumia watengeneza rai, kama vile vituo vya taarifa na taasisi za utafiti na uchunguzi wa kijamii na kufanya makongamano makubwa. Hakika sisi tuna haja ya kuwa na kanuni ya ubainifu na maalumati yanayojali mambo mbalimbali ya jamii kama vile ufakiri na ukosefu wa kazi, na ambayo yanaambatana na usalama wa kitabia na kijamii, na matatizo ya ubaguzi wa kimakundi.

Mambo yote haya na mfano wake yanahitaji hazina ya nyaraka ambazo hawezi kuziepuka yule mwenye kutengeneza rai na kuchukua maamuzi. Kama ambavyo sisi tuna haja ya kuwa na vituo vya utafiti na uchunguzi katika uzio wa kielimu na kimaudhui, na kuvutia vipaji vya ubobezi katika nyanja zake.

Na ikiwa yatatimia mazingatio katika nyanja hii muhimu, itajitokeza hali ya kujitolea kuelekea upande wake, kama ambavyo ilivyotokea katika nyanja nyingine, na kama mwelekeo wowote mpya, mwanzo unaweza kufunikwa na haiba na woga, lakini



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 12 8/27/2015 2:17:16 PM

matakwa na kujitolea vitawavusha wenye kujitolea na kuwawezesha kuvuka yote hayo.

**Wingi wa Rai na Chaguo:**

Ni kawaida kuwa na rai mbalimbali katika jamii na kuwa na hiyari nyingi mbele ya mambo muhimu kutokana na kutofautiana mielekeo na maslahi, na pia kwa sababau ya kutofautiana mitazamo na uchambuzi katika kuainisha uhalisia au matarajio ya baadaye. Na wala haiwezekani kwa yeyote kuhodhi haki ya kutoa rai au kulazimisha maamuzi yake katika jamii, kama ambavyo ni haki kwake kutoa rai yake na kufanya kazi kwa msingi wake, hakika na wengine wana haki hiyo hiyo. Lakini baadhi wanakereka kwa rai za wengine, na kufanya rai yake kama vile ndio chaguo pekee mbele ya jamii, hakuna suluhisho ila ndani ya rai yake, na hakuna kheri ila humo, na anaelekeza mishale ya ukosoaji, kupuuza na kuporomosha rai nyingine na kuwakebehi wale wanaozifuata.

Hakika kutoa maoni ni haki ya kisharia, na kukosoa rai nyingine ni jambo linalokubaliwa, lakini kupuuza rai ya mwingine na kuwatukana wanaozilingania, ni jambo linalokataliwa na ni tabia mbaya, inayodhihirisha ghuri na chuki. Na miongoni mwa maradhi hatari ya kudumu katika jamii zetu ni kuamiliana vibaya na rai za upande wa pili. Katika upande wa dini mtu anatuhumiwa kwa uasi, upotovu na kuzua, na katika upande wa kisiasa anatuhumiwa kwa hiyana na ukibaraka. Nazo ni tuhuma ambazo inawezekana upande wowote kuzielekeza kwa upande mwingine, kila upande una kiwango cha uwezo wa kuathiri kama alivyosema mshairi wa Kiarabu:

**"Alikuja Darid amechomoa upanga wake, hakika watoto wa ami yako nao pia wana mikuki."**



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 13 8/27/2015 2:17:16 PM

Lakini hilo linaigeuza jamii kuwa uwanja wa mizozo na vita ya ndani badala ya kuelekeza nguvu na juhudi katika upande wa maadui na katika kuhudumia mambo ya jamii. Hakika kutilia shaka nia na kutuhumu makusudio, ni uadui na ni kuvunja heshima ya wengine na ni kushindwa kukosoa maudhui katika rai ya mwingine na kumkinaisha kwa rai yako. Ni wajibu wetu kujaribu kuwa na rai nyingi na kutoa fursa ya kuchangamsha fikra ya kijamii na kufungua chaguo nyingi kwa njia ya kupokea vipaji vya jamii, na kuboresha ushindani mzuri na moyo wa kujitolea ndani ya kundi la wajuzi na watu wa kawaida.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 14 8/27/2015 2:17:16 PM

# MKAKATI WA NCHI NA JUHUDI ZA AMANI

Hakuna shaka kwamba mafanikio ya kisiasa ambayo yamepatikana kwa kitendo cha mapinduzi ya Mwamko wa Nchi za Kiarabu ni mafanikio makubwa na maamuzi muhimu, inatarajiwa kuwa ni vazi na ufunguzi wa kheri katika zama mpya, humo wananchi wa sehemu hizo wanapata matarajio yao katika uhuru, uadilifu na ustawi. Na mambo ambayo inatupasa kusimama kwa ajili ya kuyatafakari ni yale ambayo yamedhihirishwa na harakati pana za wananchi miongoni mwa maendeleo katika kiwango cha utambuzi na kufikiri kwa umma. Na ambayo yametengeneza mwenendo wa pamoja wa kimaendeleo kiasi cha kuwashitusha wachunguzi na wafuatiliaji katika kiwango cha kimataifa.

Nchi zetu za Kiarabu zimeishi kwa muda mrefu katika vita kali vya kifikra, na humo watu wamegawanyika katika kambi mbalimbali, wanapigana wao kwa wao na wanashughulika na mijadala na midahalo kuhusu haki ya dini hii, na ubatili wa dini ile, usahihi wa madhehebu hii na upotovu wa madhehebu ile, usahihi wa nadharia hii na ubaya wa nadharia ile. Kushughulika huku na tofauti hizi za kifikra ilikuwa ni kwa gharama ya kutojali hali mbaya ambayo wanaishi nayo na wanateseka nayo wanajamii wote bila kujali mirengo yao ya kidini na kifikra. Wote wanakabiliwa na udikteta wa kisiasa na kibano cha maisha magumu na kuanguka kwa maendeleo katika nchi zao, na kutoendelea kielimu, kifikra, kitekenolojia na kutawaliwa na nguvu za wageni.

Na badala ya kushughulika na kukabiliana na changamoto hii ya zama, kila upande unaishi na changamoto ya kupigana na upande



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 15 8/27/2015 2:17:16 PM

mwingine na unakwenda mbio kurekodi ushindi juu yake kwa kuingia katika vita vya ikhitilafu ya kifikra na uchochezi wa kimatangazo na kuhamasisha chuki na bughudha ya kulipizana. Vipaji vimepotea katika vita na mizozo na juhudi zimesambaratika, na nyoyo na nafsi zimejaa chuki na mifundo, baadhi ya medani zimeteleza hadi kwenye medani ya vita na kutumia mabavu baina ya vyanzo vyake. Na hali hiyo mbaya ilikuwa ndio sababu ya kuimarisha hali ya kutoendelea na kubakia katika ukandamizaji na kuenea ufisadi.

Sauti za warekebishaji zimekaribia kukatika, wanalingania umma katika umoja na mshikamano na kuvuka ikhitilafu na migawanyiko, warekebishaji walikaribia kukata tamaa ya watu wa umma kuitikia wito wao, nao ndio wito wa Qur'ani na wito wa akili, na ndio siri ya wananchi kusonga mbele. Mara yakaja mapinduzi ya mwamko ili kuhuisha matumaini na kuhuisha nafsi. Hawa ni wananchi wa nchi za Kiarabu katika zaidi ya nchi moja, wanafanya harakati za kupambana na udikteta na kutaka haki zao za kisharia, heshima, uhuru na uadilifu, kwa kuepuka mizozo ya kiitikadi, ikhitilafu za kifikra na mihimili mbalimbali ya kisiasa.

Na katika mtiririko huu medani ya uwanja wa Tahriri huko Misri imetoa kigezo na mfano mzuri, ambapo Wamisri walishikamana Waislamu kwa Wakristo, Waislamu kwa Waliberali, Masufi na Ikhwanul-Muslimina, na Wajamaa, na kutoka katika makundi na mihimili mbalimbali ili kutoa sauti moja na ili kusisitiza mahitaji ya pamoja yanayounganisha maslahi yao ya pamoja, na kuitikia utambuzi wao wa kitaifa na kugusa maisha ya kila Mmisri vyovyote itakavyokuwa dini yake au madhehebu yake au mrengo wake. Na kabla ya mapinduzi ya Misri kulikuwa na mapinduzi ya Tunisia, na yalifuata mfumo huu wa kimaendeleo ambao umekuwa ni mfumo wa mapinduzi mengi ya mwamko wa nchi za kiarabu.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 16 8/27/2015 2:17:16 PM

Na huwenda mwonekano muhimu zaidi katika mapinduzi haya mazuri ya wananchi ni kushikamana kwao na mfumo wa amani na kupinga utumiaji wa nguvu na mabavu, pamoja na kukabiliwa na ukandamizaji wa mifumo ya kidikteta na utumiaji wa nguvu ya ukandamizaji dhidi yao, na kujaribu kwake kuwapuuza wanamapinduzi kwa kuwapiga risasi au kuwatuma askari wake wanaofungamana na vyombo vyake vya usalama ili kuwashambulia, lakini jamhuri ya wanamapinduzi imeonyesha mshikamano wa hali ya juu, hadi kufanya mbinu za utawala zishindwe kuwakokota kwenda kwenye medani ya mabavu na vita, pamoja na kuanguka idadi kubwa miongoni mwa mashahidi na majeruhi katika maandamano na migomo ya amani. Hakika mwenendo huu wa kimapinduzi wa kimaendeleo, unadhihirisha kupatikana kwa mabadailiko katika nafsi za watu wa umma kulingana na maneno yake (swt):

إِنَّ ٱللَّهَ لَا يُغَيِّرُ مَا بِقَوۡمٍ حَتَّىٰ يُغَيِّرُواْ مَا بِأَنفُسِهِمۡۗ ﴿١١﴾

**"Hakika Mwenyezi Mungu habadilishi yaliyoko kwa watu hadi wabadilishe yaliyo katika nafsi zao." (Sura Raad: 11)**.

Hakika kushikamana na malengo ya nchi kwa ajili ya marekebisho ni jambo linalojumuisha makundi yote ya jamii bila kujali malengo maalumu yenye aina mbalimbali za kimakundi au za kimadhehebu au za sehemu. Na kushikamana na mfumo wa amani katika harakati za watu mbali na kutumia mabavu na ugaidi, ndio njia sahihi ya kukomboa wananchi wa umma na hali ya udikteta na kutokuendelea, na ili kuleta utambuzi na haki za kisharia kwa kusimamisha utawala unaotokana na matakwa ya mwanachi na kujenga dola ya kidemokrasia ya kisasa.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 17 8/27/2015 2:17:17 PM

Tunaweza kusema kwa kujiamini na nguvu kwamba juhudi za warekebishaji wastawishaji na walingania umoja na kuleta ukaribu wana dauru ya kimsingi katika kuivisha utambuzi wa umma na kunyanyua kiwango cha kifikra baina ya watu wake na katika kuzalisha mwenendo wa utekelezaji wa kimaendeleo. Warekebishaji wametoa juhudi za hali ya juu katika kuamsha jamhuri ya umma na kusambaza utambuzi ndani ya watu wake, na katika kusambaza utamaduni wa umoja na usamehevu, na kujali maslahi ya umma, na kuvuka ikhitilafu za pembezoni na kushikamana na mfumo wa amani na uadilifu.

Na mazungumzo ya urekebishaji yamekabiliwa sana na kibano cha mirengo ya kushadidia na kupetuka mipaka ambayo ilikuwa inataka kuisukuma medani ya umma kwenye mivutano ya ndani na kukuza ikhitilafu za kimadhehebu na kifikra na kuendelea katika kutumia vitendo vya mabavu ambavyo vimepokonya jamii za umma amani yake na utulivu wake na kupaka matope hali yake na hali ya dini yake katika kiwango cha kiulimwengu. Na mapinduzi ya mwamko wa Kiarabu yamekuja ili kusaidia kufanikisha jamhuri ya umma kuchagua umoja wa nchi na mfumo wa amani na uadilifu.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 18 8/27/2015 2:17:17 PM

# KUANZISHA UVUMILIVU WA KIDINI

Wengi kati ya wanadini wanaangalia ikhitilafu za kidini baina ya wanadamu kwa mtazamo wa kijuu juu usio na maana, ambapo kila mwenye kujinasibisha na dini au madhehebu anaona kwamba alichoshikamana nacho ndio haki na sahihi, na kisichokuwa hicho ni makosa na batili, na itikadi hii ni jambo linaloeleweka, kwa sababu kama asingeitakidi hivyo katika dini yake na madhehebu yake isingesihi kwake kuifuata na kuiamini.

Lakini ujuu juu na upuuzi unatokana na majivuno yake dhidi ya wafuasi wa dini na madhehebu mengine, na kushangazwa kwake namna gani wanafuata dini batili na madhehebu mabaya? Hakika yeye anaona nafsi yake iko katika haki ambayo haina mjadala, na ni ukweli ambao hauna shaka, sasa kwa nini wengine hawamfuati katika dini yake na madhehebu yake?

Na mwanadamu anaweza kuvuka hisia hizi za kipuuzi kama atatambua kwamba wengine na wao pia wanaweza kuwa na mtazamo uleule dhidi ya itikadi yake, kwamba wao wanaona nafsi zao ziko katika haki na usahihi katika imani yao ya kidini, na kwamba isiyokuwa hiyo ni batili na upotovu, na wao vilevile wanashangaa na wanajiuliza: Kwa nini yeye hafuati njia yao? Na amesema kweli Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema:

وَلَا تَسُبُّواْ ٱلَّذِينَ يَدۡعُونَ مِن دُونِ ٱللَّهِ فَيَسُبُّواْ ٱللَّهَ عَدۡوَۢا بِغَيۡرِ عِلۡمٖۗ كَذَٰلِكَ زَيَّنَّا لِكُلِّ أُمَّةٍ عَمَلَهُمۡ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّهِم مَّرۡجِعُهُمۡ فَيُنَبِّئُهُم بِمَا كَانُواْ يَعۡمَلُونَ ١٠٨



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 19 8/27/2015 2:17:17 PM

**“Wala msiwatukane wale wanaoomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu wasije wakamtukana Mwenyezi Mungu kwa jeuri bila ya kujua. Kama hivyo tumeupambia kila umma vitendo vyao. Kisha marejeo yao yatakuwa kwa Mola Wao, Naye atawaambia yale waliyokuwa wakiyatenda.” (Sura An’am: 108)**.

Hii haimaanishi kwamba hakuna haki wala ukweli, kufuata dini kumesimama juu ya msingi wa kushikamana na haki na kuachana na batili. Lakini tunayotaka kuashiria hapa na kutilia mkazo juu yake ni kwamba mas’ala ya kidini kwa mwanadamu yanazungukwa na vikwazo vingi na sababu mbalimbali zinazoathiri, nayo sio mas’ala mepesi ya kuyaangalia kijuu juu au kuyamaliza kwa mjadala na mdahalo. Hakika mtazamo huu wa kijuu juu katika kadhia ya dini iko nyuma ya msukumo wa wanadini wengi katika kutangaza itikadi yao kwa njia mbalimbali zenye mizunguko, hawafahamu mazingira ya mwingine na kwamba inaweza kusababisha kumkosea na kugongana naye. Hakika ni haki kwa mwanadamu kujifakharisha kwa itikadi yake na kuilingania, lakini ni juu yake kudurusu hali ya mtu ambaye unamwendea  na kumlingania, na kuamiliana pamoja naye kwa heshima na kutambua haki yake katika kukataa na kukubali, na huu ndio mfumo wa Mwenyezi Mungu. Anasema (swt):

ٱدۡعُ إِلَىٰ سَبِيلِ رَبِّكَ بِٱلۡحِكۡمَةِ وَٱلۡمَوۡعِظَةِ ٱلۡحَسَنَةِۖ وَجَٰدِلۡهُم بِٱلَّتِي هِيَ أَحۡسَنُۚ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعۡلَمُ بِمَن ضَلَّ عَن سَبِيلِهِۦۖ وَهُوَ أَعۡلَمُ بِٱلۡمُهۡتَدِينَ ﴿١٢٥﴾

**“Waite kwenye njia ya Mola Wako kwa hekima na mawaidha mazuri na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola Wako ndiye**



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 20 8/27/2015 2:17:18 PM

**anayemjua zaidi aliyepotea njia yake na Yeye ndiye anayewajua zaidi walioongoka." (Sura Nahli: 125)**.

Na hekima ni kuweka jambo mahala pake panapofaa, na sio kila mtu wala sio kila wakati wala sio kila njia inafaa kulingania. Kama ambavyo haisihi kujadili na wengine wanaokhitalifiana pamoja na wewe katika jambo la kidini ikiwa huna uwezo wa kufanya mjadala kwa njia bora zaidi, anasema (swt):

۞ وَلَا تُجَٰدِلُوٓاْ أَهۡلَ ٱلۡكِتَٰبِ إِلَّا بِٱلَّتِي هِيَ أَحۡسَنُ إِلَّا ٱلَّذِينَ ظَلَمُواْ مِنۡهُمۡۖ وَقُولُوٓاْ ءَامَنَّا بِٱلَّذِيٓ أُنزِلَ إِلَيۡنَا وَأُنزِلَ إِلَيۡكُمۡ وَإِلَٰهُنَا وَإِلَٰهُكُمۡ وَٰحِدٞ وَنَحۡنُ لَهُۥ مُسۡلِمُونَ ﴿٤٦﴾

**"Wala usijadiliane na watu wa Kitabu isipokuwa kwa njia iliyo nzuri kabisa; isipokuwa wale waliodhulumu miongoni mwao. Na semeni: Tumeamini yaliyoteremshwa kwetu na yaliyoteremshwa kwenu, na Mungu Wetu na Mungu Wenu ni Mmoja na sisi ni wenye kusilimu kwake." (Sura Ankabuti: 46)**.

Ambapo ibara za mwisho za Aya zinaashiria katika kuvuka ufafanuzi wa ikhitilafu kwa kutilia mkazo sehemu za kuafikiana na kushirikiana. Hakika kusoma kwa utambuzi katika aya nyingi za Qur'ani ambazo zinazungumzia mas'ala ya ikhitilafu za kidini zinampa mwanadamu uoni na mwongozo katika kuamiliana pamoja na wanaomkhalifu katika itikadi ya kidini. Hakika sisi tunaishi katika matatizo ya kukuza ikhitilafu za mirengo ya kimadhehebu na kifikra katika jamii zetu, ambapo watu wanakwenda mbio kujikalifisha kutoa ikhitilafu za kimadhebu katika kila mazungumzo au katika kila uhusiano pamoja na



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 21 8/27/2015 2:17:18 PM

yeyote kati ya wafuasi wa madhehebu nyingine na kundi lingine la kifikra.

Amepokea Abu Baswir amesema: Nilimwambia Abu Ja'far Imam Muhammad al-Baqir عليه السلام: Je niwalinganie watu katika tuliyonayo? Akasema: "Hapana." Nikasema: Yeyote akinitaka mwongozo nimwelekeze? Akasema: "Ndio, kama akikutaka umwelekeze basi mwelekeze, na akitaka umuongezee basi muongezee na akikupinga nawe mpinge."[7]

Na kutoka kwa Thabiti Abu Said amesema: Abu Abdillahi Imam Ja'far as-Sadiq عليه السلام aliniambia: "Ewe Thabiti mna nini na watu? Jizuieni wala msimlinganie yeyote katika jambo lenu. Wallahi kama watu wa mbinguni na watu wa ardhini wangekusanyika ili wampoteze mja ambaye Mwenyezi Mungu anataka amuongoze wasingeweza, jizuieni na watu, na wala asiseme mmoja wenu: 'Ni ndugu yangu na mtoto wa ami yangu na jirani yangu', hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu anapotaka kheri kwa mja basi anaifanya roho yake kuwa nzuri na hivyo hatosikia wema ila ataujua wala uovu ila atakataa, kisha Mwenyezi Mungu ataweka katika moyo wake neno litakalokusanya jambo lake."[8]

Hakika mfano wa nususi hizi zinalenga kuelekeza namna ya kuamiliana na wapinzani katika itikadi, na kutojitumbukiza na kujiingiza katika kuelezea mambo ya ikhitilafu za kiitikadi zilizopo kati yako na wengine.

**Dini ni Makuzi ya Kifamilia:**

Kama ambavyo mtoto anajifunza lugha, mila, mitindo ya maisha kutoka katika familia yake ambayo analeleka katika malezi yake, vi-

---

[7] *Wasailu Shi'ah*, Juz. 16, Uk. 191. Hadithi: 2131.
[8] *Wasailu Shi'ah*, Juz. 16, Uk. 191. Hadithi: 21318.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 22 8/27/2015 2:17:18 PM

levile anajifunza itikadi zake za kidini na anakua katika upendo wenye vielelezo vya matukufu ambayo familia yake inayaamini na kushikamana na madhehebu yake na mwenendo wake. Hii ndio hali ya watu wa dini katika kila zama na kila sehemu na ndio sababu ya kimsingi ya kubakia dini na madhehebu, ambapo vizazi vinarithishana kwa njia ya malezi na makuzi. Anayezaliwa na kuleleka katika familia ya Kikristo ya Kikatoliki anakuwa Mkrisito wa Kikatoliki, na atakuwa ni mwenye imani asilia (Orthodox) kama atazaliwa katika familia ya Ki-orthodox au Protestanti kama ataleleka katika familia ya Kiprotestanti.

Na vilevile anayezaliwa katika familia ya Kiyahudi atakuwa Myahudi wa madhehebu ya familia yake, na hali ni ileile itatokea katika familia za Kiislamu, ambapo watoto wake wanakuwa Waislamu wa madhehebu ya familia za Ahlus-Sunna, Shia n. k. Na baadaye mtu anaweza kuacha dini ya watu wake na madhehebu ya familia yake na kwenda kwenye dini na madhehebu mengine anayokinaika nayo, isipokuwa katika hali chache sana ukilinganisha na hali halisi ya jumla katika mwenendo wa jamii ya kibinadamu.

Na hiyo ndio hali ambayo ujumbe wa Manabii ulikutana nayo kupitia historia yao, kwani pamoja na uwezo aliowapa Mwenyezi Mungu Manabii Wake miongoni mwa haki iliyo dhahiri, ujumbe ulio wazi na hoja za kweli walizowapelekea watu wao ila ni kwamba kitendo cha watu hao kushikamana na dini za baba zao na kina cha athari ya makuzi na malezi vilikuwa vinawazuia wale watu kufuata haki na kukubali dini ya Mwenyezi Mungu. Anasema Mwenyezi Mungu (swt):

قَالَ مُتْرَفُوهَا إِنَّا وَجَدْنَا آبَاءَنَا عَلَىٰ أُمَّةٍ وَإِنَّا عَلَىٰ آثَارِهِمْ مُقْتَدُونَ



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 23 8/27/2015 2:17:19 PM

قَالَ أَوَلَوْ جِئْتُكُمْ بِأَهْدَىٰ مِمَّا وَجَدْتُمْ عَلَيْهِ آبَاءَكُمْ ۖ قَالُوا إِنَّا بِمَا أُرْسِلْتُمْ بِهِ كَافِرُونَ

**““....walisema: Hakika sisi tuliwakuta baba zetu juu ya desturi na tunafuata nyayo zao. Akasema: Hata nikiwaletea yenye muongozo bora kuliko mliowakuta nayo baba zenu? Wakasema Sisi tunayakataa hayo mliyotumwa nayo.” (Sura Zukhruf: 22 – 23)**

Amepokea Ibnu Abbas رضي الله عنه kwamba Nabii صلى الله عليه وآله وسلم amesema: “Kila mtoto anazaliwa katika asili ya Uislamu, na wazazi wake ndio wanaomfanya kuwa Myahudi au Mkiristo.”[9] Hii ni ishara ya wazi katika ukweli huu wa kijamii. Na ni mashuhuri kwa Mashia beti mbili za shairi katika nyanja ya kujifakharisha katika ufuasi wa madhehebu, zinakusudia kutilia mkazo nafasi ya malezi na makuzi katika kuchuma mapenzi na ufuasi wa dini, nazo ni:

“Mwenyezi Mungu asimwadhibu mama yangu hakika kwake nimepata mapenzi ya kumpenda Wasii na ameninywesha maziwa, na nilikuwa na mzazi anayempenda Abu Hasan, nikawa ni kati ya wanayempenda Abu Hasan.”

## Mazingira ya Kijamii ni Mlezi wa Dini:

Inakaribia kutokukuta jamii ya binadamu katika muda wote wa historia iliyopita na hadi hivi sasa isipokuwa ina utambulisho wa kidini, na ufuasi wa mtu katika jamii yake unaakisi hali hiyo ya kidini katika maisha yake, kwa kuanzia na ada na desturi za kijamii katika kumpokea kwake kama mtoto mpya, na kumalizia na ibada za kumuaga kwake na kumsindikiza kwake baada ya kufariki dunia, kwa kupitia kanuni za ndoa na hukumu za mambo ya kiibada na muktadha wa

[9] Ibnu Hajar al-Haithamiy katika *Majma’u Zawaid*, Juz. 7, Chapa ya 1408 Hijiria, (Beirut Darul- Kutubil- Ilimiya), Uk. 218. na mfano wake katika *Biharul-An’war*, Juz. 3, Uk. 281.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 24 8/27/2015 2:17:19 PM

minasaba na vielelezo vya kidini ambavyo vinatawala jamii yake.

Ambapo mwanadamu anakuta nafsi yake inasukumwa kuamiliana na kushirikiana na mazingira ya nyumba yake ya kijamii katika upande wake wa kidini, hata kama hajakinaika na yote au na baadhi ya mielekeo na vitendo, kwa sababu kama hataki au ikionekana ni mtu mwasi mwenye kukhalifu hali ya jamii, anaweza kukabiliwa na kibano na kufanywa mwenye kupuuzwa katika jamii yake. Hakika watu wengi katika dini mbalimbali na madhehebu hawaamiliani na itikadi za kidini kama mas'ala binafsi na maamuzi binafsi kama ulivyo wajibu wa kiakili kwa mwanadamu, bali wanaamiliana pamoja na itikadi kama ni uchaguzi wa kijamii hivyo hawazipi nafsi zao taabu ya kufikiri na jukumu la kutafiti katika maamuzi mbadala.

Tangu zamani amesema mshairi wa Kiarabu Dariyd bin as-Swamta:

"Mimi si vinginevyo isipokuwa natokana na Ghaziyah, wakipotea nami napotea, na Ghaziyah wakiongoka nami naongoka."

Na kwa hiyo wafuasi wa kila dini wanahisi na wanaitakidi kwa kuridhia yale waliyonayo, na kitendo cha imani hiyo kuafikiwa na wote katika jamii yao kinawaandalia mazingira ya kuamini kuwa itikadi yao ni sahihi, hususan kwamba wao wanakulia katika hali ya kupenda na kutukuza viongozi na wakuu ambao wanakuwa na nafasi ya kuathiri na kutukuzwa katika nafsi, na wala hawafikirii kwamba wanawapeleka kwenye kosa au wanawaelekeza kwenye batili.

Na haya ndio aliyowatahadharisha nayo Imam Ja'far as-Sadiq عليه السلام baadhi ya wafuasi wake kutokana na yale yaliyojionyesha kwao miongoni mwa hamasa na msukumo katika kuwalingania wengine katika itikadi na madhehebu, amesema عليه السلام: "Msigombane katika dini yenu hakika ugomvi unaleta ugonjwa katika moyo, waacheni



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 25 8/27/2015 2:17:19 PM

watu, hakika watu wamechukua kutoka kwa watu."[10]

Kisha hakika katika kila jamii kuna vituo vyenye nguvu vinajiona kuwa vinahusika katika kulinda dini ya jamii na kuhami itikadi yake na matukufu yake, dhidi ya uasi wowote au kutoka katika itikadi iliyopo, kuanzia na utawala wa kisiasa ambao unaweza kuzalisha mwonekano wa kidini kwa ajili ya kuimarisha utawala wake, kama inavyotusimulia Qur'ani Tukufu juu ya Firaun aliponyanyua bendera ya kutetea dini ya jamii dhidi ya Nabii Musa ﷺ, anasema (swt):

وَقَالَ فِرْعَوْنُ ذَرُونِيٓ أَقْتُلْ مُوسَىٰ وَلْيَدْعُ رَبَّهُۥٓ ۖ إِنِّيٓ أَخَافُ أَن يُبَدِّلَ
دِينَكُمْ أَوْ أَن يُظْهِرَ فِي ٱلْأَرْضِ ٱلْفَسَادَ ﴿٢٦﴾

**"Na Firauni akasema: Niacheni nimuuwe Musa, naye amwite Mola Wake! Hakika mimi nachelea asije kubadilisha dini yenu au akadhihirisha uharibifu katika nchi." (Sura Al-Mu'min: 26)**.

Na kuna taasisi za kidini katika kila jamii ambazo kazi yake ni kulinda itikadi, kuitetea na kusimama imara mbele ya rai yototе yenye kukhalifu. Kwa kuongezea ni zile nguvu nyingine za kijamii ambazo hazikawii katika kuonya mwenye kuhadaiwa na nafsi kutoka katika mwelekeo wa dini ya jamii. Hii ndio hali ya mazingira ya jamii ambayo huwa ni mlezi na mtetezi wa itikadi ya dini, vizazi vyake hukua katika hali ya kushikamana na dini yao, na huimarika kwayo, na huilinda isiweze kuathirika na daawa pinzani na mielekeo mingine ya kiitikadi.

Na hali hii ndio inayotufafanulia jinsi ambavyo hupatikana mwendelezo wa dini na madhehebu kwa kurithishana kupitia vizazi, kama inavyotufafanulia ugumu uliyopo wa watu kuacha

---

[10] *Wasailu Shi'ah*, Juz. 16, Uk, 191, Hadithi 21316.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 26 8/27/2015 2:17:19 PM

maelekezo ya kidini iliyopo katika jamii yao. Ugumu huo ambao haubebi isipokuwa aliyeiandaa nafsi yake kupambana na mateso na vibano mbalimbali, na wao kwa kawaida ni wachache miongoni mwa watu wa jamii kama inavyotusimulia Qur'ani Tukufu katika sira ya Manabii mbalimbali. Katika sira ya Nabii Nuhu عليه السلام, anasema (swt):

وَمَآ ءَامَنَ مَعَهُۥٓ إِلَّا قَلِيلٌ ۝٤٠

**"Na hawakumwamini pamoja naye isipokuwa wachache tu." (Sura Hud: 40).**

Na katika sira ya Nabii Musa عليه السلام anasema (swt):

فَمَآ ءَامَنَ لِمُوسَىٰٓ إِلَّا ذُرِّيَّةٌ مِّن قَوْمِهِۦ عَلَىٰ خَوْفٍ مِّن فِرْعَوْنَ وَمَلَإِيْهِمْ أَن يَفْتِنَهُمْ

**"Basi hawakumwamini Musa, isipokuwa baadhi ya wazawa katika kaumu yake, kwa sababu ya kumuogopa Firauni na wakubwa wao asiwatie msukosuko." (Sura Yunus: 83)**.

Ndio, mambo yanakuwa mepesi ikiwa upande mwingine na daawa mpya itatengeneza jamii yenye kupambana itayoandaa mazingira mbadala yanayokidhi mahitaji ya ufuasi wa jamii na kuhisi ulinzi na amani.

## Ugonjwa wa Kasumba na Maslahi:

Hakika kuna kundi la watu wanashikamana na nyendo zao za kidini kwa kasumba na ukaidi, hata kama utadhihirika ukweli na haki kwa mwingine, na wanaweza kuamua kuchagua dini kuto-



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 27 8/27/2015 2:17:20 PM

kana tu na misukumo ya maslahi na kupata chumo na manufaa. Na wao kwa hilo wanadhulumu nafsi zao kabla ya mtu yeyote yule, na wanabeba jukumu la msimamo wao mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na Manabii na wafuasi wao waumini hawana mbele yao jukumu lolote isipokuwa kukumbusha na kufikisha, kisha kuwaacha watu na mambo yao na waliyoyachagua kwa ajili ya nafsi zao.

Anasema (swt):

وَقُل لِّلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْكِتَٰبَ وَٱلْأُمِّيِّـۧنَ ءَأَسْلَمْتُمْ ۚ فَإِنْ أَسْلَمُوا۟ فَقَدِ ٱهْتَدَوا۟ ۖ وَّإِن تَوَلَّوْا۟ فَإِنَّمَا عَلَيْكَ ٱلْبَلَٰغُ ۗ وَٱللَّهُ بَصِيرٌۢ بِٱلْعِبَادِ ﴿٢٠﴾

**“Na waambie wale waliopewa Kitabu na wale wasiokuwa na kisomo: Je mmesilimu? Kama wakisilimu basi wameongoka; na kama wakikengeuka basi ni juu yako ni kufikisha tu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaona waja.” (Sura Imraan: 20)**.

Hakika katika baadhi ya makundi ya wabeba itikadi na maoni hujitokeza kwao utashi binafsi unaowasukuma kwenye kuudhibiti upande mwingine na kuudhalilisha, kwa kuvuka kwa hilo mipaka ya kuhubiri itikadi yao na kutoa rai zao, na haya ni mambo ambayo Mwenyezi Mungu hakuyaruhusu kwa Manabii wake tukiachilia mbali wasiokuwa wao miongoni mwa watu wengine.

## Mtazamo wa Qur’ani:

Hakika kati ya hoja kubwa za ukweli wa Qur’ani tukufu ni uhalisia wa mfumo wake, na namna ya kuelezea kwake jambo la kidini katika maisha ya mwanadamu.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 28 8/27/2015 2:17:20 PM

Pamoja na Qur'ani kutia mkazo mkubwa wenye kuungwa mkono na hoja na dalili juu ya haki ya Uislamu na kwamba ndio dini pekee ya Mwenyezi Mungu, na isiyokuwa hiyo Mwenyezi Mungu hatoikubali,

إِنَّ ٱلدِّينَ عِندَ ٱللَّهِ ٱلْإِسْلَٰمُ ۗ ﴿١٩﴾

**"Hakika dini mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu." (Surat Imraan: 19).**

وَمَن يَبْتَغِ غَيْرَ ٱلْإِسْلَٰمِ دِينًا فَلَن يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِى ٱلْءَاخِرَةِ مِنَ ٱلْخَٰسِرِينَ ﴿٨٥﴾

**"Na mwenye kutaka dini isiyokuwa Uislam haitakubaliwa kwake, naye katika akhera ni miongoni mwa wenye kupata hasara." (Sura Imraan: 85)**.

Lakini bado Qur'ani inatilia mkazo juu ya uhuru wa mwanadamu katika maisha haya ambapo inasema: **"Hakuna kulazimisha katika dini" (Sura al-Baqarah: 256)**. **"Anayetaka aamini na anayetaka akufuru." (Sura al-Kahfi: 29)**. **"Na kama angetaka Mola Wako wangeamini wote waliopo ardhini je, wewe utawalazimisha watu ili wawe waumini." (Sura Yunus: 99)**.

Na kwa mantiki ya Qur'ani kazi ya Manabii inaishia katika kufikisha na kukumbusha na sio haki kwa yeyote miongoni mwao kulazimisha watu: **"Kumbusha; hakika wewe ni mkumbushaji. Sio mwenye kuwalazimisha." (Sura Ghashiyah: 21- 22)**. **"Na wala wewe sio wakili juu yao." (Sura Shuraa: 6)**. **"Na hatujakutuma kuwa mlinzi juu yao." (Sura Nisaa: 80)**. Na ni juu ya Nabii asiudhike ikiwa watu hawatoitikia wito wake, kwani wao wanatumia haki yao ya kawaida katika kuchagua na wanabeba jukumu la nafsi zao mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 29 8/27/2015 2:17:20 PM

لَعَلَّكَ بَاخِعٌ نَفْسَكَ أَلَّا يَكُونُوا مُؤْمِنِينَ

**"Huenda ukaingamiza nafsi yako kwa kuwa hawawi waumini." (Sura Shu'araa: 3).**

طه ﴿١﴾ مَآ أَنزَلْنَا عَلَيْكَ ٱلْقُرْءَانَ لِتَشْقَىٰٓ ﴿٢﴾ إِلَّا تَذْكِرَةً لِّمَن يَخْشَىٰ ﴿٣﴾

**"Twaha. Hatukukuteremshia Qur'ani ili upate mashaka. Isipokuwa ni mawaidha kwa wenye kunyenyekea." (Sura Twaha: 1- 3).**

Na Qur'ani inakiri uwepo wa wafuasi wa dini nyingine sambamba na uwepo wa wafuasi wake waumini:

إِنَّ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَٱلَّذِينَ هَادُواْ وَٱلصَّٰبِـِٔينَ وَٱلنَّصَٰرَىٰ وَٱلْمَجُوسَ وَٱلَّذِينَ أَشْرَكُوٓاْ إِنَّ ٱللَّهَ يَفْصِلُ بَيْنَهُمْ يَوْمَ ٱلْقِيَٰمَةِۚ إِنَّ ٱللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ شَهِيدٌ ﴿١٧﴾

**"Hakika wale ambao wameamini na ambao ni mayahudi na Wasabai na Wanaswara na wamajusi na wale washirikishao, hakika Mwenyezi Mungu atawapambanua siku ya Kiyama, hakika Mwenyezi Mungu ni shahidi juu ya kila kitu." (Sura Hajj: 17).**

Na Qur'ani inausia wafuasi wake juu ya muamala mzuri pamoja na wenye kuwakhalifu katika dini maadamu hawafanyi uadui:

لَّا يَنْهَىٰكُمُ ٱللَّهُ عَنِ ٱلَّذِينَ لَمْ يُقَٰتِلُوكُمْ فِى ٱلدِّينِ وَلَمْ يُخْرِجُوكُم مِّن دِيَٰرِكُمْ أَن تَبَرُّوهُمْ وَتُقْسِطُوٓاْ إِلَيْهِمْۚ إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلْمُقْسِطِينَ ﴿٨﴾

**"Mwenyezi Mungu hawakatazi kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakuwapiga vita, wala hawakuwatoa makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu."**
**(Surat al-Mumtahinah: 8)**.

Qur'ani inatanabahisha kwamba mas'ala ya kidini aghlabu hayanyenyekei kwa binadamu kwa mantiki ya hoja na dalili, bali kwa matamanio, kudumaa na kupatwa na hali ya kasumba na ukaidi. Anasema (swt):

وَلَئِنْ أَتَيْتَ ٱلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْكِتَـٰبَ بِكُلِّ
ءَايَةٍ مَّا تَبِعُوا۟ قِبْلَتَكَ ۚ وَمَآ أَنتَ بِتَابِعٍ قِبْلَتَهُمْ ۚ وَمَا بَعْضُهُم بِتَابِعٍ قِبْلَةَ
بَعْضٍ ۚ ﴿١٤٥﴾

**"Na hao waliopewa Kitabu hata ukiwaletea hoja za kila namna, hawatafuata Kibla chako; wala wewe si mwenye kufuata Kibla chao, wala baadhi yao si wenye kufuata Kibla cha wengine."**
**(Sura al-baqarah : 145)**

Na Qur'ani tukufu inazizoesha nyoyo za waumini kuishi pamoja na dini mbalimbali kwani ndio zilizokadiriwa kwa binadamu hadi Siku ya Kiyama, na wala asidhani yeyote kuwa kuna uwezekano wa kutenganisha baina ya dini katika maisha haya ya kidunia, ambapo hakika hiyo ni kazi iliyoahirishwa hadi Siku ya Kiyama, na itakamilika mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

إِنَّ ٱللَّهَ يَفْصِلُ بَيْنَهُمْ يَوْمَ ٱلْقِيَـٰمَةِ ۚ ﴿١٧﴾

**"Hakika Mwenyezi Mungu atapambanua baina yao Siku ya Kiyama." (Sura Hajji: 22:17).**



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 31 8/27/2015 2:17:22 PM

إِنَّ رَبَّكَ هُوَ يَفۡصِلُ بَيۡنَهُمۡ يَوۡمَ ٱلۡقِيَٰمَةِ فِيمَا كَانُواْ فِيهِ يَخۡتَلِفُونَ ٢٥

**"Hakika Mola Wako ndio atapambanua baina yao Siku ya Kiyama katika yale waliyokuwa wakikhitalifiana humo." (Sura AS-SAJDA 32:25)**.

Huu ndio mtazamo wa Qur'ani unaasisi mfumo wa kuamiliana na uvumilivu baina ya wanadamu pamoja na kukhitalifiana dini zao na madhehebu zao na kulinda mazingira ya amani na utambuano ndani ya jamii yenye dini mbalimbali, na unapokosekana mtazamo huu wa uhalisia ndipo inapopigwa ngoma ya vita vya kidini na yanafululiza maonyo ya migongano ya kimaendeleo na jamii kukabiliwa na mpasuko wa ndani na vita vya kimadhehebu.

Na kinachosikitisha sana ni kutawala mazingira ya vita ya kimadhehebu na mizozo ya kimakundi katika medani ya umma ilihali watu wake wanasoma mfano wa aya hizi za Qur'ani tukufu kila asubuhi na jioni. **"Je, hawatafakari Qur'ani au nyoyo zao zimetiwa kufuli." (Sura Muhammad: 24)**.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 32 8/27/2015 2:17:22 PM

# QUR'ANI ILIYOHAMWA

Huwenda zama hizi ni kati ya zama zenye kuchanua zaidi kwa kuijali Qur'ani tukufu, ambapo kuna mwonekano wa aina mbalimbali wa mazingatio haya. Umepanuka wigo wake na harakati zake zimekuwa nyingi. Kuna idhaa kumi na moja mahususi kwa ajili ya kurusha kisomo cha Qur'ani na vipindi vinavyohusiana nayo katika nchi za Saudia, Iran, Misri, Morocco, Yemen, Jordan, Sudan, Oman, Umoja wa Falme za Kiarabu, Kuwait na Baharain.

Na nakala za misahafu mitukufu zimeenea kwa lugha mbalimbali na kwa idadi kubwa, na kuna kiwanda cha Mfalme Fahdi cha kuchapisha misahafu, nacho ni kati ya viwanda vikubwa vya uchapishaji duniani, ambacho kina ukubwa wa mita mraba 25,000 na humo wanafanya kazi watu 2000 takriban na kila mwaka zinachapishwa nakala milioni 10, na jumla ya kiasi cha misahafu iliyosambazwa na *Majmau* ni zaidi ya nakala 193,000,000 hadi hivi sasa katika lugha 50.

Na katika zama hizi wamejitokeza wasomaji wapya walioweza kuvutia nyoyo kwa uzuri wa sauti zao na uzuri wa kisomo chao, kama walivyodhihiri maelfu bali makumi ya maelfu ya wenye kuzingatia kuhifadhi Qur'ani tukufu nzima ambapo yanafanywa mashindano katika nchi mbalimbali za Kiislamu. Na kuna maelfu ya madrasa na vituo vya kujifunza Qur'ani na kuhifadhisha na mwishoni imejitokeza jumuiya ya *Haiatul- A'amati Litahfidhil-Qur'ani* iliyo chini ya Umoja wa Nchi za Kiislamu, na inayo ratiba pana ya kuhifadhisha Qur'ani. Inafadhili idadi kubwa ya vikundi na madrasa za Qur'ani katika zaidi ya nchi 65 na vyuo 72 mahususi vya Qur'ani, na idadi ya wanafunzi wake inazidi laki moja, wanafunzi wa kiume na wa kike, na 31,000 kati yao wameshahifadhi Qur'ani nzima.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 33 8/27/2015 2:17:23 PM

Zaidi ya hapo ni uwepo wa taasisi na vituo mbalimbali vinavyojali nyanja mbalimbali katika mambo ya Qur'ani tukufu, na hakuna shaka kwamba mwonekano huu wa kuzingatia Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu unaufariji moyo wa mwanadamu Mwislamu na kumzidishia fahari na utukufu. Lakini swali ambalo linajitokeza lenyewe ni je, shughuli hizi zinavuka mwonekano wa nje na kufika katika wajibu na majukumu yaliyoelekezwa na Qur'ani? Je, Waislamu wanatoka katika duara la malalamiko ya Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم kwa Mola Wake juu ya watu kuihama Qur'ani?

**Wameifanya Qur'ani Mahame:**

Qur'ani tukufu inatoa habari kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم alitoa malalamiko kwa Mola Wake juu ya watu kuihama Qur'ani, anasema (swt):

وَقَالَ ٱلرَّسُولُ يَـٰرَبِّ إِنَّ قَوْمِى ٱتَّخَذُوا۟ هَـٰذَا ٱلْقُرْءَانَ مَهْجُورًا ﴿٣٠﴾

**"Na alisema Mtume صلى الله عليه وآله وسلم: Ewe Mola Wangu hakika watu wangu wameifanya hii Qur'ani ni mahame." (Sura al-Furqan: 30)**.

Na *al-hajru* ni kuacha na kupuuza, na maelezo "*Itakhadhu*" inamaanisha kuwa kuipuuza Qur'ani imekuwa ni mfumo na njia inayotegemewa kwao.

Hakika mtu wakati wa kuamiliana na ujumbe wowote unaomfikia huathiriwa na nafasi aliyonayo katika nafsi yake yule aliyetumwa kwake, ikiwa aliyetumwa ni muhimu kwake, na ni mtukufu kwake. Anapata kwake kiwango kikubwa zaidi cha mazingatio. Ama ikiwa aliyetumwa ni mtu wa kawaida na sio muhimu katika mtazamo wake basi matokeo ya ujumbe wake yatakuwa ni kudharauliwa na kupuuzwa.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 34 8/27/2015 2:17:23 PM

Na sisi kama Waislamu, hakika tunaitakidi kwamba Qur'ani tukufu ni ujumbe unaotoka kwa Mwenyezi Mungu kwenda kwa watu wote, sasa namna gani inasihi kwetu kupuuza ujumbe huu ambao Mwenyezi Mungu Muumba wetu na Mwenye kuturuzuku na ambaye mikononi Mwake kuna uhai wetu na mauti yetu ametufadhilisha kwa kuutuma kwetu?

Na ujumbe wa Qur'ani hauna ombi lolote la kumhudumia Mola Mtukufu kwani Yeye amejitosheleza na walimwengu, bali kwa hakika ni mfumo wenye nuru na uongofu unaomwangazia mwanadamu njia ya maisha yake, na kumwelekeza kwenye kheri yake na mafanikio yake: **"Hakika Qur'ani hii inaongoza kwenye yaliyonyooka." (Sura Israi: 9)**. Kuna sababu gani basi ya kupinga ujumbe mtukufu kutoka katika chanzo kitukufu?

## Madhumuni ya Qur'an na Mfumo Wake:

Hakika Qur'ani tukufu ina pande mbili: Upande wa muundo na unaonekana katika matamko na maneno ya aya zake zilizokusanywa baina ya jalada mbili za msahafu mtukufu. Na upande wa madhumuni na unaonekana katika misingi, mifumo na sharia ambazo zinabebwa na aya za Qur'ani tukufu.

Na hata kama ikiwa kuijali Qur'ani kwa sura ya nje kwa kuisoma, kuhifadhi, kuitambua tafsiri na kuisambaza ni jambo linalotakiwa, lakini haisihi kutosheka na hayo na kuacha kupiga hatua kwenda kuitikia madhumuni ya Qur'ani, kwa kushikamana na misingi ambayo inaelezwa na Qur'ani, na kuifanyia kazi mifumo ambayo inalinganiwa na Qur'ani, na kutekeleza sharia za Mwenyezi Mungu ambazo zinapendekezwa.

Bali ni kwamba hakika thamani ya Qur'ani na kuhifadhi aya zake inakuja pale panapokuwa na lengo la kuongoka kupitia ujumbe



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 35 8/27/2015 2:17:23 PM

wake na kutekeleza maana yake katika uhalisia wa maisha. Na ikiwa usomaji na uhifadhi wa Qur'ani utaepukana na hayo na ukafinyika bila kushikamana na utekelezaji wa kivitendo, hakika utapelekea kupatwa na hasira za Mwenyezi Mungu Mtukufu na ghadhabu Yake, na haya ndio yaliyoelezwa na aya za Qur'ani na nususi za Hadithi na riwaya. Hakika Qur'ani inaelekeza kemeo kali kwa wale ambao wanasoma aya zake, lakini wao hawashikamani na misingi ya kheri na wema, anasema (swt):

۞ أَتَأْمُرُونَ ٱلنَّاسَ بِٱلْبِرِّ وَتَنسَوْنَ أَنفُسَكُمْ وَأَنتُمْ تَتْلُونَ ٱلْكِتَٰبَ ۚ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٤٤﴾

**"Je, mnawaamrisha watu kutenda mema na mnajisahau hali mnasoma Kitabu? Basi je, hamfahamu?" (Sura al-Baqarah: 44)**.

Na Qur'ani tukufu inalaumu wafuasi wa dini zilizotangulia ambao wanarushiana tuhuma baina yao na wala hawashikamani na mafunzo na tabia njema ambayo wanaisoma katika vitabu vyao vitakatifu, anasema (swt):

وَقَالَتِ ٱلْيَهُودُ لَيْسَتِ ٱلنَّصَٰرَىٰ عَلَىٰ شَيْءٍ وَقَالَتِ ٱلنَّصَٰرَىٰ لَيْسَتِ ٱلْيَهُودُ عَلَىٰ شَيْءٍ وَهُمْ يَتْلُونَ ٱلْكِتَٰبَ ۗ ﴿١١٣﴾

**"Na Mayahudi walisema: Manaswara hawana chochote na Manaswara walisema: Mayahudi hawana chochote na hali (wote) wanasoma kitabu." (Sura al- Baqarah: 113)**.

Hakika Qur'ani Tukufu inambebesha mwanadamu mradi bora wa maendeleo na mafanikio, na umma ambao unaifuata hii Qur'ani

na kuitekeleza, ni wajibu uendelee katika hali yake kivitendo kwa kushikamana na dhana za Qur'ani, na hatimaye kuwa mfano na kigezo kinachoyavutia mataifa na kuyapeleka kwenye mfumo wa Qur'ani. Lakini kinachosikitisha sana ni masafa makubwa yanayotenganisha baina ya hali ya umma na uongofu wa Qur'ani Tukufu, kwani unaishi katika hali ya kutoendelea na uovu katika pande nyingi bila ya kunufaika na nuru ya Qur'ani na mionzi yake ongofu, jambo ambalo linaifanya ishabihiane na yale iliyoyasimulia Qur'ani Tukufu juu ya Wayahudi ambao Mwenyezi Mungu aliteremsha kwao Taurati, lakini wao hawakubeba majukumu yao mukabala wake. Anasema (swt):

مَثَلُ ٱلَّذِينَ حُمِّلُواْ ٱلتَّوۡرَىٰةَ ثُمَّ لَمۡ يَحۡمِلُوهَا كَمَثَلِ ٱلۡحِمَارِ يَحۡمِلُ أَسۡفَارَۢاۚ ﴿٥﴾

**"Mfano wa waliobebeshwa Tawrat kisha wasibebe, ni mfano wa punda anayebeba vitabu vikubwa." (Sura al-Jumu'ah: 5)**.

Na vipi punda anaweza kunufaika kwa kubeba vitabu vya elimu na maarifa, naye hamiliki uwezo wa kufahamu, wala uwezo wa kunufaika? Vivyo ndivyo ilivyo hali ya umma ambao unabeba vitabu bora kabisa vya Mwenyezi Mungu na ujumbe wa mbinguni, lakini hauna matakwa ya kushikamana na kutekeleza. Na Qur'ani inazungumzia juu ya mtu ambaye anasomewa aya za Qur'ani lakini hazitii wala maisha yake hayaendi kulingana na uongofu wake, bali anaendelea na mfumo wake wa kimakosa na njia yake ya upotovu, kana kwamba sauti ya mbinguni haijayafikia masikio yake, au kana kwamba katika masikio yake kuna uziwi unaomzuia kusikia, anasema (swt):



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 37 8/27/2015 2:17:24 PM

وَإِذَا تُتْلَىٰ عَلَيْهِ ءَايَٰتُنَا وَلَّىٰ مُسْتَكْبِرًا كَأَن لَّمْ يَسْمَعْهَا كَأَنَّ فِىٓ أُذُنَيْهِ وَقْرًا ۖ فَبَشِّرْهُ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٧﴾

**"Na anaposomewa Aya Zetu huzipa mgongo kwa kujivuna kama kwamba hakuzisikia, kama kwamba masikioni kwake mna uziwi, basi mbashirie adhabu chungu." (Sura Luquman: 7)**.

Na katika aya nyingine anasema (swt):

يَسْمَعُ ءَايَٰتِ ٱللَّهِ تُتْلَىٰ عَلَيْهِ ثُمَّ يُصِرُّ مُسْتَكْبِرًا كَأَن لَّمْ يَسْمَعْهَا ۖ فَبَشِّرْهُ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ

**"Anayesikia aya za Mwenyezi Mungu akisomewa, kisha anang'ng'ania huku akijivuna, kama kwamba hakuzisikia basi mbashirie adhabu chungu." (Sura al-Jathiyah: 8)**.

Ni sahihi kwamba hizi aya zimepokewa katika mtiririko wa mazungumzo juu ya makafiri ambao walikataa kukubali Uislamu, lakini zinazungumzia juu ya msimamo mbaya katika kuamiliana na aya za Qur'ani Tukufu, kwa kuzipuuza kwake na kung'ang'ania katika kuzikhalifu kwake, na mwenye kusifika na sifa hizi anastahili adhabu kali ya Mwenyezi Mungu, na ingawa anaihesabu nafsi yake ni miongoni mwa Waislamu na Waumini.

Ama Hadithi na riwaya ambazo zinatahadharisha kitendo cha kupuuza kutekeleza amri na ujumbe wa Qur'ani na kutosheka na mwonekano wa nje, ni nyingi sana, tunataja baadhi ya mifano miongoni mwazo:



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 38 8/27/2015 2:17:24 PM

Imamu as-Sadiq عليه السلام katika kufasiri kauli yake (swt): **"Wale tuliowapa kitabu wanakisoma kama inavyostahiki kusomwa, hao ndio wanaokiamini." (Sura al-Baqarah: 121)**, amesema: "Wanasoma aya zake na wanafahamu maana zake, na wanafanyia kazi hukumu zake, na wanatarajia ahadi yake, wanaogopa adhabu yake na wanajifunza katika visa vyake, wanazingatia mifano yake na wanatekeleza maamrisho yake na wanajiepusha na makatazo yake, na wallahi sio kuhifadhi aya zake na kukariri herufi zake na kusoma sura zake na kudurusu ushuru (1/10) zake na khumsi yake (1/5), si kuhifadhi herufi zake na kupoteza mipaka yake, bali ni kutafakari aya zake, anasema (swt): 'Kitabu tumekiteremsha kwako chenye baraka ili watafakari aya zake.'"[11]

Hakika kauli yake عليه السلام: "Si kuhifadhi herufi zake na kupoteza mipaka yake" ni neno lenye kina sana linaweka mpaka wa upambanuzi baina ya kuzingatia dhahiri ya Qur'ani tu, na baina ya kushikamana na misingi yake na mifumo yake. Na amepokea Ibn Kathiri katika tafsiri ya kauli yake (swt): **"Wanasoma kama inavyostahiki"** kutoka kwa Ibn Abbas na kutoka kwa Abdillahi bin Masuud wamesema: "Kama inavyostahiki kuifuata."[12]

Na kutoka kwa Anasi kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم amesema: "Qur'ani sio kwa kisomo, na wala elimu si kwa kuipokea, lakini Qur'ani ni kwa uongofu na elimu ni kwa kuifahamu."[13]

Na kutoka kwa Ibn Umar kutoka kwa Mtume صلى الله عليه وآله وسلم: "Soma Qur'ani maadamu inakukataza na kama haikukatazi basi wewe huisomi."[14]

---

[11] Sayid Husein Tabatabai katika *al-Mizanu Fiy Tafsiril- Quar'an*, Juz. 1, Chapa ya Kwanza 1991, (Beirut Muasastu al- Ilimiy Lilimatubuaati) Uk. 262.

[12] Ismail bin Kathir al-Qarashiy ad Dimishiqiy katika *Tafsirul Qur'anil- Adhim*, Juz. 1, Chapa ya 1980, (Halab: Maktabatu Turathil- Islamiy), Uk. 163.

[13] *Kanzul- Umaal,* Hadithi 2462.

[14] Rejea iliyotangulia, Hadithi 2776.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 39 8/27/2015 2:17:24 PM

Na ni kiasi gani inaogopesha hadithi hii iliyopokelewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم: "Ni wangapi wanaosoma Qur'ani na Qur'ani inawalaani."[15] Lakini inabainisha ukweli ulio wazi, kwani mwenye kusoma kauli yake (swt): **"Eee laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu ya madhalimu." (Sura Hud: 18)**, ilihali yeye anafanya dhulma, na mwenye kusoma kauli yake (swt): **"Na tukajaalia laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu ya waongo." (Sura Imraan: 61)**, ilihali yeye anasema uongo makusudi, basi huyo na watu mfano wake ni miongoni mwa makusudio ya hadithi tukufu.

**Ratiba ya Maisha:**

Qur'ani sio matamko fasaha tu ambayo mwanadamu anaburudika kwa kuisoma, wala sio hazina ya kurithi ambayo mwanadamu analainika kwa kuisoma, na sio mkusanyiko wa nyuradi na dhikiri za kiroho ambazo mwanadamu anapata baraka kwa kuzisoma, hakika yenyewe ni zaidi ya hayo yote, ni ujumbe wa uongofu na ni ratiba ya maisha, hakika ni katiba ya vitendo na mkakati wa kujenga na kurekebisha. Na ni juu ya Mwislamu kuamiliana pamoja na kila aya ya Qur'ani kwa kuizingatia kuwa ni wito wa kazi na ni maamuzi ya taklifu, na hivyo atengeneze maisha yake, na kutengeneza hali yake kutokana na mwanga wa Qur'ani tukufu na maelekezo yake.

Na jambo linalotakiwa kupewa kipaumbele na umma juu ya Qur'ani tukufu ni kuitawalisha katika mambo ya maisha yao na kuitikia wito wake na kutekeleza mfumo wake na sharia zake katika nyanja mbalimbali. Ama umma ukikataa mfumo wa Qur'ani na ikatoweka thamani yake katika mazingira ya maisha yake na ukabadilisha hukumu zake kwa kanuni nyingine. Basi ujue kuwa hakika hayo ndio makusudio ya kuifanya Qur'ani mahame, na wakati huo hayatoufaa umma chochote mazingatio yake ya kijuu

[15] *Biharul-An'war*, Juz. 89, Uk. 185.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 40 8/27/2015 2:17:24 PM

juu unayoyafanya juu ya Qur'ani mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kama ambavyo umma hautonufaika na uzalishaji halisi wa Qur'ani, ikiwa hautachukua mwongozo wake kivitendo na kama haukuziweka aya zake katika sehemu za utekelezaji wa kivitendo. Na kama tutatafakari hali ya umma leo hii, na kuisoma katika mwangaza wa misingi na vipimo ambavyo vinalinganiwa na aya za Qur'ani Tukufu, tutakuta kuna bonde lenye kina kirefu linalotenganisha na kuna pengo kubwa baina ya hali unayoishi nayo umma na misingi ya Qur'ani Tukufu.

**Kutazama Katika Kitabu cha Ulimwengu:**

Na kati ya tofauti za mwanzo ambazo zinagongana na mwenye kutafakari katika hali ya umma na wito wa Qur'ani, ni jinsi umma unavyoamiliana na ulimwengu na mazingira, ambapo aya nyingi za Qur'ani tukufu zinatia mkazo zikilingania kutazama katika kitabu cha ulimwengu, na kugundua siri zake na kujua njia na kanuni ambazo zinatawala harakati zake. Hakika idadi kubwa kati ya sura za Qur'ani Tukufu zinabeba majina ya mwonekano wa kawaida na viumbe vya ulimwengu, na katika hayo kuna ishara ya wazi ya kujali mambo ya mazingira ya ulimwengu. Ambapo tunakuta katika majina ya sura za Qur'ani kwa mfano: al-Baqara, al-An'am, ar-Raad, an-Nahli, al-Kahfu, an-Nuur, an-Naml, al- Ankabuti, ad-Dukhan, Tuur, an-Najim, al-Qamar, al-Hadid, al-Jin, al-Insaan, at-Tak'uwir, al-Infitwaar, al-Inshiqaaq, al-Buruj, al-Fajir, as-Shamsi, al-llail, al-Dhuhaa, at-Tiyn, al-Alaq, al-Asri, al-Fiyl, al-Falaq, an-Naas.

Na tunakuta katika Qur'ani Tukufu aya nyingi zinamwamuru mwanadamu kutazama na kutafakari katika mambo ya mazingira na ulimwengu kama vile kauli yake (swt):



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 41 8/27/2015 2:17:25 PM

فَلۡيَنظُرِ ٱلۡإِنسَٰنُ إِلَىٰ طَعَامِهِۦٓ ﴿٢٤﴾ أَنَّا صَبَبۡنَا ٱلۡمَآءَ صَبّٗا ﴿٢٥﴾ ثُمَّ
شَقَقۡنَا ٱلۡأَرۡضَ شَقّٗا ﴿٢٦﴾ فَأَنۢبَتۡنَا فِيهَا حَبّٗا ﴿٢٧﴾

**"Hebu na atazame mtu chakula chake. Hakika tumeyamimina maji mminiko, kisha tukaipasua ardhi mpasuko. Tukaotesha humo nafaka." (Sura Abasa: 24 – 27)**.

Na kauli yake (swt):

فَلۡيَنظُرِ ٱلۡإِنسَٰنُ مِمَّ خُلِقَ ﴿٥﴾ خُلِقَ مِن مَّآءٖ دَافِقٖ ﴿٦﴾ يَخۡرُجُ مِنۢ بَيۡنِ
ٱلصُّلۡبِ وَٱلتَّرَآئِبِ ﴿٧﴾

**"Basi na atazame mtu ameumbwa kwa kitu gani.? Ameumbwa kwa maji yanayotoka kwa kuchupa, Yanayotoka baina ya uti wa mgongo na kifua." (Sura Twaariq: 5- 7)**.

Na kauli yake (swt):

قُلِ ٱنظُرُواْ مَاذَا فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلۡأَرۡضِۚ ﴿١٠١﴾

**"Sema, tazameni ni yapi yaliyomo mbinguni na yaliyomo ardhini! (Sura Yunus: 101).**

Na kauli yake (swt):



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 42 8/27/2015 2:17:25 PM

أَفَلَا يَنظُرُونَ إِلَى ٱلۡإِبِلِ كَيۡفَ خُلِقَتۡ ﴿١٧﴾ وَإِلَى ٱلسَّمَآءِ كَيۡفَ
رُفِعَتۡ ﴿١٨﴾ وَإِلَى ٱلۡجِبَالِ كَيۡفَ نُصِبَتۡ ﴿١٩﴾ وَإِلَى ٱلۡأَرۡضِ كَيۡفَ
سُطِحَتۡ ﴿٢٠﴾

**"Je hawamtazami ngamia jinsi alivyoumbwa? Na mbingu jinsi zilivyoinuliwa? Na milima jinsi ilivyosimamishwa? Na ardhi jinsi ilivyotandazwa?" (Sura al-Ghashiyah: 17 – 20)**.

Maelekezo haya mengi katika Qur'ani tukufu kuhusu mazingira na ulimwengu yanalenga kuimarisha imani katika upweke wa Muumba na utukufu Wake mosi, na pili ni mwanadamu kustawisha ardhi na kunufaika na kheri za ulimwengu.

Mwanadamu ni khalifa wa Mwenyezi Mungu katika ulimwengu na kinachotakiwa kwake ni kustawisha ardhi na yote yaliyopo katika maisha miongoni mwa nguvu na uwezo ulioandaliwa kwa ajili ya kunufaika na huduma yake, anasema (swt): **"Na amekudhalilishieni vyote vilivyopo mbinguni na ardhini." (Sura al-Jathiyah: 13)**. Huu ni wito wa Qur'ani, uko wapi na uhalisia wa Waislamu wa leo? Na ni upi upeo wa mwelekeo wao katika elimu ya mazingira na ulimwengu? Na ni kipi kiwango cha mafanikio yao ya kielimu na kivitendo?

Je, si ni uchungu sana kwamba mataifa ya ardhini yanashindana katika maarifa na elimu na kupata uvumbuzi na ugunduzi wa ziada, na kufanikisha mengi kati ya maendeleo ya kielimu na teknolojia, wakati ambapo umma wa Qur'ani unaiacha nafasi yake kando na mbali na harakati za maendeleo ya kielimu? Umma huu ambao Qur'ani yake inaanza kwa kulingania maarifa: "Soma" na



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 43 8/27/2015 2:17:26 PM

inasisitiza katika aya zake nyingi kutazama na kuchunguza kitabu cha ulimwengu, namna gani unaishi katika lindi la ujahili na kutoendelea na unawekwa katika orodha ya nchi zinazoendelea na katika ulimwengu wa tatu.

Hakika takwimu na namba zinazozungumzia kiwango cha utafiti wa kielimu katika ulimwengu wa Kiarabu na wa Kiislamu ukilinganisha na uhalisia wa elimu na maendeleo katika umma nyingine unadhihirisha  kina cha uduni wa maendeleo. Baadhi ya takwimu zinaonyesha kwamba nguvu za binadamu ambazo zinafanya kazi katika utafiti wa kielimu katika nchi ya Kiarabu hazizidi watafiti 8,000 wa Kiarabu wakati ambao kuna watafiti 400,000 katika Marekani na watafiti 400,000 Israeli.

Na kwamba utafiti wa kielimu haupati nafasi katika bajeti za nchi za Kiarabu isipokuwa asilimia moja, wakati ambapo vyuo vikuu vya Marekani vinatenga asilimia 40 katika bajeti yake ili kuimarisha na kupanua wigo wa utafiti wa kielimu. Na kwamba fungu la utafiti wa kielimu katika jumla ya pato la taifa la Kiarabu ni robo moja tu katika mia, mukabala wa asilimia 3 - 4 katika nchi zilizoendelea kiviwanda na teknolojia."[16]

Na takwimu za Unesco za mwaka 1993 zimedhihirisha kwamba licha ya kuwepo mamilioni ya wakazi katika nchi za Kiislamu, lakini fungu la nchi zote za Kiislamu katika utafiti wa kielimu uliosambazwa halivuki asilimia moja katika matawi yote ya elimu.[17] Waislamu wameshughulika na kutosheka na matukufu yaliyopita na kwa rekodi na ikhitilafu za kimadhehebu, na kwa mazingatio ya kijuu juu bila ya kujali wito wa Qur'ani unaopiga kelele na kulingania katika kuzingatia nyanja ya elimu ya mazingira

[16] Zainul-Abdiin Rukaabiy katika *Thamaniyatu Alaafi Baahithi Fiyl Watwaniy al- Arabiy Kulihi*, Jarida la al-Yamaamah, Toleo la 1604, Uk. 11.

[17] Dr. Rashid al-Mubaraka katika *Falsafatu al- Karahiyati*, Chapa ya Kwanza 2001, (Beirut Daru Swaadir) Uk. 95.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 44 8/27/2015 2:17:26 PM

na maisha, pamoja na kwamba wanasikiliza hizo Aya kutoka katika idhaa ya Qur'ani na kutoka kwa wasomaji wenye kujitahidi na katika majilisi na minasaba mbalimbali. Je huu si ukweli wa kuihama Qur'ani katika nyanja ya kivitendo na utekelezaji?

**Mifumo ya Uhusiano wa Kijamii:**

Kuratibu uhusiano baina ya watu katika msingi wa uadilifu na wema, ni kati ya malengo muhimu sana ya kushuka Qur'ani na ujumbe wote wa mbinguni, anasema (swt):

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِٱلْبَيِّنَٰتِ وَأَنزَلْنَا مَعَهُمُ ٱلْكِتَٰبَ وَٱلْمِيزَانَ لِيَقُومَ ٱلنَّاسُ بِٱلْقِسْطِ ۖ ﴿٢٥﴾

**"Kwa hakika tuliwatuma Mitume Wetu kwa dalili waziwazi, na tukateremsha Kitabu pamoja nao na mizani ili watu wasimamie uadilifu." (Sura al-Hadidi: 25)**.

Kwa sababu hiyo aya za Qur'ani tukufu zimetilia mkazo katika upande huu na zimetilia mkazo misingi muhimu. Ni wajibu mwanadamu ashikamane nayo katika uhusiano wake pamoja na ndugu yake mwanadamu, kama mtu binafsi na jamii, nayo ni misingi inayotokana na kukiri umoja wa ubinadamu, na kulingana kwa watu wake kama binadamu katika thamani na mazingatio, na kuneemeka kwa utukufu wa kibinadamu na kuheshimu uhuru wa mwanadamu na kuhifadhi haki zake za kimaanawi na za kimaada.

Hakika usalama wa uhusiano baina mtu na jamii na baina ya kundi lake na nguvu zake mbalimbali, kisha baina ya jamii na jamii nyingine ndani ya familia ya kibinadamu, unatengeneza lengo la msingi na kusudio la kimsingi la aya za Qur'ani na sharia za dini. Kuanzia



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 45 8/27/2015 2:17:26 PM

hapa Aya nyingi za Qur’ani zimezungumzia mambo ya uhusiano wa kijamii, kama mfumo wa jumla na kama sharia ndogo ndogo.

Qur’ani Tukufu imeshatilia mkazo juu ya misingi ya kufahamiana na kuheshimiana baina ya umma na mataifa ya binadamu, hivyo uhusiano baina yake sio uhusiano wa vita na mgongano, bali ni uhusiano wa kufahamiana, kuamiliana na kujadiliana, anasema (swt): **“Na tumewafanya kuwa mataifa na makabila ili mfahamiane.”** Na Qur’ani imeelekeza wafuasi wake kwenye kufuata siasa adilifu na wema wakati wa kuamiliana na jamii nyingine zenye kutofautiana kidini, maadamu ni zenye kujisalimisha na hazifanyi uadui, anasema (swt):

لَّا يَنْهَىٰكُمُ ٱللَّهُ عَنِ ٱلَّذِينَ لَمْ يُقَـٰتِلُوكُمْ فِى ٱلدِّينِ وَلَمْ يُخْرِجُوكُم مِّن دِيَـٰرِكُمْ أَن تَبَرُّوهُمْ وَتُقْسِطُوٓا۟ إِلَيْهِمْ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلْمُقْسِطِينَ ﴿٨﴾

**“Mwenyezi Mungu hawakatazi kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakuwapiga vita wala hawakuwatoa makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu.”**
**(Sura al-Mumtahinah: 8)**.

Na imekataza kuwafanyia ubaya wengine, kujeruhi hisia zao hata katika kiwango cha mazungumzo na maneno, na katika majadiliano ya kidini pamoja nao, anasema (swt): **“Wala msijadili watu wa Kitabu isipokuwa kwa njia iliyo bora zaidi.” (Sura Ankabuti: 46)**, na anasema (swt): **“Na semeni na watu kwa uzuri.” (Sura al-Baqarah: 83)**, na anasema (swt): **“Wala msiwapunguzie watu vitu vyao.” (Sura al- A’araaf: 85)**. Na imehadharisha ugomvi na mizozo ndani ya jamii ya Kiislamu: **“Wala msizozane mtashindwa na kupoteza nguvu yenu.” (Sura al- Anfal: 46)**. Na imeamuru



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 46 8/27/2015 2:17:27 PM

kushirikiana na kusaidiana: **“Na saidianeni katika wema na uchamungu.” (Sura al-Maidah: 2)**.

Na Qur’ani imekataza ukandamizaji na imelingania shura na kushirikisha watu katika kutafiti mambo yao na kadhia zao, anasema (swt): **“Na jambo lao ni shura baina yao.” (Sura Shuraa: 38)**. Na Qur’ani Tukufu imekataza kuwatuhumu watu katika dini zao: **“Na wala msimwambie mwenye kuwapa salamu: Wewe sio muumini.” (Sura Nisaa: 94)**.

Na Qur’ani imehadharisha katika Aya nyingi ukiukwaji wa haki ya yeyote ya kimaada au kimaanawi: **“Wala msifanyiane uadui, hakika Mwenyezi Mungu hapendi wanaofanya uadui.” (Sura Maidah: 78)**. Na inatarajiwa katika umma ambao unabeba Qur’ani kwamba waishi maisha mazuri zaidi yenye utulivu wa kijamii, kwa kushikamana na misingi ya uadilifu, uhuru, heshima, utu na kuhifadhi haki. Lakini mtazamo wa udadisi wa hali ya umma unadhihirisha hali ambayo wanakabiliwa nayo watu wengi katika umma na mataifa ya Kiislamu, hali ya kukosa utulivu wa kijamii, wakati ambapo zinaneemeka jamii nyingine kwa aina fulani ya utulivu kwa matokeo ya kukubali tofauti, kuheshimu rai za wengine na kushiriki katika mbambo ya umma.

Hakika Qur’ani Tukufu inalingania umoja wa umma na zinasomwa Aya za kulingania umoja katika masikio ya Waislamu usiku na mchana, kama vile kauli yake (swt): **”Na hakika umma wenu huu ni umma mmoja na Mimi ni Mola Wenu basi niabuduni.” (Sura al-Muuminina: 52)**. Na kauli yake (swt): **“Na shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu nyote na wala msifarikiane.” (Sura Imran: 103)**. Na kauli yake: **“Wala msizozane mtashindwa na kupotea nguvu yenu.” (Sura Anfal: 46)**. Na mfano wake miongoni mwa Aya Tukufu.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 47 8/27/2015 2:17:27 PM

Kwa nini umma katika nchi zake nyingi unaishi katika hali ya mfarakano na mkanganyiko wa ndani? Wakati ambapo watu wa Ulaya wanaishi kwa ushirikiano licha ya kutofautiana katika lugha zao mbalimbali, mataifa yao mengi na madhehebu yao yanayotofautiana, maslahi yao ya kisiasa na ya kiuchumi yenye ushindani, na wao sasa hivi wanaimarisha umoja wao kupitia uzio wa muungano wa Ulaya, ambao unazidi kuboreka siku hadi siku na idadi ya nchi zimefikia 27.

Hakika hali mbaya ambayo unaishi nayo umma katika nyanja za mkanganyiko wa uhusiano wake wa ndani, ni kutokana na kutojali na kupuuza kwake misingi mitukufu ambayo imesisitizwa na Qur'ani katika kuratibu uhusiano wa kijamii, na huo ni ukweli ulio wazi katika maana ya kuifanya Qur'ani ni mahame.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 48 8/27/2015 2:17:27 PM

# VIJANA NA KUREJEA KWENYE QUR'ANI

Kurejea kwenye Qur'ani ndio kujinasua kwa mwanadamu kutokana na ubaya na uovu ambao unamkabili licha ya kuwepo maendeleo makubwa ya kimaada na kiteknolojia. Na kurejea kwenye Qur'ani ndio njia ya umma wa Kiislamu ya heshima, utukufu na kuvuka hali ya kutoendelea. Ni wapi tutaanzia safari ya kurejea kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu? Na ni kundi lipi litaongoza msafara wake?

Wakati zilipoteremka Aya za Qur'ani Tukufu kwa mara ya kwanza kwa Nabii wetu Mtukufu Muhammad صلى الله عليه وآله وسلم, hakika nyoyo za vijana ndio ambazo zilipokea Qur'ani, na ndimi zao ndio ambazo ziliifikisha kwenye masikio, na mikono yao iliingia katika vita vya Jihadi ili kuimarisha mfumo wa Qur'ani katika maisha. Mtu wa kwanza aliyetangaza Aya za Qur'ani alizozisikia kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم alikuwa ni kijana mbichi akiwa katika mwanzo wa umri wa ujana wake naye ni Ali bin Abutalib عليه السلام, ambaye aliielewa Qur'ani Aya kwa Aya na herufi kwa herufi kama anavyosema عليه السلام: "Niulizeni kabla hamjanikosa. Naapa kwa ambaye ameumba punje na kuumba viumbe, kama mtaniuliza juu ya Aya moja moja nitawaambia ni wakati gani ilishuka na wapi imeshukia, na nitawaambia ni ipi yenye kufuta na ni ipi yenye kufutwa, ya umakhususi na ya ujumla, muhkamu na mutashabihi, iliyoshukia Makkah na iliyoshukia Madina."

Na anasema عليه السلام katika maneno mengine: "Hakika mimi ninajua Nasikh yake na Mansukhu yake, muhkamu yake na mutashabihi yake, fasili yake na kiungo chake, herufi zake na maana zake,

Wallahi hakuna herufi iliyoshuka kwa Muhammad Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم isipokuwa na mimi najua wapi imeshuka na katika siku gani imeshuka na katika sehemu gani imeshuka."[18] Hadi ulipokatika wahyi kwa kufariki Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم na ikakamilika kushuka kwa Qur'ani Ali عليه السلام alikuwa bado yuko katika umri wa ujana, ambapo umri wake haukuvuka miaka 33.

Na wa kwanza kutangaza Qur'ani mbele ya mkusanyiko wa watu alikuwa ni kijana wa Kikuraishi Abdillahi bin Masuud naye ni wa sita katika waliotangulia kusilimu, na anazungumza juu ya msimamo wake wa kishujaa mmoja wa masahaba kwa kusema: Mtu wa kwanza kuitangaza Qur'ani baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم Makkah ni Abdillahi bin Masuud (r.a) ambapo siku moja masahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم walikusanyika wakasema: Wallahi Makuraishi hawajasikia hii Qur'ani ikitangazwa kabisa, ni mwanaume gani atawatangazia? Abdillahi bin Masuud akasema: "Mimi.

Wakasema: Hakika sisi tunawahofia juu yako, bali tunataka mtu mwenye familia itakayomkinga na watu watakapokusudia kumdhuru. Akasema: "Niacheni hakika Mwenyezi Mungu atanikinga." Ibn Masuud alitoka hadi katika Maqam Ibrahim عليه السلام, wakati wa asubuhi na Makuraishi wako katika vilabu vyao akasimama katika Maqam Ibrahim عليه السلام kisha akasoma: "Bismillahi Rahman Rahim" kwa kunyanyua sauti yake "Rahman". Kisha akawaelekea akiisoma "Bismillahi Rahman Rahim". Wakatafakari wakasema: Anasemaje mtoto wa Ummi Abdi? Hakika yeye anasoma baadhi ya aliyokuja nayo Muhammad. Wakasimama wakamwendea wakawa wanampiga uso wake naye anaendelea na kisomo chake, hadi akafikia alipotaka Mwenyezi Mungu afikie. Kisha akarejea kwa maswahiba zake

[18] *Biharul-An'war*, Juz. 89, Uk. 87, Hadithi 23.

akiwa amejeruhiwa uso wake na mwili wake wakasema: "Haya ndio tuliyoyakhofia juu yako."

Akasema: "Maadui wa Mwenyezi Mungu hawakuwa wepesi kwangu kuliko hivi sasa, kama mtataka basi kesho asubuhi nitawaendea kama nilivyowaendea leo." Wakamwambia: Imetosha, hakika umeshawasikilizisha wanayoyachukia. Kijana Ibn Masuud alikuwa anasoma Qur'ani kwa bidii ya kweli hadi imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwamba alisema: "Mwenye kutaka kusikiliza Qur'ani sawa sawa kama ilivyoshuka basi aisikilize kutoka kwa mtoto wa Ummi Abdi."[19]

Na wa mwanzo kubeba Aya za Qur'ani Tukufu kwenda nazo Madina na akawafundisha watu wake Qur'ani na akauandaa mji wa Madina ili kuwa ni uhamisho wa Mtukufu Mtume ﷺ na nyumba ya Uislamu ni kijana mwanajihadi Mus'ab bin Umair, ambaye alijiunga na Uislamu katika umri wa ujana wake ambapo alichukua Aya ambazo alizisikia kwa mara ya kwanza kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika nyumba ya Arqam bin Abi Arqam kwa moyo wake wote na zikafanya mabadiliko ya haraka katika uwepo wake na mtazamo wake wa maisha. Akaachana na maisha ya kudekezwa, israfu na raha, ambapo alikuwa ni kati ya vijana matajiri hapo Makkah kama anavyosema juu yake Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ: "Nilimuona Mus'ab na hakukuwa Makkah kijana mwenye neema zaidi kwa wazazi wake kuliko yeye, lakini aliacha yote hayo kwa kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake ﷺ".

Na alivutika mzima mzima kwenye Qur'ani na akaishibisha nafsi yake dhana zake na maana yake, na zikajikita katika akili yake na moyo wake Aya zake na Sura zake, Mtukufu Mtume ﷺ akamchagua kuwa balozi wa kwanza wa Kiislamu nje ya Makkah,

[19] *Biharul-An'war*, Juz. 31, Uk. 213.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 51 8/27/2015 2:17:27 PM

akampendekeza kwa ajili ya kuwafundisha watu wa Madina Qur'ani na kuwafahamisha na kuwafunza dini.

Na katika Masahaba wa Mtume صلى الله عليه وآله وسلم siku hizo kulikuwa na ambao ni wakubwa kuliko yeye kwa umri na wenye jaha zaidi na walio karibu zaidi na Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم kwa udugu, lakini Mtume صلى الله عليه وآله وسلم akamchagua Mus'ab al-Khairi, naye anajua kwamba anampa jambo kubwa na anamkabidhi hatima ya Uislamu huko Madina, mji ambao utakuwa ndio makazi ya uhamisho wake na sehemu ya daawa yake."[20] Hiyo ni mifano na vigezo vya kizazi cha vijana walioelewa Qur'ani mwanzoni mwa kushuka kwake, ambao walibeba ujumbe na mfumo wa maisha na wakajengeka katika mwanga wa uongofu wake msingi wa maendeleo makubwa ya Kiislamu.

Ama ni kwa nini vijana ndio waliokuwa kizazi kilichoitikia zaidi wito wa Qur'ani kuliko wasiokuwa wao? Hiyo ni kwa sababu zifuatazo:

1. Hakika wao walikuwa katika hatua ya kukua kifikra na kutengeneza utambuzi, walikuta mbele yao maswali muhimu ya siri ya maisha, na sababu ya uwepo na lengo la kuumbwa kwao, na waliona katika Qur'ani Tukufu mwongozo na uongofu wenye majibu yenye kutatua na kukinaisha, ambayo yanaafikiana na maumbile na mantiki na uhalisia wa akili.
2. Na kama vijana wenye upevu wa hisia na mawazo, walikuwa wanahisi uovu wa hali ya ujahili uliopo, ikiwa ni pamoja na ibada ya masanamu na ufisadi wa kimaadili na kuenea vita na fitina, lakini wao hawajui njia ya kujinasua na ya utatuzi, na aya za Qur'ani zilikuja kuwapa uoni na

[20] Khalid Muhammad Khalid katika *Rijalu Haula Rasuuli*, Chapa ya 1422 Hijiria, (Beirut Darul- Fikri ), Uk. 27.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 52 8/27/2015 2:17:27 PM

nuru na kuweka nyayo zao katika njia ya ufaulu na salama, wakaipokea kwa moyo mkunjufu na kwa msukumo.

3. Nyoyo zao zilikuwa safi na twahara kuliko wengine, kwa sababu wao ni wapya katika maisha, maslahi hayajatawala katika nafsi zao na mabaya hayajatawala katika akili zao, na maovu na ufisadi havijajikita katika nyendo zao, na msukumo wa kujishughulisha kwao na ufisadi ulikuwa ni dhaifu, jambo lililowafanya wawe na uwezo zaidi wa kuwa huru na kuponyoka katika udhibiti wa matamanio na kuondoka kuelekea kwenye wigo mpya.

4. Hatua ya ujana hutengeneza kwa mwanadamu hali ya kujiamini na raghaba ya kujiingiza na kutarajia mustakabali bora zaidi, na hali hiyo inaoana na uongofu wa Aya za Qur'ani Tukufu na hivyo hutengeneza mazingira yanayofaa na kumwezesha mtu kuamiliana nayo.

5. Kitendo cha Mtume صلى الله عليه وآله وسلم kuwaelekea, kuwajali na kuwapokea, ikiwa ni pamoja na yale aliyokuwa anawapa miongoni mwa upendo na upole na kuwaonyesha heshima na kuwajali, katika jamii ambayo umri na mali ilikuwa ni sehemu ya heshima na uongozi, yote hayo yaliwavutia kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم na kuwavutia kwenye ujumbe wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Tabia njema ambayo alipambika nayo Mtume صلى الله عليه وآله وسلم na ikawaenea vijana wale wenye kupotea wenye kupuuzwa katika jamii yao ndio iliyotengeneza shakhisiya yao ya uongozi na kuibua vipaji vyao, uwezo wao na matarajio ya kuelekea katika utukufu na maendeleo.

Na kama ilivyoanza harakati ya Qur'ani Tukufu katika mikono ya vijana, hakika hatua ya kurejea kwenye Qur'ani itakuwa katika

mikono yao yenye baraka inshaallah. Mwenye kuchota kutoka katika Qur'ani na kunywa maji yake matamu katika muda wa ujana wake, hakika nafsi yake, fikra zake, vitendo vyake na tabia yake, vyote vitajengeka juu ya uongofu wa wahyi, kwani shakhisiya ya mwanadamu mafunzo yake hupata ubora na sifa zake hupangika katika kipindi cha ujana, na ikiwa yuko karibu na Qur'ani na ni mwenye kujifunza kutoka katika Aya zake, basi atakuwa ni mtu wa Qur'ani katika mwelekeo wake na mwenendo wa maisha yake.

Imepokewa katika Hadithi ya Imamu Ja'far as-Sadiq عليه السلام kwamba amesema: "Mwenye kusoma Qur'ani naye ni kijana muumini, basi Qur'ani itachanganyika na nyama yake na damu yake, na Mwenyezi Mungu atamjaalia kuwa pamoja na malaika wema watukufu, na Qur'ani itakuwa ni kinga yake Siku ya Kiyama."[21]

Hakika viashiria vingi vinavyoonekana katika anga vinatabiri mustakabali wa kurejea umma wetu wa Kiislamu katika mikono ya vijana wake watukufu waumini, huu hapa mwamko mtukufu wa Kiislamu, na shughuli za kidini zimeenea katika sehemu mbalimbali katika ulimwengu wa Kiislamu, vipindi vya Qur'ani katika upande wa kuisoma, kuihifadhi na kuifundisha, na pia tafsiri yake ambayo wanaikubali vijana, yote hayo ni bishara za kheri juu ya mwamko wa maendeleo yanayokuja.

[21] Muhammad bin Yaaqub al-Kulainiy katika *al-Kaafiy*, Juz. 2, Chapa ya 1405 Hijiria, (Beirut Darul- Adhuwai), Uk. 703.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 54 8/27/2015 2:17:27 PM

# HARAKATI ZA UTAMBUZI NA MAARIFA KATIKA JAMII

Kiwango cha maendeleo ya jamii yoyote ile hupimwa kwa kiwango cha ukuaji wa utambuzi na maarifa ndani ya jamii husika, na ni kutokana na msingi huo hupatikana nafasi ya jamii na hutengenezwa shakhisiya za jamii husika. Na utambuzi kama wanavyosema maulamaa wa lugha ya Kiarabu ni: "Kuhifadhi kitu kwa moyo. Na katika Hadithi: Mwenyezi Mungu amng'arishe mtu ambaye ameyasikia maneno yangu kisha akayatambua." Yaani akayafahamu. Na katika Hadithi ya Abi Umamah: "Mwenyezi Mungu hatoadhibu moyo ulioitambua Qur'ani." Amesema Ibnu Al-Athiri: Yaani ameifahamu kwa kuiamini na kuifanyia kazi. Ama mwenye kuhifadhi matamko yake na akapoteza mipaka yake huyo si mwenye kuitambua."[22] Hakika chombo kimeitwa chombo kwa sababu kinahifadhi kinachowekwa humo.

Na imekuja katika Qur'ani tukufu: **"Ili tuyafanye hayo kuwa ni waadhi kwenu na kila sikio linalosikia liyatambue." (Sura al-Haaqah: 12)**. Hiyo ni katika mtiririko wa kusimulia habari za umma zilizotangulia, namna gani ilikuwa hatima yao katika maangamio, kwa sababu ya kupotoka kwao katika mfumo wa Mwenyezi Mungu na ufisadi wao wa kijamii. Ambapo Aya Tukufu zinaashiria kwamba habari hizi na taarifa hizi za kihistoria sio kwa ajili ya kujiliwaza au kiburudisho cha kifikra, bali makusudio yake ni kupata utambuzi kwa kufahamu njia za maisha na kanuni za kihistoria, na mazingatio kwa sikio linalosikia; Kwa sababu sikio aghlabu ndio dirisha la mwanadamu la kusikia habari za historia zilizopita, nalo ni chombo

[22] Muhammad bin Mukaram bin Mandhur katika *Lisanul-Arabi*, Juz. 6, Chapa ya 14008 (Beirut Darul Jiyl, Darul Lisanil- Arabi), Uk. 954.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 55 8/27/2015 2:17:27 PM

tu cha kufikisha, kufahamu na kutambua kunatimia nyuma ya sikio ambapo moyo wa mwanadamu na fikra yake ndio chombo ambacho humo zinakusanyika taarifa na kuchujwa ili kubadilika na kwenda kwenye fikra, mtazamo na zao.

Ama *maarifa* katika lugha ni kufahamu na kuelewa. Na katika istilahi neno *Maarifa* lina maana nyingi zinazidi mia moja, na zilizo mashuri zaidi ni ile aliyoieleza Tailar, mtaalaumu wa intoprojia wa Kiingereza, ambaye ametambulisha *Maarifa* kwamba ni: "Umbo lililotengenezwa na taarifa, itikadi, fani, tabia, ada na mila ambazo anazichuma mwanadamu kwa sifa yake ya kuwa ni kiungo katika jamii."

**Maarifa na Utambuzi Katika Maisha ya Mwanadamu:**

Kila mwanadamu anafahamu nafasi ya maada katika maisha yake, na ni kwayo huratibu mambo ya maisha yake miongoni mwa chakula, mavazi, malazi na mfano wa hayo, lakini mchango wa utambuzi na maarifa hauko wazi kwa walio wengi, ambapo hawazingatii kuwa ni katika mambo ya msingi ya kimaisha, bali ni jambo la ukamilisho na la ziada.

Na uhalisia ni kwamba maisha ya mwanadamu yanaathiriwa na maarifa yake na utambuzi wake, na kila anapokuwa na maarifa na utambuzi wa juu zaidi ndivyo maisha yake yanavyokuwa ya juu zaidi na bora zaidi, na kuteremka kwa kiwango cha maarifa ni sababu ya kuteremka na kuporomoka kiwango cha maisha kwa ujumla. Kwa mfano katika nyanja ya afya kuna tofauti iliyo wazi baina ya mwenye maarifa na utambuzi wa kanuni za afya na yule asiyekuwa na utambuzi huo, na tofauti inadhihirika zaidi katika aina ya chakula na katika njia ya maisha, kuamiliana pamoja na maradhi na matukio, bali hata katika kuamiliana na viungo vya mwili wake, ni maradhi mangapi ya hatari yanapatikana kwa sababu ya matumizi mabaya



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 56 8/27/2015 2:17:27 PM

na vitendo vya kimakosa vinavyotokana na ujahili na kutokuwa na utambuzi?

Na katika upande wa mali hakika wazalishaji bora zaidi ni wale wanaotegemea uzalishaji wao harakati za uchumi na kufahamu athari za matukio na mabadiliko. Utambuzi wa mwanadamu na maarifa yake katika nyanja hii unamfanya awe ni mwenye uwezo zaidi katika kutumia fursa na kupata faida, wakati ambapo asiyefuatilia harakati za uchumi zinampita fursa nyingi na anapata hasara ya maslahi na manufaa.

Na mfano wa karibu katika hilo ni yale ambayo yametajwa na baadhi ya ripoti za kiuchumi kwamba Waarabu wanapata hasara ya zaidi ya dola 250 milioni kila mwaka huko Ulaya, kutokana na ujinga wao na kughafilika kwao na kanuni ya kurejeshewa kodi ya ziada. Katika nchi za muungano wa Ulaya kodi inachukuliwa katika kila bidhaa au mauzo kutoka kwa mwananchi na mkazi. Ama mtalii anaweza kurejeshewa kodi anayoitoa katika nguo na vifaa vingine ambavyo ni bidhaa ambazo anazinunua kama zawadi, kwa kupeleka stakabadhi katika kitengo maalumu kilichopo uwanja wa ndege wakati wa kuondoka, lakini walio wengi hawajui hilo au hawajali na hivyo hupata hasara ya kiasi kikubwa cha mali.

Na sasa hivi tunakuta katika jamii zetu namna gani baadhi ya watu wanamiliki kiasi kibubwa cha mali, kama vile wastaafu ambao wanapokea mafao yao na haki zao kutoka katika mashirika wanapofikia umri wa kustaafu lakini wao hawajui namna ya kuitumia na kuiendeleza na hupotea mikononi mwao hapa na pale.

Kama tunavyoona baadhi ya watu wanaishi katika hali mbaya ya kiuchumi pamoja na kwamba wana pato la kutosha, isipokuwa wao hawategemei mipango na uendeshaji katika matumizi yao na masurufu yao. Na mfano wa hayo yanatokea katika maisha ya familia na uhusiano wa kijamii, ambapo maarifa na utambuzi una



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 57 8/27/2015 2:17:27 PM

dauru ya msingi katika kufaulu kwa mtu na kunyanyuka kwake, wakati ambapo wasio na maarifa na utambuzi wa mambo mara nyingi wanapatwa na mdororo na misukosuko kwa sababu ya ujahili na ukosefu wa utambuzi.

**Utambuzi wa Kidini:**

Utambuzi na maarifa katika nyanja ya kidini una umuhimu mahususi, kwa sababu dini ya mwanadamu ni wajibu iwe ni matokeo ya kukinaika kwake, imani na msukumo wa dhati, na sio hali ya kuiga, au ufuataji wa kurithi au wa kijamii. Kama ambavyo dini ina maadili na misingi, malengo na madhumuni, ikiwa utambuzi haujapatikana kwa mwanadamu katika hilo, dini yake inakuwa ni mwonekano na vitendo vya kijuu juu tu visivyo na maana.

Na udhaifu wa utambuzi katika dini unamsababishia mwanadamu hatari mbili kubwa: Ama kujivua kutokana na dini na hususani anapokumbwa na kimbunga cha shaka na mielekeo kinzani, na hivyo kukosa kinachomkinga miongoni mwa utambuzi na maarifa imara. Au kutumiwa kwa jina la dini na viongozi wa kimaslahi na nguvu za uovu. Katika mwanzo wa mwaka wa 2000 yalitokea maovu yenye kutisha Kusini Magharibi mwa Uganda katika mikono ya kasisi anayenasibiana na kanisa Katholiki, anayeongoza harakati za kidini kwa jina la 'Kundi la Kuhuisha Amri ya Kumi', na aliwakinaisha wafuasi wake kwamba mwisho wa ulimwengu umekaribia, na kitatokea Kiyama. Na akawahamasisha kuuza nyumba zao na mali zao ili wanunue kupitia kwayo sehemu na kasiri peponi. Na akawapangia siku maalumu na saa maalumu ili waingie kanisani na kuweka ukomo wa maisha yao katika mikono yao ili roho zao ziungane na ufalme wa mbinguni. Na kwamba yeye atasafiri kwenda Ulaya, na kutokea huko atawatangulia peponi ili akapokee roho zao! Na waliingia katika kanisa lao watu 470



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 58 8/27/2015 2:17:27 PM

takriban na wakafungiwa milango na madirisha na wakaipigilia misumari ili asifikirie yeyote kukimbia na kutoka na kupoteza fursa ya kuhamia katika pepo ya Firdausi na wakamwagia mafuta pembezoni mwa kanisa na wakawasha moto na wote wakafa kwa kuungua na kuteketea na miongoni mwao wakiwemo watoto na wanawake!!

Vyombo vya habari vikatoa taarifa na uchambuzi kuhusu msukumo wa tukio hilo. Hakika tukio hili ni mfano wa wazi wa upotoshaji na kutumia dini vibaya. Ujahili na udhaifu wa utambuzi na maarifa hutoa fursa ya kupatikana mwonekano na vitendo vya aina hii. Na ndani ya kila dini au kila madhehebu inaweza kujitokeza na kukua nguvu ya vituo vinavyotumia dini kwa ajili ya kukandamiza watu na kuwatumia vibaya. Na tumeona hadi wakati wetu huu namna gani yametokea makundi na harakati potovu kwa jina la Uislamu yamewasukuma wafuasi wake kwenye vitendo viovu vya kigaidi na nyendo mbovu zisizo na maendeleo.

Hakika utambuzi sahihi wa kidini na maarifa sahihi ndio dhamana ya kuwa na msimamo na kuvuka majaribio ya kutumiwa na kupotoshwa. Imekuja katika *Sahih Bukhari* kutoka kwa Abdur-Rahman kutoka kwa Ali bin Abu Talib عليه السلام kwamba amesema: “Mtume صلى الله عليه وآله وسلم alituma kikosi kidogo cha jeshi na akampa uongozi wake mwanaume wa Kianswari na akawaamuru wamtii - siku moja - akakasirika akasema: ‘Je, Nabii si amekuamuruni mnitii?’ Wakasema: ‘Ndio’, akasema: ‘Basi nikusanyieni kuni.’ Wakakusanya. Akasema: ‘Kokeni moto’, wakakoka. Akasema: ‘Ingieni’, baadhi yao wakataka kuingia, wengine wakawa wanawazuia wenzao na kusema: ‘Tumekimbilia kwa Nabii صلى الله عليه وآله وسلم kuukimbia moto.’ Hawakuacha kuvutana hadi moto ukazimika na ikatulia hasira yake. Habari zilipomfikia Nabii صلى الله عليه وآله وسلم akasema:



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 59 8/27/2015 2:17:27 PM

‘Kama wangeingia basi wasingetoka humo hadi siku ya Kiyama, utii ni katika mema.’”[23]

Hivyo utambuzi na maarifa vina athari kubwa sana katika maisha ya mwanadamu katika nyanja mbalimbali. Na mwanadamu kila anapokuwa na maarifa na utambuzi zaidi maisha yake yanakuwa ya juu na bora zaidi, kwani sio jambo dogo na la ukamilisho, kwa sababu mwanadamu vitendo vyake vinatokana na misimamo yake katika kukinaika kwake na fikra zake; maarifa bora zaidi yanazaa imani na rai bora zaidi na inaakisi katika nyendo za mwanadamu na harakati zake.

**Mtazamo wa Dini:**

Nususi za kidini zinalipatia suala la utambuzi na maarifa umuhimu mkubwa ambao haulingani na umuhimu wowote. Qur’ani Tukufu inakiri kwamba kuna tofauti yenye kupambanua isiyopingwa baina ya wajuzi wawili wenye utambuzi na wasiokuwa wao, na inauliza kwa njia ya kukiri na kuthibitisha: **“Sema je, wanalingana wale wanaoujua na wale wasiojua.”? (Sura Zumar: 9)**. Na inatosha kujua kwamba Aya ya mwanzo kushuka katika Qur’ani Tukufu ni kulingania katika utamaduni wa utambuzi na maarifa, anasema (swt):

ٱقۡرَأۡ بِٱسۡمِ رَبِّكَ ٱلَّذِى خَلَقَ ﴿١﴾ خَلَقَ ٱلۡإِنسَٰنَ مِنۡ عَلَقٍ ﴿٢﴾ ٱقۡرَأۡ
وَرَبُّكَ ٱلۡأَكۡرَمُ ﴿٣﴾ ٱلَّذِى عَلَّمَ بِٱلۡقَلَمِ ﴿٤﴾ عَلَّمَ ٱلۡإِنسَٰنَ مَا لَمۡ يَعۡلَمۡ

**“Soma kwa jina la Mola Wako aliyeumba. Amemuumba mtu kwa pande la damu. Soma na Mola Wako ni Karimu sana. Ambaye**

[23] Muhammad bin Ismail al-Bukhariy katika *Sahih Bukhariy*, Juz. 3, Kitabu al- Maghaaziy, Chapa ya Kwanza 1420, (Beirut Darul- Kutubi al- Ilimiya), Uk. 104, Hadithi 4340.

**amefundisha kwa kalamu. Amemfundisha mtu aliyokuwa hayajui." (Sura al-Alaq: 1- 5)**.

Hakika ni amri ya kusoma, yaani kupata ufahamu na maarifa, na kuielezea kalamu kama ni chombo cha elimu na kufundishia. Na kuna Sura nyingine kwa jila la 'Kalamu' Mwenyezi Mungu Mtukufu ameianza kwa kuapa kwa kalamu na kinachoizunguka, katika jamii iliyokuwa inatawaliwa na ujinga na wanaoweza kusoma na kuandika humo ni idadi ndogo sana, anasema (swt): **"Nun. Naapa kwa kalamu na wanachokiandika." (Sura al-Qalamu: 1)**.

Na kuna Hadithi na riwaya nyingi zinazozingatia utambuzi wa mwanadamu na maarifa yake kuwa ni kipimo cha kiwango cha dini yake na nafasi yake mbele ya Mwenyezi Mungu, kama vile Hadithi iliyopokelewa kutoka kwake صلى الله عليه وآله وسلم: "Aliye mbora kati ya waumini kwa imani ni yule mbora wao kwa maarifa." Na kama vile Hadithi iliyopokelewa kutoka kwa Maimamu wa Ahlulbait عليهم السلام: "Baadhi yenu ni wengi wa Swala kuliko baadhi, na baadhi yenu ni wengi wa Hija kuliko baadhi, na baadhi yenu ni wengi wa kutoa sadaka kuliko baadhi, na baadhi yenu ni wengi wa kufunga kuliko baadhi, na mbora wenu ni yule aliye mbora wenu kwa maarifa."[24]

Na imepokewa kutoka kwa Nabii صلى الله عليه وآله وسلم: "Saa moja ya mwanachuoni anayeegemea katika godoro lake akitafakari katika elimu yake ni bora kuliko ibada ya mja ya miaka sabini."[25] Na imekuja kutoka kwa Imamu Ja'far as-Sadiq عليه السلام: "Ubora wa elimu unapendeza kwangu zaidi kuliko ubora wa mja."[26] Na tunasoma katika *Mafatihul-Jinan* kitabu ambacho ni mahususi kwa dua, ziyara, suna na nyuradi, cha mtunzi maarufu kwa uchamungu na

[24] *Biharul-An'war*, Juz. 3, Uk. 14.
[25] *Biharul-An'war*, Juz. 2, Uk. 23.
[26] Rejea iliyotangulia, Uk. 18.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 61 8/27/2015 2:17:28 PM

kujinyima, Sheikh Abbas al-Qummiy ﷺ, kuhusu amali za Lailatul-Qadri, na baada ya kutaja sunna mbalimbali humo miongoni mwa Swala na dua na nyuradi za usiku wa ishirini na moja na ishirini na tatu katika mwezi wa Ramadhani anasema: "Na amesema Sheikh wetu Suduqu: 'Kati ya waliyosimulia masheikh ni kwamba: Na mwenye kuhuisha mikesha hii miwili kwa kudurusu elimu ni bora zaidi.'"[27]

## Kujielimisha:

Kujua thamani ya utambuzi na maarifa na kuitikia maelekezo ya kidini, inamaanisha kila mwanadamu kuzingatia suala la kuielimisha nafsi yake na kupata kiwango kikubwa cha utambuzi katika dhati yake, hususan na sisi tunaishi katika zama ambayo kumeenea humo njia za elimu na maarifa na fursa ya kujielimisha na kupata utambuzi.

Tovuti kwa mfano, ni kati ya mafanikio muhimu ya mwanadamu katika zama hizi. Inafungua mbele ya mwanadamu wigo wa elimu na maarifa kwa anayetaka, lakini kwa masikitiko makubwa, baadhi wanatumia vibaya njia hii muhimu, wanaitumia katika mwelekeo mbaya. Mwishoni mwa mwaka 2011 idadi ya waliojiunga na tovuti katika kiwango cha ulimwengu ni bilioni 2.29, na katika Mashariki ya Kati ambayo idadi ya wakazi wake inafikia milioni 216, idadi ya waliojiunga na tovuti inafikia milioni 72 kwa wastani wa asilimia 33.5 ya wakazi, na asilimia 3.1 ya watumiaji wa tovuti ulimwenguni. Wakati ambapo idadi ya waliojiunga katika Waisraeli madhalimu inafikia milioni 5 na 263 elfu, na idadi ya wakazi wake ni watu milioni 7 na 473 elfu, asilimia 70.4 katika jumla ya idadi ya wakazi![28] Na katika hilo kuna ishara juu ya udhaifu wetu katika kiwango cha ulimwengu katika kujielimisha na kujiongezea utambuzi na uwelewa.

[27] Abbasi al- Qummiy katika *Mafaithul-Jinan*, Chapa ya Kwanza 1412 Hijiria, (Beirut muasastu al- Ilimiy Lilimatubuaati), Uk. 296.

[28] http// www.internetworldstats5.htm



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 62 8/27/2015 2:17:28 PM

Hakika sisi tunajinasibisha na umma ambao dini yake inaanza kwa kulingania kusoma "Soma", ni kwa kiasi gani kusoma kunachukua nafasi katika mfumo wa maisha yetu na wakati wetu? Kitabu ni chanzo kati ya vyanzo vya utambuzi na maarifa, inapasa kila mmoja kuzingatia uhusiano wake na kitabu na tulee familia zetu na watoto wetu katika kuwa na mafungamano na kitabu. Katika nchi za Magharibi maktaba imekuwa ni sehemu ya mahitaji ya nyumba na familia, kwa sababu hiyo hakika mpango wowote au mkakati wowote wa nyumba na samani ni lazima uwe na kabati la vitabu, na kwa kuwa njia ya kujenga na samani kwetu imepokewa kutoka kwao hakika aghlabu nyumba zetu sasa hivi zina sehemu ya vitabu, lakini inatumika kwa vitu vingine, kwa sababu ya udhaifu wa utambuzi na mazingatio yetu katika kusoma na kujielimisha.

**Harakati za Kujielimisha:**

Watu wa jamii kujali na kutilia umuhimu suala la kujielimisha inategemea na kiwango cha shughuli na harakati za kujielimisha zinazofanywa na jamii kwa ujumla katika nchi. Ikiwa katika jamii kuna harakati na shughuli za kujielimisha, hakika hali hiyo itatengeneza mazingira yenye kusukuma na kushajiisha idadi kubwa ya wanajamii kujikita katika shughuli za utambuzi na maarifa na kupanua duara la maarifa katika jamii.

Na maneno yenye kuchangia harakati za kujielimisha katika jamii ni kama ifuatavyo:

1. Kushajiisha na kuwaelekeza watu katika kujielimisha kutokana na njia za matangazo, na kwa kupitia maulamaa wa kidini na makhatibu wa mimbari na waalimu wa madrasa, na kutoka katika kila chenye kuathiri na chenye nguvu.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 63 8/27/2015 2:17:28 PM

2. Kuandaa mazingira na kutoa fursa ya shughuli mbalimbali za kujielimisha, kutoka katika vyombo rasmi vinavyohusika kama vile Wizara ya Utamaduni na Matangazo na Kuwalea Vijana, na Wizara ya Malezi na Mafunzo, kutoka katika upande wa wananchi wenye kujishughulisha na elimu. Kila sehemu kunapatikana vilabu vya michezo na kumeandikwa katika kibao kwamba ni klabu ya michezo ya kijamii na kiutamaduni. Na shughuli za utamaduni katika vilabu ni katika haki za vijana, lakini kinachotakiwa katika idara za vilabu ni kutoa kipaumbele kikubwa katika upande wa maarifa na elimu. Kama ambavyo misikiti na Husainiya inawezekana kuwa na dauru kubwa katika kukuza harakati za maarifa ndani ya udhibiti na kanuni za kisharia.
3. Kurahisisha harakati za kitabu kwa kutunga, kuchapisha na kusambaza, na kuwepo kwa maktaba kuu kwa ajili ya kujisomea na kutafiti inazingatiwa kuwa ni alama kati ya alama za uwepo wa harakati za kukuza maarifa katika jamii. Inapasa kutilia umuhimu suala la kuwa na maktaba kuu na kulitazama kwa jicho la pekee.

**Uwezo na nguvu:**

Katika jamii yetu kunapatikana uwezo na nguvu mbalimbali zinazosaidia katika kuanza harakati za kukuza maarifa.

**Kwanza**: Kuongezeka kiwango cha elimu, Alhamdulillahi kiwango cha kutokujua kusoma kimepungua katika nchi yetu hadi kiwango cha chini, watoto wetu wote wa kiume na wa kike wanasoma.

**Pili:** Kuenea kwa njia za mawasiliano na taarifa ya sayansi na teknolojia, miongoni mwa runinga, satalaiti, kompyuta, faksi na tovuti.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 64 8/27/2015 2:17:28 PM

**Tatu:** Historia pana ya kielimu na kiutamaduni iliyopo katika jamii yetu, tangu zamani tulikuwa na Seminari, maulamaa wakubwa, wanafasihi mashuhuri, na harakati za elimu za fasihi zinazozungumzia rejea za kihistoria na kwa mkazo mkubwa.

**Nne:** Uwepo wa vipaji na uwezo wa kielimu na fasihi katika nyanja mbalimbali, hivi sasa tuna vizazi vipya miongoni mwa wanafunzi wa elimu ya dini na miongoni mwao kuna waliopata daraja ya juu na wamekata masafa mazuri ya kielimu, na tuna makhatibu ambao ni fahari kwa kiwango cha khutuba zao, na wanafasihi mahiri na vipaji vya ubobezi katika zaidi ya nyanja moja ya kielimu kama vile tiba na uhandisi.

**Tano:** Uwepo wa uwezo wa kimali, harakati za elimu na maarifa zinahitaji mali na utoaji. Na tunao matajiri wenye uwezo, na wafanyakazi wenye uwezo na tunaona kuna mwelekeo katika kazi za kheri katika nchi yetu kama vile kujenga misikiti, Husainiya na kuwasaidia mafakiri na wanyonge. Na ambacho tunakihitaji sasa ni kueleza juu ya umuhimu wa kutoa na kujitolea katika shughuli za kuelimisha na kukuza uelewa na maarifa, na kwamba hiyo ni sehemu ya kupata thawabu za Mwenyezi Mungu Mtukufu na radhi Zake, na ni sababu ya kutengeneza jamii na kuiendeleza.

Kama ambavyo haki za kisharia miongoni mwa Khumsi, Zaka na Wakfu, nazo zinapatikana katika jamii, inapasa kufanya wajibu mkubwa zaidi katika kusaidia shughuli za kuelimisha na kushughulika na harakati za uelewa na maarifa. Nguvu hizi zinaweza kutengeneza mazingira yanayofaa ya mwamko wa utamaduni wenye utambuzi, utakaonyanyua kiwango cha jamii, na kuendeleza maisha yake katika nyanja mbalimbali na kuiwezesha kuchangia katika ujenzi wa nchi na kunyanyua hadhi yake.

# USTAWI WA MAARIFA NA UTOAJI WA WANANCHI

Kitendo cha ripoti ya ustawi wa mwanadamu Mwarabu ya mwaka 2002 kuchagua maudhui ya kujenga jamii yenye maarifa ilikuwa ni jambo mwafaka sana. Hiyo ni kwa sababu mwanzoni mwa karne ya ishirini na moja, kitendo cha kuwa na maarifa kwa ajili ya kuchuma, kuzalisha na kufanya kazi, kimekuwa ni nyenzo inayotoa dhamana ya kupatikana ustawi wa mwanadamu katika medani zake zote, kwani mara nyingi maarifa ndio huweka mpaka baina ya kuweza na kushindwa, baina ya uimara na udhaifu, baina ya afya na maradhi, na baina ya utajiri na ufakiri.

Na ripoti imeashiria kwamba upungufu wa maarifa na uvivu wa kutoyaboresha kwake ni mambo yaliyotawala katika nchi ambazo zinakabiliwa na udhaifu wa nguvu ya uzalishaji na uchache wa fursa za ustawi, hadi kwamba pengo la maarifa limekuwa linahesabiwa katika mtazamo wa asasi za kiuchumi za kimataifa kama vile Benki ya Dunia, kuwa ndio kigezo cha msingi wa utajiri wa nchi katika ulimwengu hivi sasa.

Hakika kurudi nyuma sana kwa jamii zetu za Kiarabu na za Kiislamu katika nyanja za maarifa na ujuzi ndiko kunakoimarisha hali ya kutoendelea kwake katika nyanja zote kama ilivyo. Na ustaarabu wa Kiislamu ulianza kwa amri ya kutafuta maarifa "soma". Na kadiri lilivyoitikiwa jambo hili ndivyo faida na mafanikio ya kimaendeleo yalivyopatikana. Na lilipopungua suala la kujali elimu na maarifa na kikateremka kiwango cha kuitikia amri ya "soma" ndipo maendeleo yakarudi nyuma na uzalishaji ukapotea na umma ukarudi nyuma na ukatanguliwa na mataifa mengine ambayo yamefuata njia ya



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 66 8/27/2015 2:17:28 PM

maarifa na elimu. – Na hiyo ndio kanuni ya Mwenyezi Mungu ambayo inahukumu, kwamba wenye elimu na maarifa watakuwa juu ya wajinga:

قُلْ هَلْ يَسْتَوِي ٱلَّذِينَ يَعْلَمُونَ وَٱلَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ۗ إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُو۟لُوا۟ ٱلْأَلْبَٰبِ ﴿٩﴾

**"Sema je, wanalingana sawa wale ambao wanajua na wale ambao hawajui. Hakika wanaokumbuka ni wenye akili tu?" (Sura Zumar : 9).**

فَلَن تَجِدَ لِسُنَّتِ ٱللَّهِ تَبْدِيلًا ۖ وَلَن تَجِدَ لِسُنَّتِ ٱللَّهِ تَحْوِيلًا ﴿٤٣﴾

**"Hutapata mabadiliko katika desturi ya Mwenyezi Mungu wala hutapata mageuzi katika desturi ya Mwenyezi Mungu."**
**(Surat Fatir: 43)**.

Na haiwezekani kuvunja tofauti wala kukata masafa makubwa ambayo yanatenganisha baina ya jamii zilizoendelea isipokuwa kwa kujenga jamii yenye maarifa, na kumiliki uwezo wa kielimu na kurekebisha upungufu wa elimu na ujuzi.

Hakika ushahidi wa kushindwa na uwepo wa udhaifu katika hali yetu ya kimaarifa, kiujuzi na kielimu, ni mwingi sana hauhesabiki wala hauna idadi. Na katika nyanja mbalimbali, ripoti iliyotajwa imeashiria baadhi ya ushahidi huo: Ambapo idadi ya magazeti katika nchi za Kiarabu ni chini ya magazeti 53 kwa kila watu elfu moja, ukilinganisha na magazeti 285 kwa kila watu elfu moja katika nchi zilizoendelea. Na vinapatikana vikokotozi chini ya 18 kwa kila watu elfu moja katika nchi za Kiarabu, ukilinganisha na



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 67 8/27/2015 2:17:28 PM

wastani wa kiulimwengu nao ni 78.3 ya vikokotozi kwa kila watu elfu moja.

Ama uzalishaji wa vitabu katika nchi za Kiarabu hauvuki asilimia 1.1 katika uzalishaji wa kiulimwengu ingawa Waarabu ni asilimia 5 ya wakazi wa ulimwengu. Na pamoja na uwepo wa milioni 284 ya Waarabu wanaozungumza lugha ya Kiarabu katika nchi 22, lakini idadi ya kawaida iliyozoeleka katika kusambaza riwaya au mkusanyiko wa visa vifupi ni baina ya nakala 1000 na 3000, na kitabu ambacho nakala zake 5000 zimeweza kusambazwa kinaonekana kuwa ni chenye kufaulu na kupata mafanikio makubwa.

Wakati ambapo idadi ya usambazaji wa kielimu huko Ufaransa unafikia 840 ya utafiti katika kila watu milioni moja, na Uholanzi ni 1252, na Uswizi ni 1878. Hakika katika nchi za Kiarabu haivuki tafiti 26 katika kila watu milioni hadi mwaka 1995. Na utafiti wa kielimu katika nchi za kiarabu unakabiliwa na upungufu wa uchangiaji wa fedha, ambapo uchangiaji rasmi hauvuki asilimia 0.2 katika uzalishaji wa taifa, na idadi hii inatofautiana kutoka nchi hadi nchi nyingine, na wengi wao wanatumia kiasi hicho cha fedha katika kulipa mishahara ya wafanyakazi. Na kwa kulinganisha tunakuta uchangiaji wa fedha katika shughuli za utafiti na maendeleo katika nchi zilizoendelea ni baina ya asilimia 2.5 hadi asilimia 5.

Na tarjuma inazingatiwa kuwa ni miongoni mwa nguvu muhimu ya kusambaza maarifa na kuwasiliana na ulimwengu, isipokuwa harakati za tarjuma katika nchi za Kiarabu bado zingali zinasifika kwa kudumaa na vurugu, kwani wastani wa vitabu vilivyotarjumiwa katika kila milioni moja ya wakazi katika nchi za Kiarabu katika miaka hii mitano ni vitabu 4.4, yaani ni chini ya kitabu kimoja kwa mwaka kwa kila wakazi milioni moja, wakati ambapo idadi imefikia vitabu 519 Hungury na vitabu 920 Hispania kwa kila watu milioni moja.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 68 8/27/2015 2:17:28 PM

Pamoja na ongezeko la idadi ya vitabu vilivyotarjumiwa katika ulimwengu wa Kiarabu hadi kufikia takriban maudhui 175 kila mwaka kuanzia mwaka 1970 -1975 kwa kiasi kinachokaribia vitabu 230, bado ni sawa na moja ya tano ya vitabu vinavyotarjumiwa katika nchi ya Ugiriki.

Na inakadiriwa kwamba jumla ya mrundikano wa vitabu vilivyotarjumiwa tangu zama za Maamun hadi leo ni vitabu 100,000 takriban, nayo ni sawa na idadi ya vitabu vilivyotarjumiwa Hispania katika kipindi cha mwaka mmoja.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 69 8/27/2015 2:17:28 PM

# JUKUMU LA MWAMKO

Serikali za Kiarabu zinabeba sehemu kubwa zaidi na ya kimsingi katika jukumu la ubaya na udhaifu katika hali ya maarifa na elimu katika nchi za kiarabu, kwa ubakhili wake wa kutowekeza na kutoa fedha katika nyanja hii, na kwa uendeshaji na mipango mibaya, na kwa kuweka kwake vikwazo na vizingiti katika uhuru wa kifikira na harakati za maarifa.

Na kama mfano wa kutokujali na kupuuzia rasmi jambo la maarifa na elimu tunaashiria katika yale aliyoyasema Dr. Shakir Mustafa mwanafikra na mwanahistoria wa Syria ambaye alikuwa anaongoza 'Jumuiya ya Kiarabu ya Malezi, Utamaduni na Maarifa' katika Umoja wa nchi za Kiarabu, amesema:

"Hakika jumuiya ilionelea kwamba iweke mkakati wa utamaduni wa Kiarabu mwaka 1982, ili kuweka siasa ya utamaduni ya mustakabali, na ilichagua wasomi 17 waliobobea kutoka katika nchi 17 za Kiarabu ili kuweka mkakati huu, ambao uliendelea kufanya kazi kwa muda wa miaka 4, na zimetumika dola milioni moja, na tulifanya mikutano 29 iliyokusanya wabobezi 25 katika matawi ya maarifa ya kibinadamu kuanzia muziki hadi afya, dini hadi elimu, na nilifanya mimi mwenyewe muhtasari wa mkusanyiko wote huu katika mijaladi mitano ambayo iko katika kabati hadi leo! Na nilikabiliwa na machungu katika kazi hii kubwa, sio kwa sababu ya juhudi niliyotoa lakini ni kwa sababu ya ukaidi wa serikali za Kiarabu, ambapo hazikutupa taarifa au takwimu rasmi, na nilikuwa nalazimika kutuma mjumbe wangu binafsi kwenye serikali hizi na kazi yake inashindikana. Nikalazimika kusafiri mimi binafsi katika zaidi ya mara moja na nilikabiliwa na idadi kadhaa ya muamala mbaya na vikwazo na ukiritimba unaotosha kukwamisha kazi yetu



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 70 8/27/2015 2:17:28 PM

kabisa. Kisha waliafiki mawaziri wa utamaduni wa Kiarabu kwa ujumla katika mkakati huu pamoja na kwamba wao hawakuusoma na hivyo hajausoma hata kiongozi mmoja wa Kiarabu hadi hivi sasa."[29]

Lakini wajibu haukomei serikalini tu. Hakika kukuza mwamko katika kiwango cha utamaduni na maarifa kunahitaji harakati za kiraia na harakati za kijamii na hususani kutoka kwa Maulamaa na wasomi, na kutoka katika upande wa wafanyakazi na mali.

Katika nchi zilizoendelea sekta za uzalishaji na huduma zinachangia, na matajiri na taasisi za kijamii za kiraia zinachangia asilimia 50 katika shughuli na juhudi za utafiti na uendelezaji wa kielimu na maarifa, wakati ambapo idadi hii ya asilimia 3 katika ubobezi haivuki katika utafiti wa maendeleo katika nchi za Kiarabu.

Na mwanzoni mwa Januari mnamo mwaka 1997 gazeti la Kristian Syines Munitor la kimarekani liliandika: "Hakika mmarekani ambaye hakupenda kutangaza jina lake alijitolea dola milioni 35 ili kulinda utamaduni, usafi na mila nzuri katika nchi yake na akatuma msaada kwenye Chuo cha Maarifa ya Jamii, ambacho kilianzishwa katika jimbo la Masachusters, na kuzatiti juhudi zake katika kupambana na upotoshaji na mmomonyoko wa maadili na tabia inayopatikana katika jamii ya Kimarekani. Na mwanaume alikuta kwamba ujumbe wa chuo unatimiza ndoto yake aliyokuwa anaitamani kwa taifa lake hivyo akaweka chini ya uangalizi wake kiasi hicho kikubwa."[30]

Na kisha mfano mwingine aliueleza Dr. Muhammad Abdu Salaam, mtaalamu wa fizikia wa Kipakistani ambaye ni Mwislamu wa kwanza kupata tuzo ya Nobeli mwaka 1979. Imeandikwa katika kitabu chake *Ahlaamu Wahaqaiq* kuwa aliendelea kuwa ni mtu

[29] *Jaridatul-Hayati* linatolewa London toleo la 11656, la tarehe 18 Januari 1995

[30] Fahamiy Huweidy katika *Athiryai Hadha Zamaan al- Ab'adun*, Jarida la as-Shariq al-Qatwariyah la tarehe 7 Januari 1997.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 71 8/27/2015 2:17:28 PM

mwenye ndoto ya kuanzisha kituo cha fizikia cha kinadharia ili wafaidike kwacho na wajifunze humo wataalamu wa ulimwengu wa tatu, na hakupata sehemu inayoitikia ndoto yake isipokuwa mji wa Tarster wa Kitaliano, na alishangazwa kwamba baraza la mji lilitenga kiasi cha dola milioni 40 kwa ajili ya mradi, na kwamba matajiri wake walijitolea kumshajiisha na kumpa mali ambazo anazihitajia.

Dr. Abdus-Salaamu alipokea kisa cha msaada wa dola milioni 70 zilizotolewa na taasisi ya Kiki, ambayo ilianzishwa na familia tajiri ya Kimarekani inayofanya kazi ya mafuta katika Chuo cha Teknolojia cha Calfonia, ili aweze kujenga darubini kubwa katika ardhi, masafa yake yanafikia mita kumi. Baada ya hapo akajiuliza kwa kusema: Wako wapi matajiri katika nchi zetu? Na kwa nini wanazembea katika kufanya kazi hizi nzuri ambazo wanazifanya matajiri katika nchi nyingine katika ulimwengu?[31]

Moyo huu ulikuwa unapatikana ndani ya matajiri wa umma katika zama zilizopita, na kwa moyo huo umma uliweza kutimiza yale ambayo historia inayazungumzia miongoni mwa mafanikio ya kielimu na maendeleo ya kibinadamu. Sunna ya Wakfu wa kheri ilikuwa inatumika katika jamii mbalimbali za umma, na kwayo kulianzishwa madrasa, hospitali, maktaba na nyumba za wageni, na kupitia hiyo kulikuwa kunapatikana masurufu na kuhudumia shughuli za kielimu na kiutamaduni.

Imekuja katika maelezo ya Sharifu al-Muratadha Ali bin al-Husain al-Musawiy (aliyezaliwa mwaka 355 na kufariki mwaka 436 Hijiria) kwamba yeye alitoa Wakfu kijiji kizima kwa ajili ya kilimo, mapato yake yatumike kwa ajili ya karatasi za Maulamaa na wanafunzi.[32]

---

[31] Rejea iliyotangulia.
[32] *Diwanu Sharifu al-Murtadhaa* katika utangulizi wa maelezo yake, Uk. 50 – 51.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 72 8/27/2015 2:17:29 PM

Na katika zama za hivi karibuni huko Misri Fatma binti al-Khadawiy Ismail alitoa msaada katika mradi wa kuanzisha chuo kikuu cha Misri, shamba la ukubwa wa ekari 3,300 na pato lake kuwa ni mahususi kwa ajili ya chuo kikuu, ukiachilia mbali kipande cha ardhi ambacho kina ukubwa wa ekari sita kwa ajili ya kujenga makao makuu ya chuo kikuu cha Cairo hivi sasa, na akatoa zaidi ya hayo paundi 18 elfu kwa ajili ya bajeti ya chuo kikuu katika mwaka wa 1913. Kama ambavyo Amir Yusufu Kamal alitoa Wakfu kwa chuo kikuu ekari 125 na akaanzisha kutokana na mali yake kitivo cha sanaa mwanzo wa karne ya ishirini, na akatuma jopo la wahitimu wake wa mwanzo kwenda Italia na Ufaransa kwa fedha zake binafsi, kama ambavyo Mustafa Kaamil al-Ghamariy alitoa Wakfu wa mashamba yenye utajiri kutoka katika Bani Suwaif ekari 500 kwa chuo kikuu cha Misri.[33]

**Kujitolea Katika Jambo la Umma:**

Haiwezekani kupinga uwepo wa kujitolea kuzuri na uwepo wa watu wema katika jamii zetu kutoka kwa baadhi ya watu wema wenye kutoa mali zao na utajiri wao katika njia ya Mwenyezi Mungu na kutumikia maslahi ya umma. Lakini kujitolea huku bado kungali ni kuchache sana hakulingani na ukubwa wa pato na upana wa tabaka la matajiri. Jarida la *Arabian Business* limezungumzia mwishoni juu ya matajiri hamsini wanaomiliki dola bilioni 404, na likasema hakika halijaelezea matrilionea wa Kiarabu mashuhuri, vinginevyo kurasa 50 zisingetosha kuelezea matajiri ambao hawadhihirishi utajiri wao kwa kuogopa husuda na kuulizwa.[34]

---

33 Fahmaiy Huwaidiy katika *Athiriyau al-Hadhwiruna al- Ghaibuna*, *Majalatul-Khairiya*, Toleo la 91 la Jumadi al- Akhira 1418 Hijiria.

34 *Shabakatu al-Maalumati al-Arabiya* (Muhiyt) kwa kunukuu kutoka Arabian bussiness. Anwani ya tovuti ni www.moheet.com



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 73 8/27/2015 2:17:29 PM

Kama ambavyo kujitolea huku hakufikii kiwango cha chini cha mahitaji na changamoto kubwa ambazo zinaukabili umma katika zama hizi; na ambazo zinaakisi athari zake katika makundi yote likiwemo la matajiri wenyewe, na kunaathiri katika hali mbalimbali za umma na mwathirika wa kwanza ni hali ya kiuchumi; ni jambo ambalo linamaanisha kwamba kujitolea katika jambo la umma kuna manufaa mazuri kwa matajiri wenyewe, na katika nyanja za kiuchumi, kama ambavyo ubakhili wa kutotoa katika kuhudumia mambo ya umma una matokeo mabaya na wao matajiri hawako mbali na athari zake.

Na cha kushangaza sana ni kuteremka kiwango cha kujitolea katika mambo ya jamii katika medani ya umma ambao dini yake inafaradhisha kutoa kama wajibu wa lazima, na nguzo ya msingi katika kujiunga na dini, ambapo Aya za Qur'ani Tukufu zinaambatanisha daima baina ya kusimamisha Swala na kutoa Zaka, na inakariri hilo katika aya 32 kama vile kauli yake (swt): **"Simamisheni Swala na toeni Zaka na shikamaneni na Mwenyezi Mungu." (Sura al-Haji: 78)**. Na baina ya imani na kutoa katika njia ya Mwenyezi Mungu kama vile kauli yake (swt): **"Wale walioamini miongoni mwenu na wakatoa, wana malipo makubwa." (Sura al-Hadid: 7)**. Kutoa katika jambo la umma kumekuwa ni hamu ya jamii katika jamii nyingine wakati ambapo katika jamii zetu bado kiwango cha kujitolea ni kidogo na kwa mtu mmoja mmoja.

Na katika makala ya Mahaa Abdul-Fataha katika jarida la *Akhibaarul-Yaumi* la Misri la tarehe 5/8/1997, aliyoiandika kutoka Washington chini ya anwani "Jambo zuri lililopo Marekani, Wakfu za Matajiri Wake na Roho ya Kujitolea," humo ameashiria kwamba inakaribia kutopatikana tajiri huko Marekani isipokuwa hutenga sehemu ya utajiri wake kwa ajili ya jamii, na amezungumzia mfano wa mwanaume mmoja kati ya matajiri wa kimarekani aliyeanzisha



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 74 8/27/2015 2:17:29 PM

taasisi mbili za kheri na akatoa kimya kimya mamia ya mamilioni ya dola kwa muda wa miaka kumi  iliyopita kwa ajili ya kazi za kheri. Na wala hakujulikana isipokuwa wakati alipouza baadhi ya makampuni yake mwishoni, na akatoa kwa ajili ya kazi za kheri dola bilioni moja, wakati ambapo hakubakisha kwa ajili ya nafsi yake na familia yake isipokuwa dola milioni tano tu.

Na imekuja katika taarifa nyingine kwamba misaada ya Kimarekani kwa ajili ya jumuiya za kheri mwaka 2003 ilifikia dola bilioni 245, na ni sawa na asilimia 2.2 ya pato la nchi.[35] Kama ambavyo wastani wa misaada kwa mwaka ni dola 500 kwa kila mmarekani.

Na imekuja katika maelezo ya Carnegie Endowment for International Peace kwamba ni taasisi ya utafiti wa kisiasa mashuhuri huko Washington, mji mkuu wa Marekani, iliyoasisiwa mwaka 1910 chini ya usimamizi wa Androw Gariygy, mmoja kati ya viongozi muhimu wa viwanda katika miongo hiyo, na ambaye alipata utajiri mkubwa katika kutengeneza chuma, kisha akaamua kujiimarisha ili kutimiza malengo ambayo alihisi kwamba taasisi rasmi haziwezi kuiachia yote serikali, na mojawapo ni kadhia ya kusambaza amani katika ulimwengu.

## Kutilia Umuhimu Mambo ya Utamaduni:

Aghlabu watu wema katika nchi zetu huelekeza utoaji wao katika mambo yanayohudumia mambo ya kidini moja kwa moja, kama vile kujenga misikiti, Husainiya, Hija, Umra, Ziara, kusoma Qur'ani na mfano wa hayo miongoni mwa shughuli za kidini. Na katika daraja la pili yanakuja mazingatio ya kutoa katika mambo ya kibinadamu, kama vile kuwasaidia mafakiri, kulea mayatima na kutibu wag-

[35] Jarida la *al-Wasat* katika kiambatanisho cha wiki cha jarida la *al-Hayaati*, Toleo la 649 la tarehe 5, July 2004.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 75 8/27/2015 2:17:29 PM

onjwa. Na katika daraja la tatu inakuja zamu ya kutoa katika mambo ya kuelimisha na maarifa, kama vile kujenga shule na vyuo vikuu, kuanzisha vituo vya elimu, kuanzisha maktaba, kusambaza utafiti, makala na vitabu, na kuendeleza vipaji na uwezo.

Na ikiwa kiwango cha utoaji cha wananchi ni kidogo, na ikawa jambo la kuelimisha liko katika daraja la mwisho, hakika hilo linamaanisha kwamba bado itaendelea kuwepo na kudumu hali ya kutoendelea na kutostawi katika nyanja hii. Hivyo kwa kasi hii ya maendeleo ya kimaarifa na kiteknolojia iliyopo katika jamii nyingine ni namna gani utakuwa mustakabali wa umma huu? Ni lazima kuamsha azma na kuelekeza nguvu katika kujitolea na kutoa katika mambo ya kielimu, kwani maarifa sio mas'ala ya pembezoni katika mtazamo wa Kiislam, bali ni katika asili ya dini. Na kutoa katika kusambaza maarifa na elimu ambayo umuhimu wake na fadhila zake si mdogo mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kuliko kutoa na kujenga misikiti na mambo ya ibada. Na ni kwa maarifa ndipo hali ya kidini inapata nguvu. Kama ambavyo kunyanyua kiwango cha maarifa ni njia bora ya kukabiliana na hali ya ufakiri na uduni wa kiuchumi.

## Al-Babatin ni Mfano wa Kuigwa:

Hakika katika mambo yanayosukuma na kushajiisha suala la kujali na kutilia umuhimu kutoa katika mambo ya maarifa na ya kustawisha ujuzi na elimu, ni kule kuwatangaza na kuwataja vizuri wale wenye kujitolea katika nyanja hii. Kuwaheshimu na kuwathamini wenye kujitolea, ambao wanajali na kusaidia shughuli za kimaarifa za kiutamaduni. Na wao kwa hakika wanastahiki kila heshima na kuthaminiwa, kwa sababu kujali kwao nyanja hii kunaonyesha kiwango chao cha juu cha utambuzi na kuhisi kwa kina juu ya majukumu.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 76 8/27/2015 2:17:29 PM

Na miongoni mwa wale wanaojitolea wanaoongoza katika eneo letu la Ghuba ni Ustadhi Abdul-Aziz bin Suud al-Babatin, Mwenyezi Mungu amhifadhi. Naye ni kati ya wafanyabiashara maarufu wa Kuwait (amezaliwa mwaka 1936) na anashughuli za kibiashara na viwanda zenye kuonekana. Naye ni mwanafasihi mshairi, ametoa diwani yake ya kwanza kwa jina la *Buhul-Bawaadiy*, mwaka 1995 na diwani yake ya pili kwa jina la *Musafiru fiyl-Qifaari*, mwaka 2004. Na kwa kujali kwake maarifa amejiunga na kuwa mjumbe katika taasisi za kielimu na utamaduni miongoni mwazo ni: *al-Haiatu at-Taasisiyat Lilujinati al- Wataniayat Lida'ami at-Ta'alimi*, na *Idarat Sunduqi al-Waqifiy Lilithaqafati wal-Fikri al-Tabiati Liliamanati al-A'mati Liliauqafi fiy Daulati al-Kuwait*, na *Rabitatu al-Udabaai fiyl-Kuwait*, *Majlisi Umanaail-Majimai Thaqafiy al-Arabiy fiy Beirut*, na *Jumu'iyatu Faasi Saayis al-Thaqafiyati fiyl-Magharib*, na Majilisi Umanaai (*Muasasatu al-Fikri al-Arabiy*), naye ni mjumbe mwakilishi wa *Majimau al-Lughati al-Arabiyati Dimishq*. Na hakuna shaka kwamba ujumbe wake katika taasisi hizi unamaanisha kuendelea kwake kusaidia pamoja na kujali maarifa na utamaduni na kutoa kwake juhudi, wakati na mali kwa namna yenye kuendelea katika kuzihudumia jamii.

Na alianzisha tuzo ya kila mwaka ya umahiri wa ushairi mnamo mwaka 1989, na ofisi yake kuu ipo Cairo, na zimefunguliwa ofisi za kimaeneo huko Tunisia, Oman na Kuwait. Kama ambavyo ameanzisha tuzo ya kila mwaka maalumu kwa ajili ya wajukuu wa Imamu al-Bukhariy yenye thamani ya dola 100,000 kwa ajili ya kukarabati madaraja ya utamaduni ya asili baina ya Umma wa Kiarabu na nchi za Kiislamu zilizojikomboa karibuni katika bara Asia.

Na ameanzisha utafiti wa kielimu ambapo wanapewa wananchi wa nchi za Kiislamu katika jamhuri za Asia ya kati nafasi mia moja



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 77 8/27/2015 2:17:29 PM

kila mwaka za masomo katika chuo kikuu cha Azhari Cairo, achilia mbali nafasi tano kila mwaka wanazopewa watu wa Morocco, na nyingine katika Niger na nyingine watu wa Uganda na Mali, na nafasi mia kila mwaka kwa ajili ya wananchi wa Iraki kwa kushirikiana na Samahatu Sayid Muhammad Baaqir al-Hakim kabla ya kufa kwake shahidi رحمه الله, na nafasi hamsini kila mwaka za masomo ya juu kwa watoto wa mashihidi wa intifadha ya Aqsa  (Palestina).

Na ameanzisha maktaba kubwa ya ushairi wa Kiarabu huko Kuwait, na Maktaba katika kitivo cha fasihi katika chuo kikuu cha Qudsi, inatoa huduma zake kwa watoto wa Palestina. Na ameanzisha tuzo ya ushairi wa Kiarabu huko Palestina kwa kuelekeza kwa vijana wa Kipalestina wenye umri wa chini ya miaka 35. Na aliasisi kituo cha tarjama huko Beirut mwaka 2004 ili kila mwaka kitarjumu makumi ya vitabu vya elimu na vinginevyo kutoka katika lugha za kigeni kwenda kwenye lugha ya Kiarabu. Kama ambavyo alianzisha madrasa nyingi na vyuo huko Misri mwaka 1990, na Lebanon mwaka 1996, na Moroco na Iraki mwaka 1988, na jamhuri ya Kyrgyzstan na Jamhuri ya Mali, na Kazakhstan na Azerbaijan, Aljeria na India. Ukiongezea mchango wake na huduma yake katika nyanja za kibinadamu kama vile kuanzisha hospitali na vituo vya tiba na kujenga misikiti.

**Wakfu za Kukuza na Kustawisha Maarifa:**

Ili wapatikane watu thabiti wa kusaidia na kustawisha maarifa, na ili kuimarisha mchango wa wananchi katika kuhudumia mambo ya maarifa, ni lazima kuwashajiisha watu kujitolea Wakfu iliyo mahususi kwa ajili ya ustawishaji wa maarifa na elimu. Kama ambavyo tunazo Wakfu za misikiti na Husainiya kwa ajili ya kudumisha ukumbusho wa viongozi wa kidini, na vilevile baadhi ya Wakfu kwa ajili ya mafakiri, masikini na mayatima, tunahitaji pia Wakfu kwa ajili ya



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 78 8/27/2015 2:17:29 PM

masomo ya juu, utafiti na maendeleo, kutunga na kuchapisha vitabu, kwa ajili ya matangazo na vituo vya runinga vyenye malengo.

Na kabla ya hayo ni wajibu kufikiria katika kufaidika na Wakfu zilizopo kwa ajili ya maslahi ya ustawishaji wa maarifa. Wakfu ambazo ni za misikiti je haiwezekani kunufaika kwazo kwa ajili ya kusomesha maimamu wa misikiti ili kuboresha vipaji vyao? Na kwa ajili ya kuendesha masomo na semina za mafunzo na kuelimisha katika misikiti? Na kwa ajili ya kusaidia shughuli za maarifa yanayohusiana na misikiti kama vile sehemu ya tovuti na machapisho yaliyopangiliwa?

Vilevile Wakfu za Husainiya je, haiwezekani kunufaika kwazo katika kuendesha shughuli za maarifa yanayohusiana na Husainiya, shughuli zinazoafikiana na malengo yake? Na tunapokuwa na Wakfu kwa jina la Imam miongoni mwa Maimamu عليه السلام je, haisihi kwetu kutumia sehemu ya pato lake kwa ajili ya kusaidia masomo ya kielimu kuhusuiana na maisha ya huyo Imamu? Au kuanzisha taasisi za kiutamaduni kwa ajili ya kufundisha sira yake na kutoa maarifa yake na elimu yake?

Ni Wakfu ngapi zipo kwa jina la Imamu al-Husaini عليه السلام lakini hadi hivi sasa hakujaanzishwa chuo au kituo cha kufundisha maisha yake na mapinduzi yake kutokana na Wakfu hizo. Alijitolea mtafiti Sheikh Muhammad as-Sadiq al- Karabasiy kuanzisha kituo kwa ajili ya mafunzo ya Husainiya huko London, na akaweka mikakati ya kutoa Ensiklopidia yenye anwani *Dairatul- Maarifi al- Husainiya* yenye mamia ya juzuu, na imeshachapishwa baadhi yake takriban juzuu arobaini, lakini kituo hiki hakipati hata msaada mdogo unaotakiwa kwa ajili ya kurahisisha kazi yake!

Kwa nini yanazingirwa manufaa ya Wakfu hizi ndani ya njia na ada zilizozoeleka tu, kama vile kujenga misikiti, Husainiya, kuendesha



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 79 8/27/2015 2:17:29 PM

majilisi katika minasaba na kutoa chakula kwa anwani yake? Na ikiwa kuna tahadhari ya kutaka kujua ni kwa wigo gani Wakfu hizi zinaweza kujumuisha shughuli za kimaarifa na kiutamaduni, hakika Marjaa wa kidini na mafaqihi watukufu wanaweza kutunufaisha katika kutatua matatizo haya kwa kubainisha wigo wa Wakfu na mipaka yake au idhini katika kutumia kiasi kinachozidi haja kutoka upande mahususi wa Wakfu, ili kitumike katika kusaidia miradi mingine. Imepatia ripoti ya ustawi wa binadamu mwarabu ya mwaka 2003, ilipoashiria katika muhtasari wake kwamba maarifa yanakaribia kuwa ni faradhi isiyopatikana katika umma wa kiarabu hivi sasa.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 80 8/27/2015 2:17:29 PM

# MAGEUZI YA KIJAMII NA KIPENGELE CHA WAKATI

Mageuzi ya kijamii ni jukumu miongoni mwa majukumu magumu. Ikiwa jamii inaelekea katika mwelekeo maalumu au inatawaliwa na fikra fulani, hakika kubadilisha fikira hizi na tabia hii ya kijamii sio jambo rahisi, na hiyo ni kwa sababu mbili:

**Sababu ya kwanza**: Kupita muda kunasababisha kujikita katika fikra, ada, mila na mieleko, na kubadilisha kitu kilichoota mizizi sio jambo rahisi. Na mfano wake ni kama yule anayetaka kung'oa mmea wenye mizizi mirefu ardhini. Hilo linahitajia misuli yenye nguvu.

**Sababu ya pili**: Kuwepo nguvu inayonufaika na iliyo na maslahi katika hali iliyopo katika jamii, na inaogopa itakapobadilika hali hii nguvu husika itakosa maslahi. Na kwa hiyo hakika nguvu hizi zinazofaidika na hali iliyopo katika jamii zitapambana na kukhalifu harakati yoyote ya mabadiliko katika jamii.

Manabii na mitume wanakuja na amri kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili ya kubadilisha hali za jamii za kikafiri, kishirikina, zilizopotoka au zile ambazo zinaishi katika ufisadi au dhulma. Na kwa kawaida halikutimia lengo la Nabii kwa haraka, na inawezekana lisitimie lengo hilo muda wote wa maisha yake. Mwenyezi Mungu Mtukufu alituma Manabii 124,000, lakini ni wangapi kati yao waliweza kupata mafanikio katika daawa yao katika kipindi cha maisha yao?

Na Qur'ani tukufu inatusimulia kuhusu Nabii wa Mwenyezi Mungu Nuhu عليه السلام, inasema: **"Na tulishamtuma Nuhu kwa watu wake akakaa kwao miaka elfu moja ila hamsini." (Sura Ankabuti: 14)**. Pamoja na urefu wa muda huu aliokaa na watu wake



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 81 8/27/2015 2:17:29 PM

lakini Qur'ani Tukufu inatusimulia hatima ya daawa ya Nabii huyu mtukufu, inasema: **"Na hawakuamini pamoja naye isipokuwa wachache." (Sura al- Hud: 40)**. Na vilevile Nabii wa Mwenyezi Mungu Musa عليه السلام baada ya kumshinda Firauni na kuwaokoa Bani Israili kutoka kwa Firauni, aliudhiwa na watu wake maudhi makubwa na hii ndio hali ya manabii wote.

Na Nabii wetu Mtukufu Muhammad صلى الله عليه وآله وسلم aliishi miaka kumi na tatu Makkah baada ya utume, akipambana na kukabiliana na machungu ya washirikina, pamoja na kwamba walikuwa wanamwita 'Mkweli na Mwaminifu.' Na baada ya kufariki ami yake Abutalib hakuwa na mtu wa kumsaidia Makkah, licha ya muda mrefu alioishi Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم baina yao, hivyo alikwenda Twaifu ili apate mtu wa kumhami kutoka kwa wakuu wake na huko pia hakupata mtu wa kumhami. Na historia inanukuu kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم alitoka Twaif na akakaa chini ya kivuli cha mti na akamwelekea Mwenyezi Mungu Mtukufu akisema: "Ewe Mwenyezi Mungu nashitakia Kwako udhaifu wa nguvu yangu, na uchache wa hila zangu na unyonge wangu kwa watu."

Na hii ni hali ya kawaida inayopitia daawa kwenda kwenye mabadiliko kutoka katika hali ya kijamii, na kwa ajili hiyo Mwenyezi Mungu alimwambia Nabii Wake Muhammad صلى الله عليه وآله وسلم kwa kauli yake: **"Subiri kama walivyosubiri Ulul-Azmi miongoni mwa Mitume na wala usiwe na haraka kwao." (Sura al-Ahqaaf: 35)**.

Raghibu al-Isfahaaniy amesema: "al-Azmi ni kuufunga moyo ili kupata yanayotakiwa. Na Ulul-Azmi katika Mitume wapo watano: Nabii Nuhu عليه السلام, Nabii Ibrahim عليه السلام, Nabii Musa عليه السلام, Nabii Isa عليه السلام na Nabii wetu Mtukufu Muhammad صلى الله عليه وآله وسلم, Mwenyezi Mungu anamwamuru Nabii wake kusubiri kama walivyosubiri Ulul-Azmi kabla yake kisha anasema (swt): **"Wala usiwafanyie haraka."** Mageuzi ya kijamii yanahitaji subira ya muda mrefu.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 82 8/27/2015 2:17:29 PM

Kuna mambo matatu anayahitajia anayetaka kuleta mageuzi ya kijamii:

**Kwanza**: Mtazamo ulio wazi, na hili linaambatana na upande wa kifikra kwa anayetaka kuleta mageuzi, ambapo inapasa lengo liwe wazi na dhahiri.

**Pili**: Nia thabiti, hii inaambatana na upande wa kinafsi kwa anayetaka kuleta mageuzi.

**Tatu**: Juhudi ya muda mrefu. Katika baadhi ya kazi na majukumu mengi muda unakuwa na nafasi ya msingi katika kufanikisha mambo. Kinyume na ilivyo katika majukumu mengine ambapo juhudi ndio inakuwa jambo la msingi katika kufanikisha na si muda. Na mfano wake ni maradhi ambayo yanampata mwanadamu, baadhi yake yanaondoka kwa kutumia tu dawa uliyoandikiwa kwa muda mchache, na baadhi yake yanahitaji muda mrefu, kama vile kisukari ambacho kinaipata mifupa. Na mfano mwingine unaambatana na mas'ala ya kujifungua. Ni kazi ambayo inahitaji muda upite kwa mwanadamu ili awe ndani ya tumbo la mama yake miezi tisa na baada yake unawadia muda wa kujifungua, na hakuna njia nyingine ya kuharakisha kujifungua isipokuwa katika baadhi ya hali zisizokuwa za kawaida ambazo humo anajifungua kabla ya muda huu. Na hali ni hiyo hiyo katika makuzi ya watoto na kuwalea kwao, mas'ala haya yanahitaji muda kwa kufumbia macho juhudi zinazotolewa humo.

Mabadiliko ya kijamii vilevile yanahitaji subira ya muda mrefu, na utakuta baadhi ya nyakati watu wanahamasika kwa ajili ya mabadiliko lakini kadiri muda unavyopita mtu anapatwa na mshangao: Kwa nini fikra hii au ile haitawali katika jamii? Na kwa nini watu hawabadiliki kwa haraka? Na hii ni hali ya kawaida; kwa sababu mas'ala yanahitajia muda! Na muda unatofautiana kulingana



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 83 8/27/2015 2:17:29 PM

na mazingira ambayo inaishi jamii, na juhudi zinazotolewa katika maudhui ya mabadiliko, ikiwa juhudi ni kubwa zaidi basi muda unaweza kuwa mrefu kiasi, na kwa hiyo tunaona Manabii عليه السلام namna gani walikuwa wanavumilia na wanasubiri.

Na katika upande mwingine, hakika mas'ala ya mabadiliko hayafungamani na kwamba rai ambayo anaibeba ni sahihi au ni ya makosa, bali tabia ya mabadiliko ya kijamii inahitaji muda vinginevyo hakuna kitu chenye ukweli zaidi kuliko kile walichokuwa wanakilingania Manabii. Na vilevile uhalisia wa hali ambayo waliishi nayo Maimamu عليه السلام ambapo Maimamu kumi na moja waliishi baina ya watu katika hatua ya kwanza, na maisha ya Imamu wa kumi na mbili yamefichikana katika mazingira ya ghaibu. Na katika hatua ya kwanza ambayo muda wake ulikuwa ni miaka 250 Maimamu waliweza humo kuandaa kundi na kutengeneza njia na kuacha urithi na hazina kwa umma, lakini natija hakuweza kila Imamu kati yao kutimiza mabadiliko kikamilifu katika maisha yake. Na baadhi ya wafuasi wa Maimamu walikuwa wanakuja kwa Imamu wakiwa wameudhika kutokana na hali iliyopo na Imamu alikuwa anawatuliza na kuwaelimisha na kuwasubirisha.

Na vivyo hivyo warekebishaji katika kila zama na jamii nyingine. Jamii ya Ulaya ambayo ilikuwa inaishi chini ya ukandamizaji wa kanisa, na katika zama za udhalimu, haikubadilika hali yake na mazingira yake kwa haraka, bali hilo lilihitajia muda mrefu, cha muhimu katika jambo ni kuwepo na kazi. Subira haimaanishi kuzembea, bali inamaanisha juhudi na kazi, na kuacha nafasi kwa muda ili lengo na dhumuni litimie. Anasema Mtukufu Mtume صلى الله عليه وآله وسلم: "Alama za mwenye kusubiri ni tatu: Kwanza: Asizembee, Pili: Asikasirike, Tatu: Asilalamike kwa Mola Wake, na akilalamika kwa Mola Wake basi atakuwa ameshamuasi."[36]

---

36 *Wasa'ilu Shi'ah,* Hadithi ya 20862.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 84 8/27/2015 2:17:29 PM

Kati ya mwonekano ambao tunauona katika jamii zetu ni kwamba baadhi ya watu hawana subira kubwa katika kazi ya kijamii bali wanaishi katika hamasa, na baada ya muda wanajiengua, kwa sababu alikuwa anatarajia kwamba kwa kufanya kazi tu basi mambo na hali ya kijamii itabadilika haraka, na matokeo yakichelewa anazembea katika kazi.

Na jamii hazibadiliki kwa kile kinachoitwa katika jamii kwa istilahi ya 'Ngoma', mabadiliko ya kijamii yanahitaji subira ya muda mrefu na bila hivyo itazingatiwa kuwa kuna udhaifu wa utambuzi katika mwenendo wa mabadiliko katika jamii za kibinadamu. Tunaona umri wa harakati za kijamii katika jamii nyingine unachukua miongo na karne kadhaa, wakati ambapo wastani wa umri wa harakati katika jamii zetu aghlabu hauvuki miaka kumi.

Tabia ya maisha inahitajia subira, sawa iwe katika kiwango cha mtu binafsi au jamii, na yametaja magazeti yaliyomo katika Ensiklopedia ya Jinsia inayozungumzia takwimu za kupigiwa mfano, ambapo Ensiklopedia hii mwaka 2003 ilizungumzia juu ya mwanamke wa huko India kwamba ndiye mwanadamu aliyeandika barua nyingi zaidi katika ulimwengu kuhusu hali ya umma, ambapo katika mwaka mmoja aliandika barua 334. Na Ensiklopedia imeweka kumbukumbu kwamba mwaka 2002 mume wake katika uhai wake aliandika barua 8000 kuhusu hali ya umma. Iko wazi katika mifano hii miwili subira kubwa anayoimiliki mwanamke huyu na mume wake, wakati ambapo katika jamii zetu kuna mambo na matatizo mengi ya umma lakini tabia ya jumla kwa watu haivuki zaidi ya kulaumu na kuudhika, na unaweza kumkuta mtu mwenye kuhamasika na kuandika kuhusu tatizo fulani lakini anaacha kulifuatilia na anakosa subira ya muda mrefu.

Inapasa kwa watu ambao wanataka mabadiliko katika nyanja mbalimbali za kijamii hali hii iwe wazi mbele yao na wajipambe na



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 85 8/27/2015 2:17:29 PM

subira ya muda mrefu na wasubiri katika udhaifu wa mwitikio wa mazingira na watoe juhudi za ziada, na taufiki iko katika mamlaka ya Mwenyezi Mungu.

**Makundi ya Kijamii na Ushindani Mzuri:**

Ushindani ni hali nzuri kwa mwanadamu, nayo ni hali ambayo inamsukuma katika kuibua uwezo wake na vipaji vyake, kama ambavyo inamletea uchangamfu na maendeleo katika jamii, ambapo nguvu zake zinafanya harakati kuelekea kwenye maendeleo, na wanashindana katika kupata mafanikio.

*Tanafus*: Katika lugha ni harakati za ushindani, *Tanafasa al-Qaum fiy Kadhaa*: Wameshindana humo na wamejitolea bila yeyote kati yao kumletea madhara mwingine. Ushindani ni hali ya kawaida inayolingania kwenye kutoa juhudi katika njia ya kushabihiana na watukufu na kuwafikia."[37] Na ushindani ni hali anayoishi nayo mwanadamu baina yake na watu wengine wanaomzunguka, kama ilivyo katika jamii ya kibinadamu, hutengenezeka na kudhihiri makundi na mielekeo; ima kutokana na tofauti za kimawazo na fikra, ambapo kila kundi linakuwa na fikra na msingi ambao unalifanya litofautiane na kundi lingine, na ima ni kutokana na misimamo na maslahi, ambapo kila kundi linakuwa na maslahi binafsi ambayo yanalifanya liende mbio katika kushindana na kundi jingine ili kupata maslahi husika. Na ima kutokana na tofauti za kiukoo na za kimakundi au za kikabila au kwa kufuata baadhi ya viongozi mashuhuri. Na mielekeo hii huwa na msukumo na ushawishi wakati wa matatizo, na hususan wakati hali ya jamii inaponyanyuka, kwa sababu kutengeneza jamii humaanisha kuleta hali ya kusonga mbele katika jamii.

[37] *Al-Muujamul-Wasiyt*, Matu: Nafasa



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 86 8/27/2015 2:17:29 PM

**Wingi ni Hali Nzuri:**

Baadhi ya jamii zilizodumaa zinaweza kuangalia uwepo, kuanza na kuunda vikundi vya kijamii kwa mtazamo mbaya na kudhani kwamba jambo hili ni mgawanyiko unaopelekea kwenye mfarakano na kusambaratika, wakati ambapo mwanadamu akitazama kwa makini hakika ataona kwamba ni hali nzuri na sio mbaya, kwa sababu inazingatiwa kuwa ni aina ya maendeleo ya kijamii. Na maendeleleo yoyote ni lazima yazalishe baadhi ya ongezeko la hasi, na hapa ndipo inakuja nafasi ya nguvu yenye utambuzi katika jamii kudhibiti ongezeko hili na kuliwekea mpaka. Ama mwonekano wa uzuri wa wingi wa makundi ya kijamii unaodhihiri zaidi ni:

**1. Kutajirisha Fikra na Kuzalisha Chaguo Nyingi:**

Panapokuwa na mielekeo mingi ya kiutamaduni ya makundi katika jamii, na kila kundi kuzungumzia fikra na rai inazoziamini, hakika hiyo inatajirisha medani ya kifikra na inawasukuma watu katika kulinganisha baina ya rai hii na fikra ile. Kama ambavyo wingi wa ratiba na miradi, na kutofautiana mapendekezo baina ya vikundi kunawaweka watu mbele ya hiyari mbalimbali katika kutatua mambo yao, na fursa ya kutafiti na kupembua katika rai na hiyari pana zaidi na bora zaidi.

**2. Kuboresha Hali ya Ushindani kwa Ajili ya Kuendeleza Jamii:**

Kila kundi linapohisi uwepo wa kundi lingine linajaribu kuwa na uwanja mpana wa kuchuma na kuungwa mkono na jamii, hakika litafanya bidii na kushughulika kadiri linavyoweza kwa ajili ya kuwa na athari na nguvu zaidi na kujinoa kwa ajili ya hilo kwa nguvu na vipaji ilivyonavyo, na hii ni kwa faida ya maendeleo ya kijamii inayonufaika na huduma ambayo inatolewa na kundi hili na kundi lingine linaloshindana nalo. Na hii ni tofauti, kama jamii ingekuwa chini ya kundi moja na mwelekeo mmoja, ambapo hakutakuwa na



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 87 8/27/2015 2:17:29 PM

ushindani, kama ambavyo itaakisi ubaya hata katika kundi lenyewe kwa sababu litadumaa na halitafanya juhudi ya kujiboresha. Na kwa hiyo hakika kuwepo kundi zaidi ya moja na jamaa inayoshughulika katika mambo ya kijamii ya umma inaboresha hali ya ushindani na inaharakisha harakati za maendeleo katika jamii.

**3. Kutatua Nukta za Udhaifu:**

Ni lazima kutakuwepo katika kila upande au kundi linalofanya kazi katika mambo ya kijamii, nukta za nguvu na nukta za udhaifu. Na katika wingi wa vikundi vyenye kujishughulisha katika jamii, kunakuwa baina yake na hali ya ushindani, na ni kawaida kwamba baadhi ya vikundi hivi vitatumia nukta za udhaifu wa vikundi vingine, na kulazimika kila upande kutatua nukta za udhaifu wake na kuziba mianya na kisha kutakuwa na msukumo wa kukamilishana na mabadiliko katika kila upande miongoni mwa pande, ama ikiwa hakuna ushindani itabaki mianya na ubaya bila ya kushughulika na utatuzi wake.

**4. Kuvutia Nguvu ya Jamii:**

Kila kundi kati ya makundi litajaribu kwa kadiri ya nguvu yake kuvutia katika jamii kundi kubwa la waungaji mkono, na ni kawaida hawatoweza kuwavutia wote ndani ya kundi lake, na kwa hiyo hakika uwepo wa kundi lingine lenye wafuasi wengine katika watu kunasaidia nguvu zote za jamii kufanya kazi katika makundi yake mbalimbali, na sio baadhi ya nguvu zenye kushughulika, wakati makundi mengine yanabaki bila ya kupata wenye kuliunga mkono na kulifuata.

**Uhusiano Baina ya Makundi ya Kijamii:**

Uhusiano baina ya makundi ya kijamii unatofautiana katika tabia yake kutoka jamii moja hadi nyingine na inawezekana kuyagawa katika aina tatu nazo ni:

**1. Uhusiano wa Mizozo na Ugomvi:**

Katika baadhi ya nyakati uhusiano unaokuwa baina ya vikundi ni uhusiano wa mizozo na ugomvi, kwa aina mbalimbali za mizozo na ugomvi, na inaweza kufikia katika hali ya mapigano na vita, kama tunavyoona hayo katika baadhi ya nchi ambapo wanapigana jamaa, vyama na makundi. Na wakati mwingine mambo hayafikii katika mapigano bali kunakuwa na fitina nyingi za kijamii na kuzidisha matangazo na kuwa na maneno makali na kuwa na uhusiano mbaya.

**2. Uhusiano wa Kuwa Mbali na Kutengana:**

Na katika hali hii kila jamaa inakuwa imejitenga na nafsi yake, na kila kundi linajali mambo yake binafsi, na kila jamaa inafuatilia uhusiano wake na jamaa nyingine, siasa ya kuachana. Na sura hii huenda inakuwa na hatari ndogo zaidi kuliko sura ya kwanza, lakini mara nyingi inabadilika na kuwa ni utangulizi wa hali ya awali.

**3. Uhusiano wa Kushirikiana na Kukamilishana:**

Ambapo kunakuwa na aina ya uhusiano na kusaidiana na kutambuana baina ya makundi haya na jamaa ndani ya jamii. Makundi haya yanakamilishana katika kutatua mambo ya jamii, na kunakuwa na mfano wa kugawana majukumu, na hii ni sura ya mfano ambayo tunapasa kuifikia.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 89 8/27/2015 2:17:29 PM

## Vipi Uratibiwe Muundo wa Uhusiano Baina ya Makundi?

Hakika kupanga muundo wa uhusiano baina ya jamaa na makundi yenye kufanya kazi katika jamii yoyote, inategemea vitu viwili vya kimsingi navyo ni:

### 1. Kiwango cha Utambuzi kwa Viongozi:

Kunapokuwa na upevu na utambuzi kwa viongozi, kunakuwa na nafasi kubwa katika kuelekeza wafuasi wake na watu wake na mwenendo wa hali katika jamii hadi uhusiano baina ya makundi unakuwa ni uhusiano mzuri. Na kinyume chake ukikosekana utambuzi na upevu wa fikra na ikatawala hali ya ubinafsi, na ikatumika njia ya kuchafuana kutoka kila upande dhidi ya makundi mengine, au mbaya zaidi kuliko hayo, basi inatawala hali mbaya ya kutaka kila kundi kulifuta kundi jingine, hapa uhusiano baina ya makundi hauwi mzuri.

Na mas'ala ya upevu wa fikra na utambuzi kwa viongozi, yana uhusiano na mas'ala ya uzoefu na ujuzi katika kazi ya kijamii, ikiwa makundi bado yangali katika hali ya awali ya ukuaji na katika upya, hakika hii inaakisi katika muundo unaofuatwa katika uhusiano wao, ambapo inafikia baadhi ya nyakati kwenye hali ya mzozo, ugomvi na mgongano.

Na miongoni mwa mifano inayodhihiri zaidi katika nukta hii ni uzoefu wa Lebanoni ambapo hakika makundi ya Kilebanoni baada ya kupigana vita vya wenyewe kwa wenyewe walifikia kwenye hali ya upevu wa fikra na utambuzi wa kisiasa, iliyowaongoza kwamba utatuzi bora ni kushirikiana na kujadiliana na kuwasiliana baina yao kama jamaa, vyama na nguvu.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 90 8/27/2015 2:17:29 PM

## 2. Kiwango cha Mazingira ya Utamaduni na Siasa:

Makundi na mielekeo ni sehemu ya jamii, na makundi hayo huathiriwa na hali ya kisiasa na kiutamaduni iliyopo katika jamii. Ikiwa yanaishi katika jamii ambayo inatawaliwa na utaratibu na kanuni, uhuru wa fikra na kazi, hali hii ya kisiasa inafanya makundi hayo na jamii kuelekeza uhusiano wake katika mwelekeo wa kawaida na kikanuni na kitaratibu. Kama hali ilivyo sasa hivi katika nchi za Magharibi, kuna vikundi, vyama, harakati za kisiasa na kiutamaduni ndani ya hali ya siasa ya umma, inayoweka kanuni na kuongoza uhusiano baina ya makundi haya. Ama ikiwa hali ya kisiasa haitoi fursa ya uwepo wa makundi, wala haitambui uwepo wa nguvu za kiraia zinazofanya kazi katika jamii, na hakuna uhuru wa kazi ya kiutamaduni, kisiasa na kijamii, hii inaakisi ubaya katika hali ya kijami, na uhusiano wa makundi.

Na ikiwa unatawala katika jamii utamaduni wa usamehevu, uvumilivu na kuheshimu rai ya mwingine, hakika inasaidia katika kuelekeza uhusiano baina ya makundi. Ama ikiwa utamaduni uliotawala ni utamaduni wa kuenguana na kufutana, hususani ndani ya anwani za kidini, na haya ni kati ya mambo ambayo yameipata nyanja yetu ya kidini, tunakuta humo yupo anayeiona nafsi yake kana kwamba anamwakilisha Mwenyezi Mungu na sharia katika ardhi hii, na kisha hakika upande wowote unaokhitalifiana naye umeikhtilafiana na Mwenyezi Mungu, sharia na haki, na unastahili kila tuhuma na upotovu, uanabidaa, shiriki, uasi na kutoka katika dini. Hakika jamii ambayo inaishi katika hali ya utamaduni kama huo haiongoki katika kuratibu uhusiano baina ya makundi yake, kwa sababu makundi haya yanashindana katika matamanio mabaya kwa fikra hizi za kuenguana na za kiuadui, na kisha hakika watu wa makundi haya wanaathirika katika uhusiano wao na wengine kutokana na hali hii iliyopo.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 91 8/27/2015 2:17:29 PM

**Makundi ya Kijamii na Kuboresha Uhusiano:**

Yalidhihiri na yanadhihiri baadhi ya makundi na jamaa katika jamii yetu ya ndani, ama kwa anwani ya Umarjaa au utamaduni, na hali hii ni nzuri kijamii kwa sababu jamii iliyodumaa hayakudhihiri humo makundi, wakati ambapo jamii ambayo inashughulishwa na shughuli na harakati za kijamii na kiutamaduni, makundi yake na mielekeo yake inakuwa ni mingi.

Na jamii yetu sasa hivi inaishi katika hali hii, kuna makundi yanaona nafsi yake kwa namna mbalimbali ya kusema, na inahitajika kuboresha uhusiano wetu baina ya makundi na mielekeo mbalimbali, na kwamba kuelekea katika mwelekeo wa ushindani mzuri kwa ajili ya kuhudumia jamii kwa kutekeleza kauli yake (swt): **"Na katika hilo na washindane wenye kushindana." (Sura al-Mutafifin: 26)**. Na tunapotaka kutekeleza Aya hii katika hali yetu ya leo, inatakikana kwenda mbio ili kuwepo na ushindani mzuri katika kuhudumia jamii, ndani ya wigo wa jumuiya za kheri, vilabu vya michezo, vilabu vya utamaduni, kuhuisha minasaba ya kidini na ndani ya shughuli na kazi mbalimbali kama vile chaguzi za halimashauri, uchaguzi sehemu za biashara na nyanja nyingine zilizopo.

Na kwa kuelekeza ushindani huu katika mwelekeo mzuri ni lazima kuandaa mambo manne nayo ni:

**1. Kutambuana na Kuheshimiana:**

Hakika tatizo la jamii nyingi ni uwepo wa nguvu au kundi lililoenea, lisilotambua kuchipuka kwa makundi mapya na kukua kwa nguvu mpya, bali halioni kwamba makundi hayo mapya yana haki ya kudhihiri katika medani na kufanya shughuli humo.

Na kufanya hivyo ni ukiritimba na kasumba. Watu wote wana haki ya kufanya kazi na sio haki ya jamaa au kundi au mtu binafsi



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 92 8/27/2015 2:17:29 PM

peke yake, na hakuna mwenye haki ya kuwakataza wengine hilo.

**2. Njia za Kisharia za Ushindani:**

Ni jambo la kawaida kila kundi au kila upande kuvutia kiasi kikubwa zaidi cha watu, na uwanja mpana zaidi wa kufanya kazi, lakini ni muhimu kuwepo na njia zinazotumika kuvutia njia za kisharia, na inatakikana njia hizi kuwa mbali na mbinu za mashambulizi, kutuhumu, kutia shaka katika nia na malengo na kuwepo na kulazimiana na tabia njema.

**3. Kufunguka na Kuwasiliana:**

Kati ya yanayosikitisha ni kuwepo katika jamii makundi na jamaa wanaoshughulika, lakini kutokuwepo baina yao aina yoyote ya mawasiliano na kufunguka. Na panapokosekana mawasiliano shutuma zinakuwa nyingi baina ya kundi hili na lile, kwa sababu ya hali ya utengano. Na hususani nukta hii, mara nyingi unavurugika uhusiano baina ya makundi mbalimbali kwa sababu ya misimamo binafsi. Ambapo kila kundi lina wafuasi, na baadhi yao au mmoja wao anaweza kufanya kitendo cha kimakosa dhidi ya kundi lingine, na kitendo hiki kuchukuliwa kuwa ni kitendo cha kundi lote, na aghlabu mambo yanabadilika na kuwa ni mzozo na mgongano. Lakini kama kuna mawasiliano na kufunguka baina ya pande hizi dhana hizi zinamalizika.

**4. Kushirikiana na Kukamilishana:**

Nacho ni kiwango cha juu zaidi katika uhusiano baina ya makundi. Makundi haya na jamaa hizi zinafanya kazi katika jamii moja, hivyo inatakikana kinyanyuke kiwango cha uhusiano baina yao hadi kwenye aina ya uelewano na kukamilishana, kiasi kwamba kila upande unajaribu kufaidika na upande mwingine kwa kile kinachonyanyua kiwango cha kazi. Na kuunganisha juhudi katika kuhudumia ma-



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 93 8/27/2015 2:17:29 PM

slahi ya jamii na kuzuia hali za mgongano na mizozo yenye madhara kwa mustakabali wa jamii.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 94 8/27/2015 2:17:29 PM

# KUJITOLEA KATIKA KUHUDUMIA JAMII

Ndani ya nafsi ya mwanadamu kuna ukinzani na matamanio mengi, baadhi yake yana mwelekeo wa shari na mengi kati yake yana mwelekeo wa kheri. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَنَفْسٍ وَمَا سَوَّىٰهَا ﴿٧﴾ فَأَلْهَمَهَا فُجُورَهَا وَتَقْوَىٰهَا ﴿٨﴾

**"Na kwa nafsi na kuilinganisha kwake! Akafahamisha uovu wake na takua yake." (Sura Shamsi: 7 – 8)**.

Na utashi wowote na mwelekeo katika nafsi ya mwanadamu unahitaji kutambuliwa, kukuzwa na kuchungwa. Tunakuta baadhi ya watu vinachomoza vipaji vyao vya fani au fasihi au elimu au vinginevyo, navyo viko tayari ndani ya mwanadamu, lakini kuna anayevitambua na kuviendeleza, na kuna anayevipuuzia na kuviua. Kwa mfano, msukumo wa kuwahudumia watu na kufanya vitendo vya kheri ni jambo lililopo ndani ya nafsi ya kila mwanadamu, lakini baadhi ya watu wanagundua mvutano huu na wanaukuza na wanauitikia, na wanakuwa kama ilivyowaelezea hadithi tukufu, ni funguo za kheri. Kutoka kwa Anasi bin Maliki (r.a) amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم: "Hakika miongoni mwa watu kuna funguo za kheri na kufuli za shari, na miongoni mwa watu ni funguo za shari na ni kufuli za kheri. Mafanikio ni kwa aliyejaaliwa na Mwenyezi Mungu kuwa na funguo za kheri katika mikono yake, na maangamio ni kwa aliyejaaliwa na Mwenyezi Mungu kuwa na kufuli za shari katika mikono yake."



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 95 8/27/2015 2:17:30 PM

Na kutoka kwa Sahali bin Sa'ad (r.a), amesema: Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: "Hakika kheri hii ina hazina zake, na hazina hizo zina funguo, basi mafanikio ni kwa mja aliyejaaliwa na Mwenyezi Mungu kuwa na funguo za kheri na kufuli za shari, na maangamio ni kwa mja aliyejaaliwa na Mwenyezi Mungu kuwa na kufuli za shari."[38]

Na imekuja katika dua ya *Makaarimil-Akhilaaq* ya Imamu Zainul-Abidina عليه السلام: "Na pitisha katika mikono yangu kheri kwa ajili ya watu."[39]

**Kukuza Utashi wa Kheri:**

Mwelekeo wa kufanya kheri ni hali ya kimaumbile katika nafsi ya mwanadamu, lakini kuikuza hali hii inahitaji sababu na visababishi na miongoni mwavyo ni:

**1. Kuimarisha Mafungamano na Mwenyezi Mungu:**

Mwanadamu kila anapofungamana na Mwenyezi Mungu kwa kutarajia thawabu Zake na radhi Zake, na kuogopa adhabu Yake na mateso Yake, hilo linakuwa ni msukumo wa kufanya amali ya kheri na kuhudumia watu, ambapo anatarajia kwa hilo kupata thawabu.

**2. Utambuzi wa Kijamii:**

Kumiliki utambuzi kunamfanya mwanadamu awe na msukumo zaidi katika amali ya kheri; kwa sababu utambuzi unamuongoza mwanadamu katika kujitolea katika amali njema inayomnufaisha yeye binafsi kama ambavyo inanufaisha jamii ambayo yeye ni sehemu yake, na kisha inaakisi maendeleo ya jamii kwake na kwa watu wake.

---

[38] Muhammad Naaswir Diyn al-Albaaniy katika *Sahihi Sunan, Ibnu Maajah* Juz. 1, Chapa ya kwanza 1417 Hijiria (Riyaadh Maktabatul- Maarif), Uk. 96 Hadithi ya 195 na 196.

[39] Al-Imamu Ali bin al- Husaini عليه السلام katika *Sahifati Zainul-Abidiyn*, Dua Makaarimil-Akhilaaq, Chapa ya kwanza 1428 Hijiria (al-Qatif Atwiyaaf Nashiri Watauzi'i), Uk. 92.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 96 8/27/2015 2:17:30 PM

**3. Mazingira ya Msukumo:**

Kuna mazingira ambayo yanamsukuma mwanadamu kufanya kheri na yanashajiisha utashi huu katika nafsi yake, kama pale anapopata taufiki ya Mwenyezi Mungu ya kuandamana na watu wa kheri, ambapo hilo linakuwa ni msukumo kwake wa kuwa sawa nao na mfano wao.

4. **Ushajiishaji wa Kijamii:**

Jamii ambayo inashajiisha katika kheri wale wanaoelekea kwenye amali ya kheri wanakuwa wengi, wakati ambapo jamii ambayo inadumaa na inayoweka vikwazo dhidi ya wenye kushughulika katika amali ya kheri, humo zinapungua harakati za kheri.

Hakika sisi tunakuta katika historia yetu ya Kiislamu na katika historia ya binadamu, na katika wakati wetu namna gani watu wanapata taufiki ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kufanya kheri na kuhudumia watu, na tunakuta wengine wanafanya ubakhili na wala hawajitolei kuhudumia watu wa jamii yao. Hakika mwanadamu anapokuza hali ya kupenda kheri katika nafsi yake anahisi utamu na raha na anahisi furaha na mafanikio kila anapofanikisha kitu na kutoa huduma kwa wengine, kama ambavyo anahisi utamu mweye kupata faida katika biashara yake, au anapopata kitu miongoni mwa maslahi yake na raghaba yake. Na hisia hii ya furaha na raha ndio ambayo inamshajiisha katika kuendelea katika amali ya kheri na kumsukuma katika mwelekeo wa kheri. Lakini baadhi ya watu wanapokonywa hisia ya utamu wa amali ya kheri, bali wanakuwa wazito kufanya hilo.

Na kwa ajili ya kuleta fikra karibu inawezekana, kuifananisha hisia hii na mwenye kumiliki hisia na shauku ya sanaa ambapo anapiga ngoma na anahamasika kwa kusikiliza kaswida yake ya ushairi, kwa sababu anapata ladha ya sanaa, wakati ambapo kama



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 97 8/27/2015 2:17:30 PM

atasikia kaswaida yule ambaye hana maarifa ya sanaa wala hakuna vionjo vya sanaa kwake hakika hatohamasika, pamoja na mazingira ya kaswida bali anaweza kuona ni kupoteza wakati. Hali ni hiyo hiyo katika fani ya uchoraji. Mtu anaweza kuingia katika maonyesho ya fani ya kuchora na kuvigeuza vibao katika maonyesho kwa ucheshi na kuchangamka mbele ya kila kibao, na kinyume cha hivyo anaweza kupita mtu mwingine katika vibao hivi kwa haraka, kwa sababu hana mazingatio na vionjo vya fani ya sanaa.

Hakika kuhamasika katika amali ya kheri ni katika aina hii. Baadhi ya watu wanahisi utamu wanapowahudumia watu au wanapofanya mradi fulani wa kijamii, wakati ambapo baadhi ya wengine hawajali mfano wa mambo haya wala hawahamasiki nayo. Na kujitolea katika kazi ya kheri kunadhihirika zaidi katika mwonekano ufuatao:

**Kulingania Kheri:**

Mwanadamu anaweza kuwa ni sababu ya kufanya kheri na mshaji-ishaji juu yake, na hiyo ni kwa kuwalingania wengine na kuwasuku-ma katika kufanya yanayohitajiwa na mahitaji ya jamii. Ni maneno mangapi mazuri yalikuwa ni sababu ya kheri nyingi na mafanikio. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

أَلَمۡ تَرَ كَيۡفَ ضَرَبَ ٱللَّهُ مَثَلٗا كَلِمَةٗ طَيِّبَةٗ كَشَجَرَةٖ طَيِّبَةٍ أَصۡلُهَا ثَابِتٞ وَفَرۡعُهَا فِي ٱلسَّمَآءِ ﴿٢٤﴾ تُؤۡتِيٓ أُكُلَهَا كُلَّ حِينِۢ بِإِذۡنِ رَبِّهَاۗ وَيَضۡرِبُ ٱللَّهُ ٱلۡأَمۡثَالَ لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمۡ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٢٥﴾

**"Je hukuona jinsi Mwenyezi Mungu alivyopiga mfano wa neno zuri kama mti mzuri, mizizi yake ni imara na matawi yake yako**

**mbinguni. Hutoa matunda yake kila wakati kwa idhini ya Mola Wake. Na Mwenyezi Mungu huwapigia watu mifano ili wapate kukumbuka." (Sura Ibrahimu: 24 -25)**.

Na imepokewa katika hadithi kutoka kwa Mtume صلى الله عليه وآله وسلم: "Mwenye kuonyesha kheri ni kama mtenda kheri." [40] Na kutoka kwake صلى الله عليه وآله وسلم: "Mwenye kuonyesha kheri basi anao mfano wa malipo ya mtendaji wake."[41]

Hakika kushajiisha wengine katika amali ya kheri hakuji bure na wala hafanyi hivyo kila mtu, bali anafanya mwenye kubeba amali ya kheri, na kuzingatia mambo ya jamii na akili yake inakuwa ni yenye kushughulika na kuwahudumia watu. Anakuwa ni mlingania kheri kutoka ndani ya moyo wake, kwa ukweli na kwa mazingatio. Ni mwenye kuandamana na juhudi ya kiakili ili kuonyesha katika namna ya mradi wa kivitendo unaokubali kutekelezeka na kufanyiwa kazi.

Marjaa wa kidini Marhum Sayyid Muhammad Shiraziy (r.m) ni mfano mzuri. Watu walimfahamu katika nyanja za kulingania katika kheri. Alikuwa hakutani na mtu isipokuwa anapendekeza kwake mradi unaolingana na hali yake na mazingira yake, ima kuandika kitabu, au kujenga msikiti au kuanzisha taasisi au kuanzisha harakati ya huduma za kidini au za kijamii. Akili yake ilikuwa ni taa na kana kwamba ni hazina ya fikra na miradi, alikuwa anatoa juhudi katika kumkinaisha mtu mmoja mmoja au kundi kwa kumwelekeza katika kushughulika na amali ya kheri kwa kumtajia nususi za kidini na kueleza matukio na namba, na kuleta visa na ushahidi. Mimi binafsi (mwandishi) nimeona na nimesoma kuhusu watendaji wengi ambao wamehamasika

[40] Wasailua-Shi'ah, Juz. 16, Uk. 123, Hadithi namba 21145.

[41] Abu Daud Suleiman bin al-Ash'athi as Sajastaaniy katika *Sunan Abi Daudi*, Juz. 2, Chapa ya kwanza 1409 Hijiria (Beirut Daru al- Jinaan), Uk. 755, Hadithi 5129.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 99 8/27/2015 2:17:30 PM

na ushajiishaji wake na wito wake na wamepata mafanikio na huduma kubwa katika nyanja mbalimbali za kuhudumia Uislamu na Waislamu.

**Kwenda Mbio na Kufuatilia:**

Kuna mambo mengi watu wanayahitaji ambayo yanaweza kufanywa na serikali au sekta zinazoshughulika na mambo ya kidini na kijamii, lakini katika utekelezaji wake kuna haja ya kuwepo mtu mwenye kutoa mapendekezo na kufuatilia utekelezaji. Hakika sekta zinazohusika zinaweza zisijue baadhi ya mahitaji ya jamii na mambo yao, na inawezekana kukawa na upungufu katika baadhi ya vyombo vya utekelezaji. Na wakati wanaposhughulika baadhi ya wananchi kwa kuwajulisha viongozi na kubainisha mahitaji na mapungufu, hakika inaweza ikawa ni sehemu ya kupatikana ufumbuzi wake. Na tumeshaona ushahidi mbalimbali katika hayo, na Alhamdulillahi hakika kwenda kwa viongozi na kuzungumza pamoja nao ni jambo jepesi katika nchi yetu.

Na vyombo vya habari vya ndani vina nafasi nzuri katika nyanja hii, ambapo vinasambaza ukweli wa baadhi ya matatizo na mapungufu ambayo yanawakabili wananchi katika nyanja hii au ile, jambo ambalo linawazindua viongozi na kufichua uzembe wa baadhi ya vyombo na wafanyakazi, na hivyo wanawahi na kutatua.

Na baadhi ya mambo na mahitaji yanafungamana na pande za raia wenyewe kama vile taasisi za kijamii, watu wanaofanya kazi, na Maulamaa wa dini, na ikiwa kuna watu wanaozinduka na kupendekeza kitu kwao na kutoa mikakati na ratiba, hakika wengi wao ni watu wa kheri nyingi na wenye kuitikia ushauri wa wanajamii. Na ni juu yetu wakati tunashughulika na mfano wa mambo haya,



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 100 8/27/2015 2:17:30 PM

tuwashughulishe na wengine pamoja nasi ili wawe wengi wenye kufuatilia ili mifano ya hali hii nzuri ienee katika jamii.

Na miongoni mwa yanayosikitisha ni kusikia watu wengi katika jamii wanalalamikia baadhi ya mwonekano mbaya au upungufu fulani, au huduma fulani mbaya katika kuwahudumia wananchi katika baadhi ya nyanja, lakini pamoja na hayo hukuti anayeshughulika kwa ajili ya kurekebisha na kubadilisha hali hiyo. Hakika kushughulika katika mambo haya ya umma ni kati ya uhalisia wa dua ya Imamu Zainul-Abidin عليه السلام: "Na pitisha katika mikono yangu kheri kwa ajili ya watu."

Baadhi wanaweza kusema kwamba juhudi hizi chache hazina faida, lakini sisi katika utamaduni wetu wa kidini tunakuta kufanya jitihada katika kheri kuna thawabu na malipo. Na tunakuta mara nyingi anapoandika mmoja wa waandishi katika gazeti la ndani juu ya haja na mahitaji ya mwanadamu mgonjwa au fakiri na kueleza tatizo lake, hazipiti isipokuwa siku chache mmoja ya watu wema anawasiliana na gazeti (husika) na anajitolea kutatua tatizo la huyu mwenye haja.

Hakika kujali kwa baadhi ya waandishi baadhi ya matatizo ya kijamii inapelekea mara nyingi kutatuliwa kwake, na hii ni dalili yenye nguvu juu ya kwamba vitendo vya kheri katika baadhi ya sehemu zake vinaweza visihitajie isipokuwa kuomba na kufuatilia, sawa iwe katika sekta rasmi au zisizo rasmi.

## Kujitolea Katika Amali ya Kheri:

Kila jamii inahitaji sana kujitolea katika amali ya kheri, na Qur'ani Tukufu imesimulia katika Aya nyingi juu ya fadhila ya kufanya haraka katika kufanya kheri, na anasema (swt): **"Fanyeni haraka katika kheri."** Na anasema (swt): **"Na wanafanya haraka katika**



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 101 8/27/2015 2:17:30 PM

**kheri na hao ni miongoni mwa wema." (Sura Imraan: 114)**. Na imepokewa kutoka kwa Imamu Ali bin Abutalib عليه السلام kauli yake: "Ni juu yenu kufanya amali za kheri. Zifanyieni haraka na wala isije ikawa wasiokuwa nyinyi wana haki zaidi kwayo kuliko nyinyi."[42]

Na inasikitisha kuona wananchi wengine wasiokuwa Waislamu wanajitolea katika kuanzisha shughuli mbalimbali za kheri katika jamii zao na katika kiwango cha kiulimwengu, wakati ambapo hali hii inapungua katika jamii zetu za Kiislamu. Jarida la al-Hayatu limesambaza ripoti kuhusu Chuo cha Hadson cha Maendeleo ya Ulimwengu, chini ya anwani 'Kiashirio cha Misaada ya Kheri Ulimwenguni', ripoti hii inazungumzia juu ya taifa la Marekani na Wamarekani wanavyotoa misaada ya kheri. Inaashiria kwamba rekodi zilizoandikwa zinadhamini kiasi cha dola bilioni 71 katika mambo ya kiulimwengu kutoka katika jumuiya za kheri za kimarekani, taasisi za kidini, vyuo na mashirika.

Na ripoti inaashiria kwamba sehemu ya misaada hii ni kutoka kwa wahamiaji waliohamia Marekani kutoka nchi nyingine, ambapo wanatuma fedha kwenda nchi walizotokea, na kinafikia kiasi cha dola bilioni 47, wakati ambapo misaada ya Wamarekani wenyeji kwenda sehemu nyingine inafikia dola bilioni 24. Na ripoti inasema kwamba nusu ya Wamarekani walio baleghe wanafanya kazi ya kujitolea, wakati ambapo kama tukifanya uchunguzi katika jamii zetu tutakuta kwamba kiasi cha wafanyakazi katika nyanja za kujitolea ni kiasi kidogo sana. Na kati ya mambo yanayotajwa na ripoti ni kwamba vyama mahususi vya Kimarekani vya kujitolea peke yake vimetoa kiasi cha dola bilioni 9.7 kwenda kwenye nchi zinazoendelea; Na kwamba katika muongo uliopita taasisi za kheri huko Marekani zimeongezeka kwa kiasi cha asilimia 77 na

[42] Abdul-Wahdi al-Amadiy Tamimiy katika *Ghuraril-Hikami wa Duraril-Kalimi*.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 102 8/27/2015 2:17:30 PM

uchangiaji wa watu kwa taasisi hizi umeongezeka kwa kiasi cha asilimia 100.[43]

Hakika kila mmoja anatakiwa awe ni sehemu ya kazi ya kujitolea katika jamii, na wala haisihi kwa yeyote kuikubalia nafsi yake iwe ni yenye kuangalia mahitaji ya jamii na hali zake bila kufanya chochote. Aitake nafsi yake kuwa ni sehemu ya taasisi yoyote ya kheri ya kijamii, na katika hayo kuna thawabu na malipo makubwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na hiyo ndio njia ya kuendelea jamii.

---

[43] Jarida la *al-Hayat*, Toleo la 15721 la Alhamisi 20 April 2006 sawa na 22 Rabiul-Awwal 1427 Hijiria, Uk. 23.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 103 8/27/2015 2:17:30 PM

# MSOMI NA JUKUMU LA KUDHIHIRI-SHA RAI[44]

Tatizo lingine ni tatizo linalokabili jamii nyingi za Kiarabu na za Kiislamu, lakini linatofautiana katika daraja ya ukubwa na ugumu. Na tatizo hilo linafungamana na sababu tatu za kimsingi zinazozalisha tatizo hili, kuliimarisha na kulilazimisha katika jamii.

**Sababu ya kwanza**: Ufahamu wa kidini ulioenea katika jamii hizi ambao unazingatia kuwa rai ya mwingine ni upotovu na uovu na ni wajibu kupigwa vita na kuondolewa.

**Sababu ya pili**: Siasa ya mifumo tawala ambayo inapinga uwepo wa rai nyingine inayokhalifu mwelekeo wake na misimamo yake, na hayo ni miongoni mwa mambo ambayo yamefanywa na mifumo mbalimbali katika nchi za Kiarabu na za Kiislamu, miongoni mwa Ujamaa, Kilebrali na Kiislamu. Hakika baadhi ya walahidi na wakosoaji wa hali ya kidini wanazungumza juu ya kumwangamiza mwingine, kama ni alama ya mwelekeo wa kidini tu, na hii ni kutokujua ukweli, Wajamaa katika zama za utawala wao walitumia ukandamizaji mkali kwa wapinzani wao, na Waba'athi (chama cha Sadam Husein) Iraki kwa mfano, walikandamiza Hawza za elimu za Najafu na wakazima harakati zote za Kiislamu za Masuni na Mashia. Na walifanya vivyo hivyo watu wa al- Qaumiya ya Nasri huko Misri.

**Sababu ya tatu**: Inaonekana katika malezi na ada za kijamii ambazo zinamlea mtu katika misingi kwamba kutoa rai inayopingana na ya baba au mzee wa kabila au kiongozi wa idara au mwanachuoni

44 Imesambazwa katika gazeti la *al-Madinatu* linalotolewa na Muasastu al- Madiynati Liliswahafati wa Nashiri, kiambatanisho cha Jumatano cha Thaqafiy, Toleo la 14860 la taerehe 8 Dhil Qaad 1424 Hijiria.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 104 8/27/2015 2:17:30 PM

wa kidini ni ukosefu wa adabu na ni kinyume na heshima na adabu, na anaweza akakabiliwa na kisasi cha hasira na kupatiwa adhabu. Hakika haiwezekani kuvuka tatizo hili isipokuwa kwa kutatua sababu ambazo zimelizalisha na kulilazimisha katika hali ya jamii zetu.

Ni lazima kuangalia upya katika ufahamu huu uliopo wa kidini katika jamii yetu, ikiwa Mwislamu anaamini usahihi wa itikadi yake na rai yake ya kidini, na anaona kwamba kuna haja ya kisharia katika kupiga vita upotovu ambao unaonekana katika rai ya mwingine, basi ni juu yake ajue kwamba kukabiliana na rai inakuwa ni kwa rai nyingine. Ama kuzuia, kukandamiza, kufuta na kutokomeza, inapelekea kwenye natija ya kinyume chake, ambapo rai nyingine itatekeleza dauru yake kwa kificho na kuwa na nguvu kwa sababu ya changamoto, na inaweza kushangaza kwa kusambaa kwake na kuvutia kwa nguvu ambayo imeilimbikiza mbali na mwangaza.

Qur'ani tukufu imelingania kwenye kukabiliana na rai kwa namna bora zaidi ya mazungumzo na tabia njema na muamala mzuri: **"Lingania katika njia ya Mola Wako kwa hekima na mawaidha mazuri na jadiliana nao kwa ambayo ni bora zaidi."** Bali imekataza kutumia lugha ya kumuudhi mwingine wakati wa kujadiliana naye **"Wala usijadiliane na watu wa kitabu isipokuwa kwa njia iliyo bora zaidi."** Hakika Qur'ani Tukufu inalingania wengine kutoa rai zao na kudhihirisha hoja zao na dalili zao **"Sema leteni hoja zenu," "Sema je, mnayo elimu muitoe kwetu?"**

Na katika upande mwingine, hakika mlango wa ijitihadi katika kufahamu dini uko wazi, na wala haisihi kwa yeyote kumiliki tafsiri ya dini na ufahamu wake, na kutuhumu kila rai nyingine kwamba ni upotofu na bidaa, kwa sababu ni haki kwa wengine kukabiliana naye kwa mantiki hiyo hiyo, na ikiwa anaitakidi kwamba anamiliki



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 105 8/27/2015 2:17:31 PM

hoja yenye nguvu juu ya usahihi wa rai yake hakika wengine pia wanaitakidi katika nafsi zao hayo vile vile.

Na katika upande mwingine hakika siasa ya serikali ndio yenye athari kubwa katika hali ya jamii zetu, na ikiwa serikali itatoa fursa sawa kwa pande zote, na hususan katika nyanja ya matangazo na kazi ya utamaduni na kijamii, basi wingi na kuamiliana kwa amani baina ya makundi ya kijamii ndio hali itakayokuwepo. Kama tunavyokuta hayo katika nchi nyingi. Ama kufungamana na upande fulani na kuweka nguvu zote chini ya mamlaka yake na kuwanyima wengine fursa ya kutoa rai zao na uwepo wao matokeo yake yatakuwa ni ubinafsi na udikteta wa kifikra. Baadhi ya pande zinatumia nafasi ya ukandamizaji inayoimarisha udikteta na ubinafsi na kuimarisha hali ya uchupaji mipaka. Na vyombo vya habari katika nchi zetu vyote ni rasmi, runinga na idhaa zinafanya kazi kwa mfumo wa ubinafsi havina nafasi isipokuwa kwa ajili ya rai ya mwelekeo mmoja tu.

Hapa ni lazima msomi abebe jukumu la kudhihirisha rai yake na kujiandaa kulipatia thamani. Tatizo letu ni kwamba wasomi wengi wao hawataki kuupa thamani uhuru wanaouzungumzia na wanaoulingania, wanaogopa kupitwa na manufaa fulani. Hakika jamii zetu ziko katika hatua hatari kubwa na ni juu ya wasomi kusimama kivitendo sambamba na maarifa yao na jamii zao na wawe na ushujaa na ujasiri zaidi katika nyanja za kutoa rai. Ama watu ni wajibu wavuke msimamo mbaya na kuangalia mateso ya wanafikra na wasomi na wenye ijitihada mbalimbali za Kiislamu. Mas'ala sio ya kibinafsi yanafungamana na mwandishi au mtunzi au maktaba ambayo inasambaza kitabu bali yanafungamana na haki ya watu katika maarifa na utambuzi.

Jamii zetu zimeshalipatia thamani kubwa kutokana na makundi yenye kuchupa mipaka na ya kigaidi wala haiwezekani kukabiliana na uchupaji huu mipaka isipokuwa kwa kukubali wingi na uhuru wa rai.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 106 8/27/2015 2:17:31 PM

# KUFUTA UTU WA MTU BINAFSI

Kukomboa utu wa mtu binafsi, na kumuokoa kutokana na uovu na udhibiti wa jamii katika fikra yake na mwenendo wake, ilikuwa ni jukumu la msingi la ujumbe wa Manabii. Hiyo ni kwa sababu hakika mtu binafsi katika jamii zisizoendelea, zenye kutengana na jamii ambazo zinatawaliwa na udikteta, utu wake unakuwa ni wenye kukandamizwa, ni zenye kuporwa matakwa, hazina haki ya kufikiri. Kuna fikra iliyoenea inayowakilisha haki ya jumla na hakuna uhuru wa kutoa rai nyingine, kwani huo ni ukafiri, uzandiki, upotofu na bidaa, na wala hakuna fursa mbele yake ya kuchagua muundo wa tabia na namna ya kuishi. Yeye ni mtu katika kundi na ni nakala iliyorudufiwa katika utu wa jamii, hakuna mabadiliko humo. Hakika yeye anayeyuka kikamilifu na inakosekana humo hisia yoyote katika dhati.

Na anapokuja Nabii kwenye jamii yake anawalingania watu kwa Mwenyezi Mungu. Hakika daawa yake inagongana na hali hii ambayo ndani yake hakuna ujasiri wa kusikiliza rai ya mwingine au kujadili fikra mpya. Hapa Nabii anakabiliana na kutibu mizizi ya tatizo, nayo ni kuyeyusha ubinafsi wa mtu na ufuataji wake wa jumla wa kundi na kudumaza kwake akili yake na matakwa yake.

Na katika Qur'ani Tukufu kuna aya nyingi zinazozungumzia juu ya mapambano ya Manabii kwa ajili ya kumkomboa mwanadamu kutoka kwenye udhibiti wa kundi ambalo linafuta utu wake na kupora matakwa yake. Nabii Muhammad صلى الله عليه وآله وسلم anaelekeza daawa yake moja kwa moja kwa watu kwamba watoe fursa kwa nafsi zao ya kufikiri nje ya udhibiti wa kundi, na kwamba hiyo inatosha kubadilisha mwelekeo wa maisha yao. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 107 8/27/2015 2:17:31 PM

۞ قُلۡ إِنَّمَآ أَعِظُكُم بِوَٰحِدَةٍۖ أَن تَقُومُواْ لِلَّهِ مَثۡنَىٰ وَفُرَٰدَىٰ ثُمَّ تَتَفَكَّرُواْۚ ﴿٤٦﴾

**“Sema hakika ninawapa mawaidha kwa jambo moja tu kwamba msimame kwa ajili ya Mwenyezi Mungu wawili wawili na mmoja mmoja; Kisha mfikiri.” (Sura Sabaa: 46)**.

Na Manabii wote walikuwa wanapinga mantiki ya kufuata waliotangulia na kufuata bila ya kutumia fikira na mtazamo **“Bali walisema hakika sisi tulikuta baba zetu wako katika mila na sisi ni wenye kufuata nyendo zao” (Sura Zukhurufu: 22)**. Mwenyezi Mungu anawahadharisha wanajamii ya kibinadamu na utii wa upofu kwa viongozi na vituo vyenye nguvu katika jamii, anasema (swt): **“Na wakasema Mola wetu hakika sisi tumewatii viongozi wetu na wakubwa wetu basi wakatupoteza njia.” (Sura al-Ahzab: 67)**.

Hakika aya hizi tukufu sio tu zinaashiria watu waliopita bali ni ubainifu wa mfumo wa Mwenyezi Mungu katika kupanga uhuru wa mwanadamu, na kulinda utashi wake katika kufanya vitendo vyake na kutumia akili yake hadi asitumbukie chini ya udhibiti wa wengine na kumpokonya utu wake. Na hakuwa akiitikia daawa ya Manabii isipokuwa mwenye ushujaa wa kuasi na kupinga udhibiti huo, na kuamua kutumia haki yake katika kufikiri na kuchagua.

Hivi ndivyo ilivyokuwa dini katika uhakika wake na uhalisia wake, daawa ya kukomboa akili ya mwanadamu na matakwa yake, na njia ya kujinasua na unyenyekevu na udhalili kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Lakini tofauti inayoshangaza katika historia ya dini ni umma na jamii kurudi nyuma dhidi ya mafanikio ya zama za Manabii na mwanadamu kurejea katika udhibiti wa utawala wa kijamii na kutumbukia katika kibano cha udikteta upya, chini ya joho la kidini na kutumia nembo zake na anwani zake



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 108 8/27/2015 2:17:31 PM

na dini kugeuka kutoka katika chombo cha kukomboa na mfumo wa mapambano, na kuwa ni nyenzo ya udhalili na chombo cha ukandamizaji. Kama inavyosimulia hayo historia ya Ulaya katika zama za kati, na historia nyingi ya Waislamu baada ya zama ya Nabii na ukhalifa mwongofu, hivyo pindi alipopinga Arius, mwaka 336 kauli ya uungu wa Isa alishutumiwa na vitabu vyake vikachomwa moto na ikaharamishwa kuvinunua na wafuasi wake wakavuliwa vyeo vyao, na akahukumiwa kunyongwa yule aliyeficha chochote katika vitabu vyake au aliyempa hifadhi yeyote kati ya wafuasi wake.

Na fedheha za mahakama za upelelezi ambazo zilianzishwa na kanisa katika zama hizo ni mashuhuri kuliko kuelezwa. Zilikuwa zinawaadhibu watu si tu kwa rai zao za kidini zenye kukhalifu, bali kwa rai wanazozifuata katika mambo ya kawaida ya kimaisha. Galileo alihukumiwa kwa sababu ya kusema kuwa ardhi inazunguka. Na ilifikia idadi ya waliohukumiwa hukumu za adhabu kwa sababu ya rai zao zaidi ya watu 300,000, kati yao watu 32,000 waliuliwa kwa kuchomwa moto.

Kama ambavyo jamii ya Kiislamu iliteseka katika zama zake nyingi katika hali inayofanana na vitendo vya mahakama za upelelezi. Hii ndio hali ya jumla katika jamii za kuiga ambazo hazitambui uhuru wa mtu binafsi wala haziruhusu kuneemeka na uhuru wa watu binafsi na wanamtaka awe ni sehemu ya kundi lisilojiengua katika rai au mwenendo, hivyo hakupatikani mtu anayetofautiana na mtu mwingine, wala sifa mahususi anayotofautiana kwayo na wengine. Na ilikuwa muundo wa maisha ya kiuchumi ni mfinyu sana katika jamii ya kuiga inayoimarisha hali ya kuteketeza, ambapo ilikuwa inategemea kuwinda au kuchunga au kulima, na watu wote wa kabila walikuwa wanafanya kazi hiyo hiyo na wanaishi katika namna moja ya daraja ya maisha.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 109 8/27/2015 2:17:31 PM

Na inawezekana kuelezea hali ya kuteketeza na kukandamizwa mtu binafsi katika jamii hizo kwa sifa zifuatazo:

- Mtu binafsi hana uoni wala lengo analolikusudia kwa sababu haoni uwepo huru wa nafsi yake, unaomsukuma katika uoni na kutaraji. Yeye ni sehemu ya kiungo katika kundi linaloendeshwa bila ya utambuzi au matakwa yake. Kama alivyosema mshairi wa kabila la (Ghuziyah):

  "Je, mimi si natokana na Ghuziya, kama wakipotea, nami napotea, na kama Ghuziya wakiongoka nami pia naongoka."

- Kifikra: Si haki kwake kufikiri nje ya uzio wa fikira iliyopo katika jamii yake, wala haijuzu kwake kuwa na rai inayokhalifu. Hakika ni wajibu wake kuamini fikira ya jamaa na kuitakidi usahihi wake, kwani ndio haki pekee, na isiyokuwa hiyo ni upotovu na ni bidaa. Hata katika lengo la sharia ya Kiislam pamoja na kukubali kurejea kwenye Kitabu na Sunna, hakika akili ya kundi, kufuata na roho ya kasumba ya kundi, imeshapenya ndani ya hali ya kielimu na kidini, hadi imenukuliwa kutoka kwa Abu Hasan al-Karakhiy kauli yake: "Kila aya inayokhalifu waliyonayo jamaa zetu basi imefanyiwa taawili au imefutwa, na kila hadithi ya namna hiyo basi imefanyiwa taawili au imefutwa."[45]

- Kitabia: Mtu binafsi anashikamana na ada, mila na desturi zilizopo katika jamii, hata kama gharama yake ni kubwa au hata kama hakukinaika nazo, kwa sababu kudharau chochote kati yake kunampelekea kudharauliwa. Hakuna hiyari mbele yake katika kujenga maisha yake, kwani

[45] Sayyid Saabiq katika *Fiqihi Sunnah*, Juz. 1, Chapa ya tatu 1977 (Beirut Darul- Kitabi), Uk. 13



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 110 8/27/2015 2:17:31 PM

anaweza kupokonywa haki ya kuchagua mshirika wa maisha yake kama vile mume kwa mfano, na maamuzi yanakuwa mikononi mwa familia. Na vivyo hivyo katika nyanja nyingine za maisha.

Na ijapokuwa maendeleo ya maisha katika jamii ya kibinadamu yamelazimisha hali mpya ya mtu kuneemeka kwa kiasi kikubwa cha uhuru binafsi, baadhi ya jamii bado zingali zinabana watu wake kwa ubabe kupitia mifumo ya udikteta wa kisiasa, na mielekeo ya ubabe wa kidini na ukali wa mila na ada  za kijamii.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 111 8/27/2015 2:17:31 PM

# ISTIKHARA NA KUSITASITA KATIKA MAAMUZI

Mwanadamu anaweza kukuta nafsi yake wakati wa kuchukua maamuzi kwamba yuko katika hali ya tahayari na kusitasita, na kwamba mbele yake kuna zaidi ya hiyari moja, je, afanye jambo au aache? Na je, alifanikishe kwa njia hii au kwa njia nyingine?

Pamoja na kwamba mwanadamu anakaribia kutosalimika na kutumbukia katika hali ya tahayari na kusitasita wakati wa kuchukua baadhi ya maamuzi ila kiwango cha hali hii kinatofautiana kati ya mtu na mwingine kwa uchache au kujirudiarudia katika kutokea kwake na katika namna ya kuamiliana nayo. Watu wengi wanapatwa na hali ya kusitasita wakati wanapokuta nafsi zao mbele ya tukio la ghafla au jambo kubwa lenye athari kubwa katika maisha yao na maslahi yao, na hili ni jambo la kawaida. Lakini kuna uhusiano baina ya hali ya kusitasita katika mambo na misimamo mbalimbali, na hali hii sio ya kawaida. Hakika tahayari na kusitasita katika kuchukua maamuzi kuna sababu nyingi, muhimu zaidi ni hizi zifuatazo:

**Kwanza**: upungufu wa mwanadamu wa kutojua pande za maudhui ya maamuzi, jambo ambalo linamfanya asiamini uwezo wa kulifanikisha, au kutopata matumaini ya usalama wa matokeo yake au kutokuwa wazi njia bora na mbinu bora ya kulifanikisha.

**Pili**: Msongamano wa raghaba na maslahi katika nafsi ya mwanadamu. Yeye anataka kitu lakini anaogopa kupitwa na raghaba nyingine, na anatarajia chumo fulani, lakini hilo linaweza kumgharimu thamani ambayo hataki kuilipa. Hakika yeye wakati huo analazimika kutanguliza maslahi juu ya mengine, na kwa



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 112 8/27/2015 2:17:31 PM

kuvumilia baadhi ya hasara kwa ajili ya baadhi ya manufaa, jambo ambalo linamtumbukiza katika kudumu na tahayari na kusitasita.

**Tatu**: Udhaifu wa kujiamini na azma. Kuna uhusiano madhubuti baina ya hali ya kusitasita kwa mwanadamu na kiwango cha kuiamini nafsi yake na kiwango cha azma yake na matakwa yake. Wenye kujiamini sana katika nafsi, na wenye nguvu katika azma, kunapungua kwao tahayari na kusitasita katika kuchukua maamuzi, wakati ambapo wenye udhaifu wa azma na kujiamini katika nafsi zao wanakuwa ni mateka wa hali hiyo isiyokuwa sawa kutokana na wingi wa kusitasita na mkanganyiko katika kuchukua maamuzi.

Na ada na mazoea vinaathari kubwa katika upande huu, ambapo mwanadamu anaweza kuimarisha hali ya kujiamini katika nafsi yake na kuimarisha azma yake anapotegemea fikira na kutumia umakini na kutoikubalia hali ya kusitasita.

**Akili na Uendeshaji wa Maisha:**

Kati ya dalili zilizo wazi zaidi juu ya kuwepo Mwenyezi Mungu Mtukufu na utukufu wa mamlaka Yake ni kule kuwepo nidhamu yenye kuutawala ulimwengu na maisha, ni kutokuwepo humo upuuzi wala fujo **"Je, mnadhani kwamba tumewaumba bure" (Sura Muuminina: 115)**, **"Mola Wetu hukuviumba hivi bure" (Sura Imran: 191)**. Hakika kila chembe katika ulimwengu imepatikana kwa lengo maalumu na madhumuni yaliyopangwa, na inakwenda kutembea katika utaratibu makini na kipimo madhubuti, anasema (swt): **"Hakika kila kitu tumekiumba kwa umakini" (Sura al-Qamar: 49)**. **"Mwenyezi Mungu amejaalia kila kitu kwa kipimo." (Sura Twalaaq: 3)**. **"Na kila kitu kwake kipo katika kipimo." (Sura Raad: 8)**.

Na Mwenyezi Mungu alipoudhalilisha ulimwengu ili umtumikie mwanadamu, hakika Mwenyezi Mungu alimpa mwanadamu uwezo utakaomwezesha na kumsaidia kujua kanuni na njia zenye kutawala ulimwengu na maisha **"Na akamfundisha Adamu majina yote" (Sura al- Baqara: 31)**, na uwezo huo ni akili tukufu. Kwa akili mwanadamu anavumbua njia za maisha na mifumo ya ulimwengu, ili aweze kunufaika na viumbe na kheri ambazo Mwenyezi Mungu amezidhalilisha kwake, na ili aweze kuendesha maisha yake na kuendesha mambo yake. Na kwa kiwango ambacho mwanadamu anaelekea kwa akili yake na kutumia fikira yake, maarifa yake yanasonga mbele na kuongezeka uwezo wa kuathiri kwake na kuendeleza maisha yake. Na kwa hiyo hakika mwanadamu analinganiwa kuangalia hazina hii tukufu, akili, kuamini na kustawisha uwezo wake mkubwa, na kuongoka kwa nuru yake yenye kuangaza katika njia ya maisha.

Hakika ni juu ya mwanadamu airejee akili yake wakati wa tatizo lolote linalompata, na katika kujibu swali lolote linalomjia mbele yake, na wakati anapotaka kuchukua maamuzi yoyote au kufuata njia yoyote au kufanya jambo lolote. Na kitu hatari zaidi kwa mwanadamu na kibaya zaidi ambacho anaweza kutumbukia humo, ni kuipinga kwake akili yake na kughafilika kwake kujihukumu kwayo, na kuongoka kwa nuru yake, na wakati huo anakuwa ni kitoweo cha ujahili na ukhorafi, na mateka wa matamanio na hawaa.

Na kwa kiwango cha kughafilika kwake juu ya akili yake anakosa kiwango cha utambuzi wake wa kibinadamu, na anateremka kwenda kwenye kiwango cha wanyama. Kama anavyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu katika sifa ya wenye kughafilika na akili zao:



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 114 8/27/2015 2:17:31 PM

ۖ لَهُمْ قُلُوبٌ لَّا يَفْقَهُونَ بِهَا وَلَهُمْ أَعْيُنٌ لَّا يُبْصِرُونَ بِهَا وَلَهُمْ ءَاذَانٌ لَّا
يَسْمَعُونَ بِهَآ ۚ أُوْلَٰٓئِكَ كَٱلْأَنْعَٰمِ بَلْ هُمْ أَضَلُّ ۚ أُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْغَٰفِلُونَ

**"Wana nyoyo lakini hawafamu kwazo, na wana macho lakini hawaoni kwayo na wana masikio lakini hawasikii kwayo, hao ni kama wanyama bali wao ni wapotevu zaidi, hao ndio walioghafilika" (Sura al-A'araf: 179)**.

Na kwa kuwa mwanadamu anakabiliwa na kutumbukia katika hatari hii kubwa, hatari ya kuisahu akili, Mwenyezi Mungu alituma Manabii na Mitume ili kumhadharisha mwanadamu kutokana na kuisahau akili yake na kumuongoza katika njia bora za kunufaika na akili, mbali na vikwazo, vizuizi na athari zenye kushawishi katika fikra. Na kwa hiyo tunaona Qur'ani inatilia mkazo katika mas'ala ya akili na kuwa na akili na yanayofungamana nayo miongoni mwa mifumo ya kufikiria, elimu, kutazama na kutafakari, ambapo kumepokewa tamko *al-Aqil* na *Ata'aqul* katika aya za Qur'ani Tukufu mara 49, kama vile kauli yake (swt): **"Je, hawatafakari"** ambalo limepokelewa mara 13, na kauli yake (swt): **"Ili mpate kuwa na akili"** ambalo limepokelewa mara 7.

Ama neno *al-Fikru*, na *Tafakur* limepokewa mara 18 katika Qur'ani Tukufu na limekuja tamko la *al-Fiqih* na *Tafaquhu* mara 20. Ama tamko *al-Ilimu* na *Taalum* limepokelewa katika mamia ya Aya. Na kwa kuongezea Aya ambazo zinazungumzia juu ya tadaburi, kukumbuka na kutazama. Kama ilivyokuja katika Sunnah Tukufu idadi kubwa kati ya Hadithi na riwaya ambazo zinatilia mkazo juu ya kuirejelea akili na kitovu chake katika maisha ya mwanadamu kwa namna ya jumla.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 115 8/27/2015 2:17:32 PM

- Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwamba amesema: "Hakika inafikiwa kheri yote kwa akili."[46]
- Na kutoka kwake ﷺ: "Ishaurini akili mtaongoka na wala msiiasi mtajuta."[47]
- Na kutoka kwake ﷺ: "Ukitaka jambo basi tafakari mwisho wake ikiwa ni kheri basi lipitishe na ikiwa ni shari basi liache."[48]
- Na anasema Imamu Ali عليه السلام: "Akili ni kutengenekewa kwa kila jambo."[49]
- Na kutoka kwake عليه السلام: "Hauombwi msaada dhidi ya dunia isipokuwa katika akili."[50]
- Na kutoka kwake عليه السلام: "Wala akili haimhadai mwenye kuitaka nasaha."[51]
- Na kutoka kwake عليه السلام: "Kwa kutafakari linapambanuka giza la mambo."

Nususi hizi za kidini na mfano wake zinatilia mkazo juu ya kuirejelea akili, na kwamba ni juu ya mwanadamu kurejea kwenye akili yake, na kuitumia fikira yake katika kukabiliana na tatizo lolote katika maisha yake, na kuchukua maamuzi yake kwa kujengea juu ya ambayo inamuongoza kwayo akili yake na kumwelekeza fikira

[46] *Biharul-An'war*, Juz. 74, Uk. 157
[47] Rejea iliyotangulia Juz. 1, Uk. 96
[48] *Kanzul-Ummal*, Juz. 3, Uk. 99, Hadithi 21075, na mfano wake katika *al-Kaafiy*, Juz. 8, Uk. 131 Hadithi ya 130.
[49] *Ghurarul-Hikam wa Durarul- Kalim*
[50] *Biharul-An'war*, Juz. 75, Uk. 7.
[51] Rejea iliyotangulia, Juz. 1, Uk. 95.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 116 8/27/2015 2:17:32 PM

zake pamoja na kulazimiana na mifumo ya fikira sahihi. Na ambayo ameyapata mwanadamu miongoni mwa mafanikio makubwa ya kielimu na kivitendo katika nyanja za kimaisha ni ushahidi mkubwa juu ya utukufu wa akili na uwezo wake katika kuvuka magumu na kukabiliana na changamoto.

Hakika miongoni mwa sababu za kusitasita mwanadamu katika kuchukua maamuzi ni udhaifu wa kuiamini akili yake na kutojitahidi kwake katika kutumia fikira zake, jambo ambalo linapelekea kudumaa uchangamfu wake wa kifikra, na inawezekana mwanadamu asitambue vidhibiti vya kutafakari kwa usahihi na hivyo anakanganyikiwa na mambo na kupatwa na tahayari na kusitasita.

**Kufaidika na Akili za Wengine:**

Mwanadamu anaweza kufikiri kuhusu maudhui ambayo hana ujuzi nayo katika baadhi ya vipengele vyake na anaweza kupatwa na mvutano na matamanio ndani ya nafsi yake, na anaweza kuishi katika mazingira yenye kumbana yanayomsukuma kwenye chaguo hili au lingine na kukuta nafsi yake ni yenye kushindwa kuchukua maamuzi na kuwa mateka wa hali ya kusitasita na kutahayari.

Hapa ni juu yake kurejea kwenye akili kwa mara nyingine kwa kunufaika na akili za wengine kati ya wale anaowaamini walio na mifumo sahihi ya kufikiri na kutafakari, wale ambao ana matumaini na ukweli wao na ujuzi wao katika maudhui, awatake ushauri na kupata msaada katika akili yao ili ashirikiane nao katika kufikiri na kulitazama jambo, ili avuke nukta za udhaifu ambao zimemsababishia tahayari na kusitasita. Na Hadithi imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم kwamba kuwashauri wenye rai kunamsaidia mwanadamu kupata hali ya umadhubuti na



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 117 8/27/2015 2:17:32 PM

umakini na kuvuka tahayari na kusitasita, anasema صلى الله عليه وآله وسلم: "Udhibiti ni kuwashauri wenye rai."[52] Na katika Hadithi nyingine kutoka kwake صلى الله عليه وآله وسلم: "Hakuna mtu anayemtaka ushauri mtu isipokuwa anaongozwa katika yaliyo sawa."[53]

Na imepokewa kutoka kwa Imamu Ali عليه السلام kwamba amesema: "Mwenye kutaka ushauri kwa wenye akili huangaziwa kwa nuru ya akili."[54] Na kutoka kwake عليه السلام: "Ukipinga kitu katika akili yako basi fuata rai ya mwenye akili itaondoa uliyoyapinga."[55] Na kutoka kwake عليه السلام: "Ni haki kwa mwenye akili kuongezea katika rai yake rai za wenye akili."[56] Na Imamu Ali عليه السلام anaashiria kwamba miongoni mwa sifa muhimu za kutaka ushauri ni kuwa mtu mwingine ambaye unamtaka ushauri awe nje ya athari za vibano ambavyo vinasababisha kwa mwanadamu kusitasita, anasema عليه السلام: "Hakika imehimizwa kutaka ushauri kwa sababu mwenye kutakwa ushauri hajaathirika, lakini rai ya mwenye kutaka ushauri imechanganyika na matamanio."[57] Na kutoka kwake عليه السلام: "Mwenye kutaka ushauri kwa wenye akili anaongoka katika yaliyo sawa."[58] Kwa hakika ni juu ya mwanadamu kuwataka ushauri wenye msimamo na wenye ujuzi na uzoefu, anasema Ali عليه السلام: "Watake ushauri katika mambo yako wale ambao wanamuogopa Mwenyezi Mungu, utaongoka."[59] Na kutoka kwake عليه السلام: "Watu bora wanaofaa kutakwa ushauri ni wale wenye akili, elimu, wenye uzoefu na wenye udhibiti."[60]

---

[52] *Biharul-An'waar*, Juz. 72, Uk. 105
[53] Sheikh Tusiy katika *Majimaul-Bayaan*, Juz. 9, Chapa ya kwanza 1415 Hjiria (Beirut: Muasastu al-A'lamiy lilimatubuati), Uk. 57.
[54] *Ghurarul-Hikami wa Durarul-Kalim* 8634.
[55] Rejea iliyotangulia 5754
[56] Rejea iliyotangulia 4920
[57] Rejea iliyotangulia 3908
[58] *Biharul-An'war*, Juz. 74, Uk: 420.
[59] *Ghurarul-Hikam wa Durarul-Kalim* 5756.
[60] Rejea liyotangulia 4990.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 118 8/27/2015 2:17:32 PM

Na kutoka kwa Ma'aliy bin Khanisi amesema: Amesema Abu Abdillahi عليه السلام: "Kipi kinamzuia mmoja wenu anapopatwa na asilolijua kutaka ushauri kutoka kwa watu wenye akili, wenye dini na uchamungu." Kisha akasema Abu Abdillahi عليه السلام: "Kama atafanya hivyo Mwenyezi Mungu hatomdhalilisha."[61]

## Nafasi ya Istikhara:

Na ili mwanadamu akamilike na anufaike na nguvu ambayo Mwenyezi Mungu ameiweka katika akili yake, na kwa ajili ya kupevuka matakwa yake na kuinoa shakhisiya yake, Mwenyezi Mungu amempa uhuru wa kufikiri na kujituma, hivyo anafikiri na anaamua, anafanya kazi na anajituma ndani ya kanuni za ulimwengu na mifumo ya maisha, na kisha anabeba jukumu la uamuzi wake na kitendo chake.

Na kwa huruma ya Mwenyezi Mungu kwa mwanadamu, amemuongoza kupitia Mitume Wake na Manabii Wake kwenye mifumo sahihi ya kufikiri, na njia sahihi za kuchukua uamuzi, na mwelekeo bora zaidi wa kufuata katika harakati na kazi. Na hiyo ni kwa kumuongoza mwanadamu kwenye akili yake na kumtahadharisha dhidi ya kutii matamanio yake na utashi wake au kuathirika na visababishi vya ushawishi na upotovu.

Akili ndio rejea ya mwandamu katika kuendesha maisha yake, kama ambavyo nususi za sharia zinatilia mkazo na zinaungwa mkono na hali ya maendeleo ambayo ameyapata mwanadamu katika harakati za kuboresha maisha katika uhai wake. Lakini tatizo la mwanadamu ni jinsi ya kunufaika na akili yake na ni kwa kiwango gani atanufaika na kushikamana na mfumo sahihi wa fikra sahihi, na katika kiwango cha matakwa yake, ili kukabiliana na mashinikizo mbalimbali ya upotovu na upotoshaji na sababu za udhaifu na makosa.

---

[61] *Biharul-An'war*, Juz. 72, Uk. 102.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 119 8/27/2015 2:17:32 PM

Na mwanadamu anapokabiliwa na jambo lenye umuhimu kwake na mbele yake kukawa na chaguzi nyingi, hakika anahitajia daraja ya juu ya usafi wa nafsi, na fikira madhubuti na mtazamo salama ili achukue maamuzi ya kimaudhui yaliyo sawa. Na hapa mwanadamu anarejea kwa Mola Wake kwa kutaka kwake taufiki na ulinzi kwa kutaraji kwake kupata matumaini na kujiamini ili aongoke kwenye maamuzi sahihi na rai bora zaidi. Kuelekea huku kwa Mwenyezi Mungu ili kuvuka hali ya kusitasita na tahayari katika kuchukua maamuzi na kupata taufiki ya Mwenyezi Mungu na kulindwa kwake, ndilo jambo ambalo katika nususi za kidini na istilahi zake linaitwa Istikhara.

Na istikhara maana yake ni kutaka kheri katika jambo, na hii ndio maana ya kilugha. *Allahumma khar liy*: Yaani nichagulie mimi lililo bora zaidi kati ya mambo mawili, na jaalia lililo na kheri zaidi humo, na inaposemwa: *Kharallahu laka,* yaani ni amekupa ambalo ni kheri kwako. Na Raghibu al-Isfahaaniy (aliyefariki mwaka 502 Hijiria) amesema: "*Istakhaara llaha al-Abdu fakhara lahu*, yaani ametaka kheri Kwake naye akampa." Na Ibnu Idris amesema: "*Al-Istikharatu* katika maneno ya Waarabu ni dua" Na maana halisi ya istikhara ni dua na kutaka kheri kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na *istakharallaha*, ameomba kheri kutoka Kwake.

Na nususi ambazo zinamraghibisha mwanadamu katika kufanya istikhara na zinamhadharisha juu ya kufanya jambo kabla yake, hakika zinakusudia istikhara kwa maana hii yaani dua na kuomba kheri kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na baadhi ya nususi zinaelekeza kuwa ni kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuswali rakaa mbili na kusoma Sura au Aya za Qur'ani Tukufu na kumuomba Mwenyezi Mungyu Mtukufu kwa baadhi ya dua zilizopokelewa kutoka kwa Nabii صلى الله عليه وآله وسلم na Maimamu Watukufu عليهم السلام.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 120 8/27/2015 2:17:32 PM

Na kuna ufahamu mwingine na aina nyingine ya istikhara kwa maana ya kumtaka ushauri Mwenyezi Mungu Mtukufu, ili amuongoze mwanadamu katika maamuzi sahihi kupitia baadhi ya njia na mbinu za wazi, kama vile kufanya istikhara kwa kutumia Qur'ani Tukufu au tasbihi au karatasi. Na katika baadhi ya njia za istikhara kwa Wairan, wao hutumia diwani inayonasibishwa na Imam Ali عليه السلام au diwani ya Hafidh Shiraziy.

Na kuna upindukiaji kwa baadhi ya watu katika kufanya istikhara kwa kutumia msahafu mtukufu na tasbihi, kwa kuitakidi kwamba inadhihirisha rai ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika maudhui ambayo wanaifanyia istikhara. Na kutokana na utaratibu huu wa kupindukia wanadumaza akili zao na hivyo hawafanyi juhudi yoyote katika kutafakari na kujituma, wala hawaendi kuwataka ushauri wenye rai na uzefu, bali wanaharakisha katika kufanya istikhara katika kila jambo na katika tatizo dogo kabisa. Kama ambavyo baadhi wanatumia istikhara pasipo mahala pake, kama vile wanafunzi ambao wanafanya istikhara karibu na mtihani ili kutaka kujua mada na maudhui ambazo ni wajibu kwao kuzitilia mkazo wakati wa kuzipitia na kuzirejea. Na kuna baadhi ya wazazi ambao wamesitisha kuozesha binti zao hadi wakapitwa na msafara wa kuolewa kwa sababu tu wao wanafanya istikhara wakati anapowajia mposaji anayefaa.

Na imeenea kwa wengi kati ya wanadini kwamba matokeo ya kufanya istikhara kwa msahafu au tasibihi yanadhihirisha kheri na usahihi, hivyo ni juu ya mwanadamu kushikamana na istikhara hiyo na kwamba kuikhalifu kwake ni haramu au ni sababu ya hatari. Ni sahihi kuna riwaya zilizopokewa kuhusu kufanya istikhara kwa msahafu na tasibihi lakini sio kwa kiasi hicho cha daraja la usahihi na mazingatio. Na hata ikiwa kuifanyia kazi ni kwa msingi wa kanuni ya kufumbia macho hoja za Sunnah, na kuamini uzoefu wa



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 121 8/27/2015 2:17:32 PM

kupokezana kuhusiana nayo, na kwa kuwa imeenea baina ya watu wa sharia, lakini hakika hayo hayatoi kisingizio cha kuchupa mipaka na kupindukia katika kuitumia na kufumbia macho upande wa mabaya yanayotokana na jambo hilo.

Baadhi wanaweza kuona kwamba kukosoa kufanya istikhara ni kutilia shaka katika itikadi na ni kutoka katika mambo ambayo yameafikiwa na ni kutia ila katika kitendo halali kilichopitishwa na Marajii na wanachuoni. Hawa hawakuzipa nafsi zao taabu ya utafiti wa kielimu katika maudhui wala hawajui kwamba kuna rai nyingine ndani elimu inayoona ni makosa kufanya istikhara kwa msahafu na tasbihi, na mfano wake ni al-Muqadas al-Ardabiliy ambaye anaona uharamu wa kufanya istikhara kwa njia kama hii na anaiona kuwa inafanana na kuagua kwa mizimu.

Na Sayid al-Yazdiy katika *al-Uruwatul-Wuthqaa* yuko katika rai hii kwa kauli yake katika fasili ya Hija katika adabu za safari ya Hija, kwa tamko lake anasema: "Istikhara kwa maana ya kuomba kheri kwa Mola Wake na kumtanguliza Yeye wakati wa kusitasita katika asili ya safari, au katika njia yake au kwa ujumla, na katika lengo la safari na kila jambo muhimu au sehemu yenye hatari, na hususani wakati wa tahayari na kuhitalifiana katika ushauri, hiyo ni dua ili kheri iwe katika jambo lake, na aina hii ya istikhara (yaani dua) ndio asili, bali baadhi ya maulamaa wamepinga ile isiyokuwa hiyo, ikiwa ni pamoja na kufanya istikhara kwa kutumia karatasi, changarawe na tasbihi, kutazamia na mengineyo, kwa sababu hadithi zake nyingi ni dhaifu, ingawa kuzifanyia kazi kwa msingi wa kufumbia macho hoja za Sunnah si vibaya pia, ambapo ni kinyume na aina hii (kufanya istikhara kwa dua) ambapo kumepokewa habari nyingi juu yake."

Na inasikitisha baadhi kusema kwamba kukosoa istikhara ni kutilia shaka katika itikadi na ni kukhalifu mambo yaliyoafikiwa,



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 122 8/27/2015 2:17:32 PM

wakati kuna maelezo ya Marajii wakubwa wakionesha kutothibiti kwake kama Sunnah. Ambapo Sayyid Sistani (Mwenyezi Mungu amhifadhi) alipoulizwa: "Je istikhara inayofuatwa kwetu hivi sasa imependekezwa kisharia au imepokewa (katika sharia)?" Yeye alijibu kwa kauli yake: "Inafanywa kwa kutaraji wakati wa tahayari na kutoelemea katika dhana yoyote baada ya kutafakari na kutaka ushauri."[62] Kama alivyojibu Sheikh Tabriziy (r.m) kuhusu swali aliloulizwa: "Kati ya aina za istikhara ni ipi iliyothibiti kuwa ni mustahabu?" Akajibu kwa kauli yake: "Haijathibiti Sunnah ya istikhara, lakini kuna riwaya juu yake, nayo ni mujarabu."[63]

Na mwisho hakika mimi naafikiana na Allamah Twabatwabai katika rai yake kwamba kazi ya istikhara ni kumaliza hali ya kusitasita kwa mwanadamu tu, bila ya kumaanisha hilo kwamba ni matokeo ya kufichua maslahi au kheri. Ni kama mwanadamu anavyoweza kumaliza kusitasita kwake kwa njia ya kutafakari kwake au kwa kumshauri yeyote.

Anasema Sayyid Twabatwabai katika *al-Mizan*: "Hakina lolote kitendo hiki (*istikhara*) isipokuwa kuainisha kufanya au kuacha, bila ya kuwa (kitendo hiki) ni wajibu wala haramu, wala si hukumu yoyote nyingine ya taklifu (Si Suna wala sio makruhu), wala haifichui ambayo yako nyuma ya pazia la ghaibu miongoni mwa kheri au shari, isipokuwa kheri ya mwenye kufanya istikhara ni kupata uamuzi wa kufanya au kuacha, na hivyo kutoka katika tahayari na kusitasita.

Ama yale ambayo yanahusiana na kutenda au kuacha miongoni mwa matukio huenda yakawa na kheri, na huenda yakawa na

[62] Sayyid Ali Sistaniy katika *al-Fiqihi Lilimughitaribiina*, Mas'ala 598, Chapa ya kwanza 1425 Hijiria (al-Baharain Daru Kumail), Uk. 344.

[63] Abu al-Qasim al-Musawiy al-Khuiy katika *Swiratwa Najaati fiy Ajuwibati al-Istiftaati*, Juz. 1, Mas'ala 1534, Chapa ya pili mwaka 1416 Hijiria (al-Kuwait: Maktabatu al-Fiqihiyah), Uk. 553.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 123 8/27/2015 2:17:32 PM

shari, kama vilevile ambavyo angeacha au kufanya kwa sababu ya kutafakari au kwa kutaka ushauri, hivyo yenyewe (istikhara) ni kama vile kutafakari na kutaka ushauri, ni njia ya kuondoa tahayari na kusitasita wakati wa kutenda, na matokeo ya kitendo alichokichagua ni yale yale kama ambavyo angekuwa amechagua hilo kwa kutafakari au kwa kutaka ushauri."[64]

**Anwani ya Mtunzi:**
Al-Mamlakatu al-Arabiyah Saudiyah
S.L.P. – 1322, Qatif 31911,
SAUDI ARABIA.

[64] *Al-Mizan Fiy Tafsiril- Qur'ani*, Juz. 6, Uk. 118.



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 124 8/27/2015 2:17:32 PM

## ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu Ya Kwanza Mpaka Thelathini
2. Uharamisho Wa Riba
3. Uharamisho Wa Uwongo Juzuu Ya Kwanza
4. Uharamisho Wa Uwongo Juzuu Ya Pili
5. Hekaya Za Bahlul
6. Muhanga Wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo Iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab Vazi Bora
9. Ukweli Wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu Imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini Katika Swala
16. Misingi Ya Maarifa
17. Kanuni Za Ndoa Na Maadili Ya Familia
18. Bilal Wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi Wa Historia Ya Uislamu Na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an Na Hadithi
24. Elimu Ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu Ya Shia
26. Ukusanyaji Na Uhifadhi Wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo Kutoka Katika Qur'an
29. Uislamu Mfumo Kamili Wa Maisha Ya Kijamii
30. Mashukio Ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu Kwa Mujibu Wa Kitabu Na Sunna.
34. Haki Za Wanawake Katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu Na Sifa Zake
36. Kumswalia Mtume (S)
37. Nafasi Za Ahlul Bayt (A.S)
38. Adhana

39. Upendo Katika Ukristo Na Uislamu
40. Tiba Ya Maradhi Ya Kimaadili
41. Maana Ya Laana Na Kutukana Katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka Juu Ya Khofu
43. Kukusanya Swala Mbili
44. Bismillah Ni Sehemu Ya Qur'ani Na Husomwa Kwa Jahara
45. Kuwaongoza Vijana Wa Kizazi Kipya
46. Kusujudu Juu Ya Udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (S)
48. Tarawehe
49. Malumbano Baina Ya Sunni Na Shia
50. Kupunguza Swala Safarini
51. Kufungua Safarini
52. Umaasumu Wa Manabii
53. Qur'an Inatoa Changamoto
54. As-Salaatu Khayrun Mina -'N Nawm
55. Uadilifu Wa Masahaba
56. Dua E Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu Wa Binadamu
58. Umaasumu Wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu Wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu Wa Mitume - Umaasumu Wa Mtume Muhammad (S)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu Ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu Ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu Ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu Ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu Ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu Ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu Ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu Ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala Ni Nguzo Ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora Wa Imam 'Ali Juu Ya Maswahaba Na Ushia Ndio Njia Iliyonyooka
75. Hukumu Za Kifikihi Zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-U-Llaah
77. Muhammad (S) Mtume Wa Allah
78. Amani Na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani Na Mtume Muhammad (S)

81. Mitala Na Ndoa Za Mtume Muhammad (S)
82. Urejeo (Al-Raja'a )
83. Mazingira
84. Utokezo (Al - Badau)
85. Hukumu Ya Kujenga Juu Ya Makaburi
86. Swala Ya Maiti Na Kumlilia Maiti
87. Uislamu Na Uwingi Wa Dini
88. Mtoto Mwema
89. Adabu Za Sokoni
90. Johari Za Hekima Kwa Vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu Ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu Ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu Ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi Katika Usunni Na Ushia
96. Hukumu Za Mgonjwa
97. Sadaka Yenye Kuendelea
98. Msahafu Wa Imam Ali
99. Ngano Ya Kwamba Qur'ani Imebadilishwa
100. Idil Ghadiri
101. Kusoma Sura Zenye Sijda Ya Wajibu
102. Hukumu Zinazomuhusu Mkuu Wa Kazi Na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kumsalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Ndoa ya Mutaa
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 127 8/27/2015 2:17:32 PM

123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu
135. yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur’an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur’an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur’ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu

165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Upotoshaji dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina ('as) na Makhalifa
197. Uongozi na Utawala katika Mwenendo wa Imam 'Ali ('a)
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni wa Kisunni na Mwanachuoni wa Kishia (*Al-Muraja'aat*)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Mjadala wa Kiitikadi



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 129 8/27/2015 2:17:32 PM

206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza
213. Imam Ali na Mambo ya Umma
214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
215. Mwanamke na Sharia
216. Mfumo wa Wilaya
217. Vipi Tutaishinda Hofu?
218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo
219. Mahali na Mali za Umma
220. Nahjul-Balagha – Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala, Mawaidha na Semi za
Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)
221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Husein (as) hapo Karbala
222. Uimamu na Tamko la Kutawazwa
223. Imam Husain ni Mfumo wa Marekebisho na Mageuzi
224. Saada Kamili – Kitabu cha Kiada cha Maadili
225. Maeneo ya Umma na Mali Zake
226. Imam Hasan na Mfumo wa Kujenga Jamii
227. Adhana ni Ndoto au ni Wahyi?

## KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba'Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi

## ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION KWA LUGHA YA KIFARANSA

1. Livre Islamique



05_15_Utamaduni wa mwamko_27_August_2015.indd 130 8/27/2015 2:17:32 PM